# Kuhuzunika na Kuomboleza

## Harakati za Bibi Zainab

Kimeandikwa na:
**Sayyid Jawad Naqvi**

Kimetarjumiwa na:
**Dk. Mohamed Salehe Kanju**

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 512 - 80 - 5**

Kimeandikwa na:
**Sayyid Jawad Naqvi**

Kimetarjumiwa na:
**Dk. Mohamed Salehe Kanju**

Kimepangwa katika Kompyuta na:
**Hajat Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Octoba, 2010
**Nakala: 1000**

Kimetolewa na kuchapishwa na:

**Alitrah Foundation**

P.O. Box 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Fax: +255 22 2127555

Email: alitrah@raha.com

Website: www.alitrah.org

Online: www.alitrah.info

**Kwa kushirikiana na:**

Al-Mustafa International University,
S.L.P. - 3616
Dar es Salaam.
Tanzania
Barua pepe: Tanzania@miu.ac.ir
na:Info@miu.ac.ir
Tovuti: www.miu.ac.ir

# YALIYOMO


## Sura ya Kwanza:

Azadari kuhuzunika na kuomboleza)..........................................2

Azadari - Harakati ..........................................................................5

## Sura ya Pili:

Ujumbe wa Ashura.......................................................................23

## Sura ya Tatu

Hamasa- Husein..........................................................................37

## Sura ya Nne

Msimamo (istiqamat) somo kutoka karbala................................62

**Khutba ya Mina -** Imam Husein (a.s)....................................................89

**“Yeye Ndiye aliyempeleka Mtume katika watu wasiojua kusoma anayetokana nao, akiwasomea Aya Zake na akiwatakasa na akiwafunza Kitabu na hekima, na ingawa zamani walikuwa katika upotovu ulio wazi.” (Sura al-Baqara: 129)**

# UTANGULIZI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni kazi nyingine nzuri ya Ustadh **Seyyid Jawad Naqavi**. Tukio la Karbala na Ashura ambalo ni bahari yenye lulu zake zilizowekwa ndani kwenye kina, zinaweza tu kugunduliwa na wale ambao wamelainishwa kabisa kwa fikra za Imamu Khomein (r.a) na kufanya mapinduzi ya marekebisho ya moyo wa kijamii katika jamii ambayo imeathiriwa na maradhi ya kijamii na ya vikundi mbali mbali vya kijamii. Huu ulikuwa ujumbe wa Imamu Husein (a.s), njia ya Kiongozi wa Mashahidi (wahanga) na hali halisi ya safari ya mateka kutoka Karbala kwenda mji wa Kufa, na kutoka Kufa mpaka Syria. Safari hii ya shujaa dada yake Husein Ibn Ali (a.s) aliibadilisha kuwa harakati ambayo ilionekana kama iliyolengwa kubadilishwa kuwa kama safari ya mateka masikini, wanyonge na wachovu. Hutuba za Bibi Zainab (as) zilizopakwa rangi ya damu ya Husein na masahaba zake watukufu iliutikisa umma na ufalme wa Yazid. Ilikuwa ni juhudi za watoto wa Fatima na Ali (as) – Husein na Zainab (as) - ambazo zimeifanya Karbala kuwa Hamasa ya kudumu na kuvunja majaribio yote katika zama tofauti ya kubadilisha tukio hili kuwa ugomvi wa kifamilia au tukio linalofaa tu kufanyiwa kumbukumbu, kupatisha thawabu na kafara la dhambi.

Kitabu hiki ni tarjuma ya makala tatu zilizoandikwa na **Ustadh Syed Jawad Naqvi** katika jarida lake linalotoka kila baada ya miezi miwili; *bi-monthly magazine Mashrabe Naab* la mwezi wa Muharram – Safar. Vilevile kitabu hiki kina sura ya mwisho ambayo ni moja ya tarjuma ya hutuba nyingine. Sura zote nne katika kitabu hiki zimelenga katika kumuamsha msomaji na kufanya maumivu katika moyo wake kuelekea kwenye mateso katika zama yake ambayo ni kioo cha taswira ya kile

ambacho kilitokea wakati wa Imamu Husein (a.s). Chini ya mwanga wa hatua za Imam Husein, maneno na tabia yake, kitabu hiki humshawishi msomaji kwamba wakati hali inayokuzunguka ni sawa na ilivyokuwa wakati wa Husein Ibn Ali (as) na Zainab bint Ali (as), basi na wewe vilevile unahitaji kuonesha tabia kama ile ile iliyooneshwa na watu wa Karbala.
Hakuna uhalali au sababu yoyote ambayo itakubaliwa kwa ajili ya kukaa kimya bila kufanya chochote wakati watawala madhalimu wanatawala jamii, wakati maziwa na mito ya maji inapobadilika kwa damu za watu wasio na hatia.

Sura ya kwanza ya kitabu hiki ambayo ni mada ya kitabu hiki huelezea na kufichua asili halisi ya Azadari ambayo ni harakati ya haki kuelekea kwenye kuiangamiza dhulma na ukandamizaji. Katika sura ya pili, ambayo imepewa jina la "**Ujumbe wa Ashura**" ambao kama haukueleweka unakuwa chanzo cha msingi cha kudorora na ukosefu wa harakati. Sura ya tatu juu ya "*Hamasa-e-Husein*" huwasilisha jina halisi la somo la tukio la Karbala ambalo limekuwa lenye kuathiriwa na upotofu na limegeuka kuwa kitu kingine mbali na kitu kinachohusika na harakati. Sura ya nne ina habari kama zile zile za sura ya tatu lakini pamoja na uchambuzi wa kihistoria na mazingira ambayo yaliwafanya watu wapoteze matumaini na kuwa chini ya shinikizo lenye matokeo ya ukimya.

Kitabu hiki ni johari nyingine na ni kazi ambayo haiishii kwa Mashia tu, bali ni kitabu cha *Umma* wote wa Kiislamu, na kwa kweli kwa wale wanadamu wote ambao wana maadili fulani yaliyo hai ndani yao.

Namshukuru sana Allah (s.w.t) mara nyingine tena kwa kunibariki kwa fursa hii kubwa kuwa njia ya kufikisha ujumbe huu wa haki, wenye kuamsha harakati kwa jumuiya ya wazungumzaji wa Kiingereza (na sasa kwenye jumuiya ya wazungumzaji wa Kiswahili).

"Ewe Allah! Wakati wowote kama kuna haja ya huduma kwenye dini Yako, nipe kipaumbele na nifanye mimi wa mbele zaidi kama njia ya kufikisha." Imam Sajjad (a.s).

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 3

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, *AZADARI (Mourning and Lamentation)* kilichoandikwa na Sayyid Jawad Naqvi. Sisi tumekiita, *Kuhuzunika na Kuomboleza.*

Kitabu hiki ni tarjuma ya makala tatu zilizoandikwa na Ustadh Sayyid Jawad Naqvi katika jarida lake linalotoka kila baada ya miezi miwili - *Mashrabe Naab*, toleo la mwezi wa Muharram–Safar.

Maana ya *azadari* – ni kuomboleza. Kiistilahi, ni mkusanyiko wa watu wanaokusanyika sehemu moja iliyoandaliwa kwa ajili ya kumbukumbu na kuomboleza ushahidi, hasa wa Imam Husain AS (*‘**A**layhi ‘s-**S**alaam*: amani iwe juu yake). Katika mkusanyiko huo (ambao ni maarufu kwa jina la “majlis”) hutolewa hutuba za kuwahamasisha waumini kuendeleza harakati aliyoianzisha Imam Husain AS ya kupambana dhidi ya watawala madhalimu na mafisadi ambao ni kikwazo cha maendeleo na ustawi wa jamii. Mwanzilishi wa azadari hii ni dada yake Imam Husain, yaani Bibi Zainab AS, ambaye alitoa hutuba ya kwanza kabisa kuhusu masaibu ya Karbala mbele ya mkusanyiko mkubwa wa watu katika baraza ya Yazid na mbele ya Yazid mwenyewe. Kwa ujasiri mkubwa alitoa hutuba ambayo iliuliza umati ule wa watu waliokuwepo pale kiasi kwamba hata Yazid mwenyewe alinywea na kutahayari. Na kutokana na hotuba hii kali, Yazid aliamuru wafungwa hawa akiwemo Bibi Zainab na mdogo wake Ummu Kulthum, Imam Ali Zainul Abidin (Sajjad) mwana wa Imam Husain AS na kina mama wa familia za mashahidi wa Karbala, wafunguliwe minyororo waliyofungwa na watayarishiwe safari ya kurudi Madina.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana , hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Dk. M. S. Kanju kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni changamoto kubwa kwa wasomaji wetu.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam**

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 1

بسم الله الرحمن الرحيم

# SURA YA KWANZA

## Azadari
## (Kuhuzunika na kuomboleza)
## Harakati ya Bibi Zainab (a.s.)

Allah *Azza wa Jallah* amewajalia Waislamu na hususan Waislamu Mashia neema mbalimbali na fursa ambazo kwamba tunakosa utambuzi wake (*Maarifa*). Kwa ajili ya kukosa utambuzi hatujui thamani ya neema hizi na kwa matokeo yake hatufaidiki na athari za neema hizi juu yetu. Neema kubwa kuliko zote ni kwamba Allah *Aza wa Jallah* ametujaalia sisi utambuzi wa dhati Yake na kutufanya tuamini katika Mungu, kwa kuwasilisha uthibitisho wa umoja Wake kwetu, ametufanya sisi ni wenye kuamini na kuabudu Mungu Mmoja, kwa kutufundisha njia za ibada Yake, amejaalia waabudu (kupatikana), upole na ukarimu Wake umetuongoza sisi kwa taa ya Utume, ametupa sisi dini halisi ya Uislamu, ameteremsha Kitabu – Qur'ani Tukufu - , ametufanya sisi kuwa wafuasi wa Mtukufu Mtume (s.a.w), na ametujaalia mapenzi na utiifu kwa kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w), na mbali na haya kuna maelfu ya neema nyingine tulizopewa ambazo hatuna habari nazo kabisa na kwa hiyo hatuna shukurani kwa neema hizo; lakini bado Allah *Aza wa Jallah* hakututupa katika neema hizi. Allah ametupa maelfu ya fursa; ambazo umuhimu na ubora wake hatuujui kwa sababu hatunufaiki kwa fursa hizi tulizopewa ingawa baadhi ya fursa hizo ni zenye kutosheleza haja ya kuifanya Akhera yetu kuwa nzuri.

Moja ya neema miongoni mwa hizi ni Azadari (mikusanyiko ya huzuni na kuomboleza) ya Kiongozi wa mashahidi (a.s) ambaye Waislamu wengi hawana ujuzi naye, baadhi wamekuwa waathiriwa wa mashaka na uzushi, na kwa huzuni kubwa kabisa kuna wachache ambao kwa ajili ya ujinga wamekuwa maadui wa Azadari. Hata wale ambao wamekubali na kuitekeleza Azadari na wao vilevile hawana ujuzi sawasawa wa uhalisi wake na hawatambui hadhi na cheo chake kitukufu. Fursa, muda wa ziada

na neema hupotezwa kwa sababu ya utovu wa shukurani, na adhabu kwa ajili ya matendo kama hayo kutoka kwa Allah ni kali sana kwa sababu hasara inayotokana na upotezaji wa fursa hii ni ya juu sana hususan kwa fursa zile ambazo kupatikana kwake kumetokana na juhudi kubwa, mihanga na shida. Allah *Aza wa Jallah* havumilii uzembe na wingi wa neema hizo ambazo kwazo mtaji mkubwa umetumika.

Fursa ya Azadari haikuja kwetu kwa urahisi; kwa hili mtaji mkubwa wa ulimwengu umetumika; kwa hili watakatifu kabisa wa wanadamu wamepatwa na misiba isiyofikirika kutoka kwenye mikono ya wanadamu wachafu kabisa, waovu.

Kama utambuzi wa Azadari unapatikana, basi mtu kuwa Azadar kamwe hakutachukuliwa kama dosari, bali itakuwa ni kitu kitukufu. Hapo ndipo Azadar atatambua ukweli halisi ambao kwamba amejihusisha nao, na vilevile atafahamu kuhusu majukumu yake. Kiwango chochote cha uoneshaji wa shukurani utachukuliwa kama pungufu kwa wale ambao wamepokea fursa hii kubwa ya Azadari – na Mungu aepushilie mbali – kama wanakuwa sababu ya madhara yoyote kwa Azadari, hivyo hakutakuwa na jinai kubwa kama hii. Ni muhimu kufahamu kwamba mwanadamu hawezi kutekeleza haki ya kitu chochote bila utambuzi wake; bila utambuzi tendo haliwezi kufikia lengo lake na haliwezi kuwasilishwa katika njia ambayo inatakiwa kuwasilishwa.

Amma kwa matendo bila utambuzi, Imamu Ali (a.s) anasema:

**قصم ظهري عالم متهتّك و جاهل متنسّك**

“Watu wawili wameuvunja mgongo wangu; Mwanachuoni bila matendo na mjinga afanyaye matendo.”

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 4



Ali (a.s) anasema kwamba; wote, mwanachuoni ambaye ana ujuzi lakini haifanyi elimu yake kuwa ya matendo na yule mtu mjinga ambaye anafanya matendo lakini bila ujuzi na utambuzi wameuvunja mgongo wangu. Maana ya kuuvunja mgongo wa Imamu ni kuvunja mgongo wa dini. Matokeo ya matendo haya yote ya mwanachuoni bila vitendo na vitendo bila ujuzi yako sawa; yaani yote huwa ni sababu ya kuidumaza dini, kuwaweka watu mbali na dini na kuvunja migongo ya Viongozi. Kitendo chochote kinachofanywa kwa utambuzi, hutoa matokeo (mazuri) wakati ambapo hata kwa maisha yote kama kitu kinafanywa bila utambuzi, hakitoi matokeo mazuri. Kama rakaa mbili zinaswaliwa kwa utambuzi zitatoa matokeo, wakati ambapo kama sijda inafanywa kwa maisha yote bila utambuzi haitatoa matokeo yoyote. Kama mwenye utambuzi akiiangalia tu Ka'ba Tukufu atapata matokeo wakati ambapo mtu ambaye hana utambuzi hata akifanya tawafu kuizunguka Ka'ba Tukufu kwa maisha yake yote, hatapata matokeo. Halikadhalika kama Azadari inafanywa kwa utambuzi itatoa matokeo, lakini kama ikifanywa bila utambuzi itakuwa haina athari yoyote.

Hivyo kila kitendo lazima kifanywe kwa utambuzi; tokwa na machozi lakini pamoja na utambuzi, piga kifua chako lakini pamoja na utambuzi; soma tenzi za huzuni na mashairi ya maombolezi lakini pamoja na utambuzi, soma sifa za Ahlul Bayt (a.s) lakini pamoja na utambuzi na andaa Majalis na khutba za misiba lakini pamoja na utambuzi. Shughuli zote hizi lazima ziwe pamoja na utambuzi, na kama matendo yanafanywa pamoja na ujuzi sahihi na utambuzi, basi hakuna mtu atakaye kupokonya haya, lakini kama yanafanywa bila utambuzi, basi mtu yeyote anaweza kukupokonya kwa kufanya mashaka kidogo tu kuhusu vitendo vyako, wakati mwingine kwa hila, wakati mwingine kwa upotoshaji na wakati mwingine kwa kukufanya wewe ulale usingizi. Kama mtu akilala, basi mazuri yake yote yako hatarini na kwa kawaida watu huibiwa wakiwa wamelala. Wale ambao wanalala kwenye viwanja vya ndege na kwenye stesheni za reli mizigo yao hupotea na wakati wakiamka wanakuta kwamba wameibiwa na kuna baadhi ya wapumbavu wanaweza wakajisikia furaha kwamba sasa hawahitaji kube-

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 5



ba mizigo yao.

Iqbal ana malalamiko haya kutoka kwenye jamii yake. Allama Iqbal anasema: “Ole juu ya wenye kushindwa! Bidhaa za msafara zilikuwa zinapotea. Na msafara unaendelea kupoteza hisia za hasara hiyo.”

Inasikitisha kwamba bidhaa za msafara zilikuwa zinapotea, lakini baya zaidi ya hili inasikitisha mno kwamba msafara hata hauhisi kwamba bidhaa zao zinapotea.

Azadari ni desturi ya bimkubwa Zainab (a.s) na desturi hii kubwa ina kadiri mbili; kadiri moja ni ile ya faida zake na kadiri ya pili ni ile ya madhumuni ndani yake. Faida ya Azadari ni thawabu lakini madhumuni ya Azadari ni kitu kingine. Tunahitaji kuja na kuelekea kwenye madhumuni ya kuhuzunika na kuomboleza ambako hutufikisha kwenye ibada na dini. Hata kama hatukusudii kupata thawabu bado tunapata thawabu, lakini lengo haliwezi kupatikana mpaka tukusudie kwalo. Lengo lenyewe humaanisha kitu ambacho pamoja na nia na haliwezi kupatikana bila nia. Thawabu zaweza kupatikana bila utambuzi, lakini lengo haliwezi kupatikana bila utambuzi.

**Azadari – harakati:**

Desturi ya Azadari (kuhuzunika na kuomboleza) ni harakati. Azadari katika asili yake, kuwepo na uhalisi wake ni harakati. Harakati ni kukifanya kitu kiwe katika hali ya mwendo. Hii humaanisha kwamba kama kitu kina mwendo wa ufanyaji kazi na kimeacha kufanya kazi yake na kudorora, kitu fulani kingine kikaja na kukifanya kuwa katika mwendo, basi hiyo hujulikana kama harakati, Allah *Aza wa Jallah* amemfanya mwanadamu katika hali ambayo kwamba lazima aendelee katika hali ya harakati na harakati hii ni ya kuelekea kwenye utukufu wa Mungu. Qur’ani Tukufu imemuelezea mwanadamu kama mhamiaji kuelekekea kwa Allah:

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 6



يَـٰٓأَيُّهَا ٱلْإِنسَـٰنُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَـٰقِيهِ ﴿٦﴾

**"Ewe Mtu! Hakika wewe ni mwenye kufanya juhudi (harakati) kwa Mola wako, juhudi (harakati) ambayo utaikuta." (84:6)**

Maisha ya mwanadamu yako katika harakati; kama harakati ikisimama mwadamu hufariki. Kama harakati ya moyo ikisimama mwili hufa. Hii ni harakati moja ambayo kama ikisimama mwanadamu hufariki, lakini kuna harakati kadhaa za aina nyingine ambazo vilevile zina matokeo ya aina tofauti ya vifo. Ukimya, utuliaji na udororaji vilevile ni vifo. Hii humaanisha kwamba kama harakati ya moyo inasimama, basi ni kifo, na roho ya mwanadamu vilevile iko katika hali ya harakati ambayo nayo ikisimama basi hiki ni kifo. Halikadhalika jamii ya mwanadamu vilevile iko hai kwa sababu ya harakati, na jamii vilevile hufa kama harakati ikisimama. Umma vilevile uko hai kwa sababu ya harakati na kama harakati ikisimama basi umma vilevile hupatwa na kifo. Dini na itikadi vilevile ziko hai kwa sababu ya harakati, na bila harakati dini vilevile hufariki. Ulimwengu wa uhai vilevile huishi kwa sababu ya harakati na bila ya harakati ulimwengu mzima ungeangamia. Udororaji na ukimya vyenyewe ni majina mengine ya kifo. Maji ni mfano mzuri wa kuelewa uhusiano wa harakati na maisha na udororaji na kifo.

Maji ambayo ni elementi ya msingi wa kuishi kwa kila kitu yenyewe yako hai kwa sababu ya harakati. Kama harakati ikisimama maji vilevile hufariki. Maisha ya maji yako kwenye kutiririka kwake, yanakuwa hai wakati wote yanapotiririka, kama yakisimama hufariki. Maji yaliyotuama (kudorora) huitwa dibwi lilotuama au hori ambalo kwalo maji ya mvua, maji ya mafuriko na vijito vichafu vya maji humiminikia humo lakini hakuna njia ya kutokea. Kwa vile hakuna njia ya kutokea maji yale yaliyojikusanya hufariki. Uajemi kuna jina sahihi kwa hali hii, huitwa "*Murd-Aab*" yaani maji yaliyokufa. Katika maji haya hakuna maisha au uhai; kwa kweli kama maji haya atapewa mtu kunywa atafariki. Kama maji yaliyok-

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 7



ufa yatapewa kwa kiumbe hai hukiuwa vilevile kiumbe kile hai. Alama za maji yaliyokufa ni kuwepo kwa aina mbili za viumbe ndani yake; moja ni vyura na cha pili ni ruba.

Ruba ni mdudu anayeishi katika madibwi yaliyotuama na mahori machafu, mdudu ambaye kazi yake ni kung'ang'ania kwenye miili ya wanyama na viumbe wengine na kunyonya damu zao. Inasemekana kwamba mdudu huyu mdogo ana uwezo wa kunyonya damu mara kumi ya uzito wake na wakati mwingine hutumika kunyonya damu chafu kutoka kwenye miili ya wanadamu. Kazi ya chura ni kusema na kupiga makelele. Kazi yake kubwa ya kuwepo kwake ni kufanya makelele na sauti zisizo na maana. Wakati wowote viumbe hawa wawili wanapoonekana kwa wingi basi maji hayo kwa hakika yamekufa.

Mfano wa jamii ya mwanadamu vilevile unafanana; kama kuna harakati iko hai, kama ikijielekeza kwenye odororaji basi inakufa. Jamii iliyokufa ni kama dibwi la maji machafu ambalo huzalisha ruba, vyura wadudu wenye madhara na vijidudu viini vya maradhi. Uhalifu ni mwingi sana katika jamii zilizokufa, dhulma na uchafu wa maadili ni jambo la kawaida katika jamii iliyokufa, soko la uovu liko juu, wizi na udanganyifu ni jambo la kawaida, mauwaji ya watu maarufu, mauwaji na ugaidi huwa ni kitu cha kawaida, na juu ya haya yote kuna wale walaghai ambao hunyonya damu ya jumuiya zilizokufa na hivyo kuzifanya jumuiya hizo kuwa dhaifu na wao wenyewe kustawi. Jamii hii huzaa mfumo wa tabaka na kwa sababu ya hilo ruba wachache huwa wamiliki wa mitaji yote, utajiri na rasilimali zote. Ukabaila ni urithi wa jamii zilizokufa. Katika mfumo wa kikabaila damu yote ya jamii inanyonywa na mtu wa kawaida hawezi hata kupata mahitaji yake ya kila siku na hivyo uwezo wa harakati hufikia mwisho.

Qur'ani Tukufu imeanisha utajiri na rasilimali kama njia za harakati kwa ajili ya jamii; hubeba hadhi ya uti wa magogo kwa ajili ya jamii. Mtu ambaye uti wake wa mgongo umevunjika hawezi kusimama na kutembea. Halikadhalika kama utajiri wa jamii unaibiwa na kuishia mifukoni mwa

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 8



mabepari wachache basi jamii nayo haiwezi kuwa katika hali ya harakati, huanguka chini, huwa dhalili na masikini. Qur'ani imeelezea hali hii kama kukanyangwa chini (*Miskin*) yaani ni wakati jumuiya inapobadilika kuwa chini na haitaki kuingia kwenye harakati. Wakati mabepari wanakusanya utajiri kwa ajili ya vizazi vyao kumi vijavyo, kizazi kilichopo cha umma hakipati chakula na maji ya kutosha. Utajiri ambao unaibiwa kutokana na mahitaji ya msingi ya watu unatumika katika anasa na ufujaji mkubwa wa mali unaofanywa na mabepari na makabaila. Watu wa jamii ile ambao hawana uwezo wa kupata mahitaji yao ya kila siku hupoteza uwezo wao wa harakati na maasi; mawingu ya kifo siku zote yanagonga kwenye vichwa vyao; udhalili na umasikini vimekuwa ndio majaaliwa yao. Hali hii ikijitokeza katika jumuiya basi hali hiyo haiishi kwa urahisi, kwa kweli huendelea kwenye kizazi kijacho. Watoto wa ombaomba nao vilevile ni ombaomba na watoto wa makabaila nao vilevile ni makabaila. Leo nchi nyingi za Waislamu na watu ni masikini wa kutupwa kwa sababu hii; wamerithi umasikini kutoka kwenye kizazi chao kilichopita.

Viumbe wengine kama ruba na vyura wanapatikana katika jamii iliyodorora. Katika jamii iliyotuama na kudorora watu ambao huzungumza tu sana hupatikana kwa wingi sana lakini hawana tabia za busara. Wanasiasa wanatosheka kwa kutoa tu kauli badala ya kufanya siasa za busara. Watawala hawachukui hatua yoyote na kuwafanya watu wajinga na kuwapa ahadi za uwongo. Viongozi wa dini vilevile wanatosheka kwa maneno makubwa na hutuba zisizo za kiroho. Wasomi wajuzi huchukulia ukosoaji kuwa unatosha, ambapo kwamba watu huibua tu misemo ya kaulimbiu. Zote hizi ni sifa za vyura ambazo huzipata katika maisha yake katika dibwi.

Kuna madai makubwa hufanywa katika jumuiya zisizo na harakati na zilizodorora lakini matendo hakuna. Kila mahali wadai huonekena lakini wote hawana unyofu katika madai yao. Baadhi wanadai kuwa wao ni washika bendera (au viongozi) wa jumuiya, baadhi wanadai kuwa wao ni wachamungu sana, baadhi hudai kuwa wanao uwezo mzuri zaidi, baadhi

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 9



hudai kwamba wana unyofu wa hali ya juu, baadhi wanadai kuwa watumishi wa jumuiya, baadhi wanadai kuwa watu wa dini sana, baadhi kama wazalendo lakini nyuma ya madai haya matupu na yasiyo ya kimoyo si chochote bali ni uwongo, udanganyifu, ulaghai na unafiki. Kama watu wakidanganyika kwa hutuba na madai haya, na kujisikia raha kwamba mazingira yao yatabadilika kwa maneno haya, basi mbali na kuwa ndoto si chochote. Hii ni kama kumsumbua mtu ambaye anajisikia raha kwa kusikiliza kelele za vyura na kufikiria kwamba kundi kubwa linakuja kumsaidia. Vyura wa kisiasa za kidini hawawezi kutegemewa kwa uhai wa jumuiya yoyote.

Katika maji yaliyotuama na yasiyo na harakati kuna viumbe wengine hatari sana wanaopatikana humo ambao hawaonekani kwa macho na ili waonekane huhitajika darubini. Viumbe hawa ni viini vya maradhi ambavyo hueneza magonjwa. Lazima tuelewe kwamba viini hivi huzaliwa katika mazingira machafu na katika maji yaliyotuama. Kuna aina mbili za viini vya maradhi; kundi moja linaitwa Bakteria na kundi lingine huitwa virusi, vyote hivi hueneza magonjwa lakini njia zao za kushambulia ni tofauti. Bakteria hungia mwilini na kushusha chini nguvu za mwili, huzuia chakula kuingia mwilini na zenyewe hukifyonza chakula hicho au hukiharibu. Njia ya kushambulia ya virusi ni tofauti; huingia mwilini na kuharibu mfumo wa mwili. Huchukuwa uendeshaji wa shughuli mbalimbali za mwili, na hii ndio sababu ambayo hufanya ugumu zaidi kutibu magonjwa yanayosababishwa na virusi.

Viini hivyo vya maradhi huzaliwa ndani ya jumuiya na jamii zilizokufa halikadhalika. Baadhi ya hizo ni kama bakteria wanaoeneza magonjwa ya kijamii na ya vikundi katika jamii, ambapo baadhi ni kama virusi ambavyo huifanya jamii idumae. Wale ambao huchukua hongo hufanya kama bakteria. Wezi, wanyang’anyi na majambazi huzuia au huharibu nguvu za jamii, lakini wale wanaoingia ndani ya vituo nyeti na vyama muhimu vya jumuiya na kudhibiti mfumo wa kijamii ni virusi vya kijamii. Wanapata vyeo vya kisiasa, vya kijumuiya, vya kielimu, vya kidini na vya kiuta-

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 10



maduni na kuifanya jumuiya yote kudumaa. Jumuiya na jamii zilizokufa ni waathirika wa majanga haya.

Swali muhimu linalokuja hapa ni kwamba jamii au jumuiya inapokufa na kupatwa na magonjwa yote haya kwa sababu ya kudorora na ukosefu wa harakati basi vipi itaokolewa jamii hii? Vipi watapata ukombozi? Watu mbalimbali na vikundi wamejibu swali hili. Wanafikra wa kijamii wengi wamefariki na wamewasilisha maoni mbalimbali na taratibu za jinsi ya kutoa ukombozi kwa wanadamu. Kila mtu amefikiria kwa akili yake mwenyewe na chochote walichokifikiria kwa njia hii na juhudi zao hushukuriwa, lakini maoni na fikra hizi haziwezi kamwe kuleta uhai kwenye jumuiya zilizokufa. Ili kuhuisha jumuiya iliyokufa, kwanza lazima tuangalie ni kwa nini imekufa? Jamii hufariki wakati harakati ndani yake inaposimama. Kama kukosekana kwa harakati ndio sababu ya kifo chake, basi ili kuihuisha tunahitaji kujenga harakati ndani yake; na mara inapoingia katika harakati, polepole itapata uhai ndani yake.

Ni sawasawa na kinachofanywa wakati moyo unaposimama kupiga. Wakati moyo uposimama kupiga au ukiwa dhaifu, basi njia mbalimbali hufuatwa kuurudishia uhai wake; kama vile kupumua kwa kutumia vyombo, kifua kuminywa ili kuufanya moyo urudie hali yake ya harakati. Wakati moyo unapoanza kupiga dalili za uhai huwa dhahiri; na kila mtu hutabasamu, kwa sababu moyo kupiga ni dalili ya uhai na kuishi. Kwa moyo kuanza kupiga tena mgonjwa hupata maisha mengine na uhai wake kuwa umerudishwa. Lakini ni nini kifanyike wakati umma unapofariki? Vilevile umma hufariki kwa sababu ya kukosa harakati. Hivyo ili kuurudishia uhai umma uliokufa tunahitaji kuleta harakati ndani yake ili kwamba udororaji na ukimya wa umma uweze kuvunjwa. Ukimya wake lazima uvunjwe na mawimbi ya hekaheka lazima yaanzishwe ndani ya umma huo. Lazima ugeuke kuwa wa mafuriko na lazima litengenezwe tufani ndani ya maji haya yaliyotuama.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 11



Njia ambayo kwa ubora kabisa Allamah Iqbal ametambua ugonjwa wa umma na ametoa utaratibu kwa ajili ya ukumbozi wake. Katika rai ya Allamah Iqbal, ugonjwa wa umma ni kwamba harakati ndani yake imesimama, na kwa ajili hiyo umma huu umekufa na kwa hiyo kuna haja ya kuurudisha kwenye uhai wake. Allamah Iqbal anasema katika *Zarb-e-Kalim:*

"Moyo uliokufa sio moyo tena; urudishe tena kwenye uhai. Kwani hii ndio tiba ya ugonjwa wa umma. Bahari yako imetulia, huu ni utulivu au ni uchawi? Wala samaki wakubwa hamna, na hamna mawimbi wala ufukwe wake hausumbuliwi. Huna ujuzi wa bara na bahari. Wala dalili dhaifu za nyotahazikufanyi uhangaike".

Moyo uliokufa sio moyo kabisa na lazima uhuishwe kwa sababu kuishi kwake kuko katika harakati (mapigo) yake. Moyo unaitwa moyo kwa sababu uko hai na unadunda; na tiba kwa ajili ya maradhi ya muda mrefu ya umma iko ndani ya hili. Asili ya maradhi ya umma ni ukosefu wa harakati ndani yake ambapo kwayo hufariki na tiba kwa ajili ya maradhi au kifo cha umma ni kuuhuisha na kurudia uhai wake. Allamah Iqbal anaiambia jumuiya yake na anasema kwamba bahari yako imetulia na sielewi iwapo ni utulivu au ni uchawi (kwa sababu bahari haiwezi kutulia), kwa sababu haina viumbe wa bahari au samaki wakubwa, sioni mawimbi yoyote au ghasia ndani yako, na pwani na fukwe yako hazina mahangaisho (yaani hazikuathiriwa na majanga).

Anachokusudia kusema Allamah Iqbal ni kwamba umma na jumuiya ni kama bahari na kuishi kwa bahari ni katika maji kupwa na kujaa na ghasia. Bahari nzuri ya kupendeza ni ile yenye tufani, mawimbi, maji kupwa na kujaa, vimbunga; lazima iwe na samaki wakubwa kama vile papa na nyangumi. Bahari ni ile ambayo kwamba fukwe zake zinahangaishwa kwa sababu ya kupigwa na mawimbi na maji kupwa na kujaa. Ukimya na utulivu ni kifo cha bahari, na bahari ambayo haina samaki ndani yake ni bahari iliyokufa; bahari ambayo kwamba fukwe zake haziguswi na zime-

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 12



tulia basi bahari hiyo imekufa. Ukimya ndani ya bahari ni dalili ya aina fulani ya uchawi, kwa sababu ni kinyume cha tabia ya bahari.

Jumuiya na umma vilevile ni kama bahari ambazo kuishi kwake ni katika harakati, matufani, vurugu na machafuko. Ukimya na udororaji ni kifo cha jumuiya. Dalili za kifo cha jumuiya ni kwamba watu wenye haiba kubwa na viongozi hawazaliwi katika jumuiya hizo, badala yake huzaliwa ruba, vyura na viini vya maradhi. Fukwe za jumuiya zilizokufa ni wapenda anasa ambao huhusika na kujirembesha na mapambo. Tabibu huyu wa umma anawaambia hao kwamba mpaka sasa bado hamna ujuzi wa siri na kina cha ndani cha upande wa anga za juu. Mvuto wa nyota hauwafanyi muhangaike. Hii ina maana kwamba leo matukio ya ulimwengu, hali na mambo mbalimbali hupeleka dalili za kuvutia kwenu, lakini hamna hisia zilizobakia ndani yenu. Ujumbe nyuma ya dalili hizi hauwaletei ndani yanu maumivu na uhangaisho.
Iqbal anawaambia wanafunzi wa umma wake:

“Allah akuingizeni katika tufani. Maji kupwa na kujaa kwa bahari yenu hakunavurugu yoyote.”

Hii ina maana ninyi ni bahari lakini bila mawimbi na kama kiasi cha maji kupwa na kujaa kinapotokea kinakuwa hakina vurugu na ghasia ndani yake, lakini badala yake mawimbi yenu hayana uhai na hayana roho. Mnakuwa hamna ari ya hali ya juu, wala kazi zenu hazina hadhi na hamkusudii kuchukua hatua yoyote kuelekea kwenye malengo makubwa na kazi kubwa.

Anasema katika *Armaghane Hijaz*:

“Kwa nini hakuna tufani katika bahari yenu,
Kwa nini sioni nafsi zenu ndani yenu, Enyi Waislamu!”
Kwa vile sasa tunafahamu kwamba tiba ya umma uliokufa ni kutengeneza harakati ndani ya umma hizo, kutengeneza matufani katika bahari zao zili-

zotulia na kutengeneza hekaheka katika mawimbi ya jumuiya zilizokufa; swali ambalo linakuja ni jinsi gani ya kutengeneza harakati hizi, tufani na kimbunga? Na ni nani anayeweza kufanya kazi hii kubwa? Jawabu kwa hili ni muujiza ambao Allah *Aza wa Jallah* aliompa Nabii Isa (as) kupulizia uhai katika miili iliyokufa. Nabii Isa kwa amri ya Allah alikuwa anarudisha uhai kwa mtu ambaye mwili wake umekufa na ambaye moyo wake umesimama. Hivyo tunaweza kusema kwamba Allah amemfanya mwana wa Mariam (as) mkombozi wa miili iliyokufa; halikadhalika Allah Aza wa Jallah vilevile ametengeneza mkombozi kwa kupulizia roho ndani ya jumuiya zilizokufa na umma zisizo na uhai. Muujiza wa mkombozi huyu ni kurudisha uhai kwenye jamii zilizokufa na kupulizia roho ndani ya jumuiya zilizokufa. Jina la mkombozi huyu ni Mwana wa Zahra (as); Husein ibn Ali (as).

Kiongozi wa Mashahidi (as) aliona kwamba bahari ya umma wa Waislamu ambao kwawo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitengeneza matufani kwa mara nyingine tena umekuwa muathirika wa udororaji; mawimbi yake yenye hekaheka yamekuwa tulivu na harakati zake zimekuwa kimya na kudorora. Aliona kwamba ilikuwa ni umma uleule ambao humo wanadamu mashujaa na wenye heshima walizaliwa humo kabla, lakini sasa wadudu wabaya (wenye kushambulia nafaka) kama vile Yazid wamejitokeza; tabia chafu na dhulma imekuwa jambo la kawaida, vifusi vya matendo maovu na tabia mbaya vimeeneza harufu mbaya na balaa kila mahali. Hazina ya Waislamu (*Bayt-ul-Maal*) inanyonywa na ruba, kuporomoka kwa maadili kumeanza, viini mbalimbali vya maradhi vimeingia kwenye shughuli mabalimbali za umma, juu ya haya yote wakandamizaji wamepata nafasi (vyeo) kwenye ngome ya umma, yaani mamlaka ya utawala, na Banu Umayya wameufisidi umma wote wa Waislamu kwa uovu wao. Yeye (a.s.) aliichukulia hiyo kuwa ni haja ya kuusafisha umma kutokana na maovu yote, kuwazindua na kutengeneza harakati ndani yao. Ili kuzamisha hali ya u-Yazid kuna haja ya kutengeneza hekaheka, mawimbi na matufani ndani ya bahari iliyotulia ya umma. Kiongozi wa Mashahidi (a.s.) anasema:

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 14



أريد أن أمر بالمعروف وأنهى عن المنكر

"Natoka kwa ajili ya kuutengeneza
(mageuzi ya) umma wa babu yangu, kuamrisha
mema na kukataza maovu."

Mageuzi (matengenezo) hufanywa juu ya kitu ambacho kimeharibika, hivyo tunaweza kuelewa kutokana na maelezo haya kwamba umma umeharibika kwa hiyo Kiongozi wa Mashahidi (as) alitangaza mageuzi ya umma. Kiongozi wa Mashahidi anasema kwamba ni kwa sababu ya dhulma ndani ya umma kwamba mtu kama Yazid amekuwa mtawala. Kama jumuiya ziko hai, maadili yao yako hai na wana harakati ndani yao, basi Yazid asingeweza kujitokeza na kuwa mtawala. Kwa mujibu wa Kiongozi wa Mashahidi (as) dhulma kubwa sana ya umma ni kwamba umekuwa kimya na kudorora; unyofu unakanyangwa mbele ya macho yao na wanageuka kuwa watazamaji, hali ya u-Yazid inapata malezi mbele yao na wamekaa bila kujali, damu ya wenye kukandamizwa inamwagwa kwa dhulma mbele yao na wamekaa kimya.

Kiongozi wa Mashahidi (as) anasema:

"Wakati umma utakapopaza sauti zao kwa ajili ya haki zao binafsi na za wazee wao lakini wakajizuia kupinga wakati haki za dini na mipaka iliyowekwa na Allah Aza wa Jallah inakiukwa, basi uwe na hakika kwamba umma huo umekufa na umma kama huo unahitaji mageuzi."

Kiongozi wa Mashahidi (as) anaeleza kwamba mageuzi ya umma ni mwenendo wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alihuisha jamii iliyokufa kabla ya ujio wa Uislamu, alipulizia roho ndani ya jamii hiyo na kuwabadilisha kuwa umma ulio hai na bora. Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alitengeneza tufani ndani yao, aliwabadilsha wafugaji kuwa kama Abu Dharr, aliwafanya wakazi wa jangwani kuwa

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 15



wakazi wa mbinguni, alitengeneza hisia miongoni mwa wale ambao walikuwa wakipoteza wakati wao katika mashairi, kusengenya na mihadhara isiyo na maana, akawafanya watu wenye kupenda starehe washaghulikaji. *Bethat* kwa jina lake ni uzinduzi, utiaji moyo, kubadilisha na kumfanya mtu asimame, akimbie, kuwa na uchungu na kuingia katika makabiliano. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizinduliwa na Allah Aza wa Jallah na umma ulizinduliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), lakini baadae umma huu uliozinduka ukarudi tena kwenye usingizi na umma huu uliochangamka ukawa kwenye hali ya kudorora.

Qur'ani Tukufu inasema: Mlikuwa mmekufa na Allah akanyanyua Mtume miongoni mwenu ambaye alikuja na kuwarudisheni kwenye uhai.

هُوَ ٱلَّذِى بَعَثَ فِى ٱلْأُمِّيِّـۧنَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ

ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا۟ مِن قَبْلُ لَفِى ضَلَـٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٢﴾

**"Yeye ndiye aliyempeleka Mtume kwa watu wasiojua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhahiri." (Sura al-Jum'a: 2)**

Tulinyanyua Mtume miongoni mweni wakati ambapo mlikuwa katika ujinga ulio wazi na upotofu ulio dhahiri. Mlikuwa mkila na kunywa lakini jamii ilikuwa imekufa. Dalili ya kifo kwa jamii hii iliyokufa ilikuwa kwamba ma-Abu Jahil walizaliwa katika jamii hii. Jamii hii imemzaa Abu Lahab, Abu Sufyani na kizazi chake. Kama umma haukufa basi viini maradhi hivi havizaliwi ndani yao. Ruba na vyura havizaliwi katika jamii iliyo hai. Samaki huzaliwa katika maji hai, na kama maji yana uhai wa hali ya juu basi samaki wakubwa kama papa wanazaliwa katika makazi hayo katika bahari. Kuna watu wakubwa ulimwenguni wanazaliwa katika jamii zilizo hai na viongozi wa kiulimwengu wanazaliwa. Kama Khomein anazaliwa katika umma, basi sababu yake ni kwamba hii ilikuwa ni kwa sababu umma ulikuwa una busara. Kama Nasrullah anazaliwa Lebanon,

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 16



basi busara waliyo nayo umma huo vilevile ina nguvu katika hili.

Kama Kiongozi wa Mashahidi anaulizwa: "Ewe Husein! Unakwenda wapi?" Jibu litakuwa kwamba umma umedorora, mawimbi yake yametulia na ninakwenda kutengeneza harakati ndani yao.

أريد أن أمر بالمعروف وأنهى عن المنكر

"Natoka kwa ajili ya kuutengeneza
(mageuzi ya) umma wa babu yangu,
kuamrisha mema na kukataza maovu."

*Amr Bil Ma'ruf* maana yake kuupa umma harakati; ni kama kusema; Ewe umma! Ingia kwenye harakati, zinduka na ufanye *Amr Bil Ma'ruf*, pingeni maovu, teteeni msimamo na maadili na mlaani maovu. Imamu (as) alisema kwamba ninakwenda kufanya *Amr Bil Ma'ruf* (kuamrisha maadili mema) na *Nahl Anal Munkar* (kukataza maovu). Waislamu wanatekeleza Hija lakini hawafanyi *Amr Bil Ma'ruf*, wanasali na kufunga lakini hawafanyi *Amr Bil Ma'ruf*, wanatoa hutuba lakini hawafanyi *Amr Bil Ma'ruf*, hii maana yake ni kwamba mawimbi yao hayana vuguvugu; yamesimama na yametuama.

Udororaji huu lazima uvunjwe na harakati lazima ianzishwe katika umma. Kitu ambacho hutengeneza harakati ndani ya umma ni mwendo wa Husein (a.s).

Harakati ambayo Kiongozi wa Mashahidi (as) ameianzisha kwa ajili ya kuamsha umma ilikuwa katika awamu, na uongzi wake vilevile ulikuwa katika awamu. Awamu moja ilikamilishwa chini ya uongozi wa Kiongozi wa mashahidi (as) na ya pili ilikamilishwa na Bibi Zainab (as). Kiongozi wa Mashahidi alianzisha uasi, akatoa muhanga maisha yake na maisha ya wapenzi wake, na alishika uongozi mpaka mkesha wa Ashura, lakini baada ya mkesha wa Ashura uongozi huu ulichukuliwa na Imamu Sajjad (as) na Bibi Zainab (as).

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 17



Dada wa Husein hakudai fidia kwa ajili ya wahanga kwa njia inayotokea sasa wakati muumini anapouliwa kishahidi ambapo mara moja madai ya fidia kwa ajili ya watu waliouawa na upinzani hufanywa. Taratibu zinaandaliwa kudai fidia kwa ajili ya kiumbe aliyeuawa na malalamiko hufanywa kudai kwamba mtu fulani mwingine aliyeuawa alifidiwa zaidi na sisi tunapewa kidogo.

Allamah Iqbal hapa vilevile amevuta nadhari yetu: "Msiombe malipo ya fidia (ya damu) kwa ajili ya mashahidi hawa kutoka kwa watu wa Kanisa.Thamani na hadhi ya damu yao ni kubwa mno kuliko sehemu takatifu."

Malipo ya pesa za fidia ya damu ya mashahidi haipaswi kuombwa kutoka kwenye mamlaka kwa sababu damu inayomwagika kutoka kwenye shingo zao ni mshumaa kwa ajili ya umma, ni mwanga kwa ajili ya umma kwa hiyo msidai fidia kwa ajili ya mashahidi. Bibi Zainab (as) kamwe hakudai fidia kwa ajili ya mashahidi badala yake aliigeuza damu ya mashahidi kwenye harakati na kuleta vuguvugu kwenye umma uliokufa na hivyo kuiamsha jamii iliyokufa. Kamanda huyu wa harakati ya Karbala alikuwa hai takriban kwa mwaka mmoja na nusu baada ya Karbala, lakini kipindi hiki kilikuwa kinatosha kwa ajili ya Bibi huyu mtakatifu kukamilisha kazi hii. Zainab (as) ni jina la haiba ambalo huleta harakati katika jamii iliyokufa.

Hakusema kuuambia umma kwamba kaka yangu ameuawa shahidi na sasa jukumu langu ni kukaa tu na kumlilia, lakini badala yake alisema:

> "Kama nikilia machozi yangu vilevile yatazaa harakati, kuhisi kwangu vilevile kutazaa harakati na popote pale ambapo machozi yangu na kuhisi kwangu kusipoleta harakati nitasimama na kutoa hutuba. Je, unajua jinsi ambavyo binti ya Ali (as) alivyozalisha harakati katika jamii iliyodorora kama ya mji wa Kufa?"

Kufa ilikuwa jumuiya iliyokufa ambayo haikutoka kumsaidia Imamu Husein (as) kwa ajili ya hofu ya Ubaidullah. Wakati kamanda wa msafara (yaani Bibi Zainab) alipowasili Kufa aliona hii ni jumuiya iliyokufa na jamii hii iliyokufa wametoka nje kama watazamaji ili kutuangalia na kuangushia macho yao kwetu, hivyo alipaza sauti yake:

"Enyi watu wa Kufa sikilizeni, bint wa Ali na Fatima anataka kusema kitu kuwaambia ninyi, anataka kusema kwamba ninyi wote ni wafu, dhamiri yenu imekufa na heshima yenu imekufa. Bibi huyu ameahidi kwamba nitapulizia uhai katika jamii hii iliyokufa." Na chini ya mwaka mmoja watu walewale wa Kufa, wasaliti, walewale waoga na mamufti walewale waliwageukia watu na kuunda jeshi la watu elfu nne kwa jina la jeshi la kutubia (*Lashkar-e-Tawwabin*). Waliahidi juu ya damu yao kwamba watapigana katika njia ya Husein Ibn Ali (as) mpaka mwisho wa tone la damu yao, na watu hawa wote elfu nne waliuawa. Kamanda huyu wa harakati alitoa katika mji uliokufa wa Kufa jeshi la watu elfu nne la wanadamu wanaoishi. Bibi Zainab (as) alizalisha harakati ambako jumuiya iliyokufa ilihuika na kuja kuingia kwenye harakati.

Mkesha wa Ashura wakati Husein (as) aliendelea kuita: "Je, yuko yoyote wa kunisaidia mimi?" lakini hakuna aliyetoka kwenye nyumba zao kwa sababu kulikuwa na ukimya na kutuama sehemu ile. Bibi yule akaahidi pale yeye mwenyewe kwamba sasa nitakamilisha kazi hii ambayo sitamruhusu mtu yeyote kukaa nyumbani kwake, nitamaliza kudorora kwao, nitavunja ukimya wao, na nitazalisha vurugu ndani yao. Azadari ni jina la wimbi hili ambalo lilizalishwa ndani ya jamii iliyodorora na kimya na bint Ali (as). Ni kwa matokeo ya wimbi hili na maji kupwa na kujaa kwamba umma wote unaomboleza na kufanya Azadari leo.

Usifikirie kwamba Azadari ni njia tu yakupatia thawabu. Azadari ni uhai na maisha ambayo bila hivyo ni kifo. Mtu ambaye haombolezi na hafanyi Azadari ni mfu, na kumhuisha anahitaji kutoka nje. Machozi kwa ajili ya kupata thawabu yanaweza kutolewa majumbani vilevile, lakini machozi

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 19



kwa ajili ya kupata thawabu hayazai harakati. Hivyo unahitaji kutoa machozi ya kupinga, na yako wapi machozi ya kupinga? Lazima utoe machozi nje ya uwanja wa mapambano, kusoma tenzi za huzuni, kusoma mashairi ya kuomboleza na katika mashairi haya pigeni vifua vyenu ili kuujulisha ulimwengu kwamba tutavunja ukimya na udororaji huu licha ya ukatili mkubwa. Hii ni kwa sababu Bibi mkubwa huyu Zainab (as) ameuamsha ubinadamu. Leo hakuna mtu awezaye kuisimamisha harakati hii, wala si wafuasi wa Yazid wawezao kuisimamisha harakati, wala Yazid aliyepo sasa hawezi kuisimamisha harakati hii na wala sio ma-Yazid watakaokuja baadae katika zama nyingine, pia hawataweza kuisimamisha harakati hii. Je, kuna harakati nyingine ambayo inafanyika katika kila nyumba? Je, kuna harakati yoyote kwa watoto? Je, kuna harakati yoyote ambayo ipo ndani ya wazee pia? Na kwa wanawake pia? Ndani ya vijiji, ndani ya miji na kuwepo kila mahali? Je, kuna harakati nyingine ambayo kwamba wanachuoni na watu wa kawaida wote kwa pamoja wanashiriki bila kukaribishwa? Hii ni harakati iliyoanzishwa na Binti wa Ali (as) na hubeba ukombozi ndani yake.

Sio kwamba tunapoomboleza tutajiepusha na moto wa Jahannam, bali badala yake kama tukiomboleza basi machozi haya yataleta uhai kwenye nyoyo zetu na ujumbe huu wa uhai utapokelewa na ulimwengu. Jamii itahuika na ukombozi utakuwa kwa ma-Yazid wa zama zetu, na vilevile ukombozi katika Akhera. Kwanza Azadari hutoa kinga katika ulimwengu huu na kisha katika Akhera. Azadari ni jina la uhai na vijana hawa lazima wawe na ujumbe wa uhai na vijana hawa lazima wawe na harakati ndani yao.

Ni wapi ambapo sisi wote tunahitaji harakati? Harakati inahitajiwa na moyo, na akili na fikra. Ni muhimu kuwa na harakati za fikra na harakati za hisia. Kama hisia hazizai harakati mpaka wakati huo, hakuna anayetoka nje. Bibi mkubwa huyu alizipa hisia hizo harakati, aligawa harakati kwenye fikra na akili; aliifikisha harakati katika nyoyo na nafsi. Ni matokeo ya harakati ambayo yeyote yule asikiaye jina la Husein Ibn Ali

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 20



(as) hakubakia ndani ya nyumba yake.

Azadari ni ya Husein na kamwe usiweke alama ya jina la mtu yeyote kama vile kusema Azadari ni ya kikundi mahususi (*Anjuman*) au chama mahususi, au mzungumzaji mahususi au khatibu mahususi. Ni jinai kufanya hivi na ni jinai kuipa Azadari majina. Usiende kwenye Azadari kwa sababu tu ya khatibu fulani au kwa ajili ya kuliridhisha kundi. Usije kwenye Azadari kwa sababu tu ya makundi (*Anjuman*). Kama ukihudhuria Azadari, basi fanya hivyo kwa ajili ya Bibi Zainab (as). Azadari sio miliki ya mtu yeyote binafsi. Hii ni harakati ile ambayo ilizalishwa na Bibi Zainab (as) na uzuri ulioje kwamba aliizalisha katika mtindo uleule kama wa Husein (as). Na mateso makubwa yaliyoje aliyoyapata kwa kuzalisha harakati hii. Leo hakuna mtu awezaye kuisimamisha na ujumbe huu kamwe hauwezi kusimama kwa njia yoyote ile. Watu wangapi wamekufa (Iraq, Pakistan na kwingineko), lakini maandamano hayajasimama wala mikusanyiko ya maombolezi haikusimama.

Silaha na mabomu hayawezi kusimamisha hili kwa sababu adui hajui ni wapi harakati hii imeanzia. Kutoka wapi harakati imeletwa. Harakati hii haikuanzia kutoka kwenye chumba cha kuchorea cha nyumba fulani. Imeanzishwa kutokana na miili iliyoanguka na yenye sanda ya Karbala, na hii imeanzishwa kwa damu na kiu. Haiwezi kusimamishwa na mtu yeyote, jinsi unavyozidi kuuwa waombolezaji, harakati hii huzidi kukua na kupamba moto zaidi. Umekosea katika kulielewa hili, kwa sababu kama wasingewauwa watu pale Karbala basi harakati hii ya Bibi Zainab isingeanzishwa. Leo kiasi chochote cha watu mtakaowauwa harakati hii itazidi kupamba moto, kwa sababu harakati hii imeanzishwa na miili iliyokufa (ya mashahidi wa Karbala), basi vipi itasimamishwa kwa miili iliyokufa. Hii ilianzishwa kwa shingo zilizokatwa, na hii itaendelea pamoja na miili iliyovishwa sanda. Miili hii iliyokufa na kuvishwa sanda ni bendera ya harakati hii na kwa hiyo usiwafikirie kuwa ni wafu, kwa sababu mashahidi hawa ni makamanda wa harakati hii.

> Nguvu za kijeshi haziwezi kuuvunja ukweli, hata nguvu hiyo ikiwa ya Yazid yeyote. Maiti husimama tena kama bendera, hata kama maiti hiyo ikiwa ya shahidi yeyote.

Ujumbe huu ni wa damu na ujumbe wa Zainab (as). Kuna mengi ya kusema juu ya nukta hii, na mengi lazima yasemwe. Nukta hii haikumalizika kwa sababu haikuanzishwa kwa nia ya kufikia mwisho. Unahitaji kubadilisha mwelekeo wako wa kuitazama Azadari. Usifanye Azadari kwa njia ambayo italeta udororaji na ukimya. Azadari hii imekusudiwa kwa ajili ya harakati na kuleta vuguvugu. Kwa harakati hii iliyoendelea ndani ya nafsi yako na harakati ndani ya jamii, kama ulimwengu mara moja unaingia kwenye kazi basi hakuna Yazid awezaye kuisimamisha; si Yazid wa zama hiyo wala wa zama hizi atakuwa na uwezo wa kuisimamisha kwa sababu Bibi mkubwa Zainab (as) ameanzisha harakati iliyofanikiwa.

Wakati mwingine harakati huanzishwa hususan dhidi ya watu binafsi au serikali mahususi, lakini harakati haianzishwi dhidi ya serikali tofaouti za zama tofauti; lakini harakati hii inaendelea kuwepo tangu miaka elfu moja mia nne iliyopita. Kwa nini kuna baadhi ya watu wanaotaka kuisimamisha harakati hii? Kwa nini kuna maadui wa Azadari? Hawa sio maadui wa kitu chochote kingine bali kwa Azadari tu kwa sababu wanafahamu kwamba bahari hii ina nguvu ndani yake. Inawezekana kwamba leo wale ambao wana nguvu hii hawaihisi. Allamah Iqbal ameandika katika moja ya mashairi yake kwamba shetani amewaambia wanafunzi wake kwamba nguvu ya umma huu ni Qur'ani. Wanafunzi wa shetani wakajibu kwamba umma huu hausomi Qur'ani. Shetani akasema kwamba siku ambayo umma huu utageuka na kuilekea Qur'ani, basi hakuna shetani wala wanafunzi wake watakaobakia katika juu ya ardhi. Ingawa naelewa kwamba umma huu hauna ujuzi wa Qur'ani lakini Qur'ani hii imo ndani ya umma kama volkano. Siku itakapolipuka itaangamiza kila kitu. Hii ndio njia ambayo Bibi mkubwa Zainab hakuruhusu tukio la Karbala kugeuka kuwa

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 22



tukio la kihistoria, hakuruhusu siku ya Ashura kugeuka kuwa siku ya neema, aliibadilisha Karbala kuwa volkano, ni aina gani ya volkano? Volkano ile ambayo lava yake itaendelea kuchemka, kwa hiyo lazima uisome misiba ya Ashura ili kwamba lava hii iendelee kuchemka.

إنّ لقتل الحسين حرارة في قلوب المؤمنين لا تبرد أبداً

“Hakika mauaji ya Husein yalileta joto katika nyoyo za waumini ambalo kamwe halitashuka.”

Kumbukumbu ya kuuawa kishahidi kwa Husein (as) ina volkano ambayo siku zote itakuwa inawaka na itaendelea kupasha moto nyoyo za waumini. Wakati lava hii ndani ya nyoyo za waumini itakapovimba na kupasuka, itamuangamiza Yazid wa zama za sasa. Kama lava hii ikilipuka basi usiipoze, kuna baadhi ya watu ambao huimba mashairi ya kuliwaza kwa jina la Azadari wakati ambapo Azadari ni jina la harakati. Ni ujumbe, sio ujumbe wa udororaji na kusimama sehemu fulani. Siku utakapoisimamisha hii utakufa. Siku utaposimama kimya utakufa. Hii ndiyo sababu Imamu Khomein (ra) anasema: “Fanyeni Azadari katika mazingira yote kwa sababu kama Azadari ya kweli inasimamishwa, Uislamu utaishi; hivyo basi wekeni milango ya uadilifu wazi.

# SURA YA PILI

## Ujumbe wa Ashura

Ili kuuelewa ujumbe wa Ashura tunahitaji kuelewa tukio na ujumbe wa Ashura na sababu mbalimbali nyuma yake. Kwanza tunahitaji kuelewa ni kwa nini kadhia hii ya Ashura na Karbala ilitukia? Wote tunafahamu ni lini na wapi kadhia hii ilipotukia. Historia inatufahamisha kuhusu zama, mahali, ardhi na watu waliohusika na kadhia hii, lakini kwa kuelewa tu vitu hivi vidogo hatuwezi kuelewa ukweli nyuma ya kadhia yoyote. Ukweli hauwezi kupatikana mpaka tuingie ndani ya mizizi ya kadhia yoyote na kutafuta watu na sababu nyuma ya kadhia hiyo. Kadhia yoyote haiwezi kufahamika mpaka watu wazifikie sababu halisi na sababu nyuma ya kadhia hiyo, na bila hivyo kadhia hiyo inakuwa ya kitendawili. Hali ambayo kadhia ya Ashura bado ni ya kuduwaza kwa akili mahususi hata baada ya mamia ya miaka ya kadhia hii, na hata kwa wale wanaochukulia kwamba kadhia ya Ashura ni suala lililosuluhishwa. Kwa mujibu wa wanachuoni fulani, kadhia ya Ashura ilianza asubuhi ya siku ya kumi ya mwezi wa Muharram na awamu ya kwanza iliishia katika usiku wa Ashura; kwa maana kwamba mapambano yaliisha.

Katika historia juu ya mpito wa muda wa mapambano ya Karbala ni muda mfupi sana wa mapambano kinyume na mapambano ambayo yanatajwa katika historia kama vile mapambano huendelea kwa muda wa miaka arobaini, hamsini na zaidi ya nusu karne. Lakini marefu, mapana na maelekezo ya mapambano hayategemei juu ya idadi ya miaka iliyopiganwa bali badala yake msingi wa maelekezo yake, marefu na mapana ni vyanzo na sababu zinazopiganiwa.

Ipo kadhia katika historia ambako mtu mmoja mwenye ari kutoka kabila la Kiarabu alikuwa akifukuza panzi kwa kuwinda na wakati wa kumfukuza

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 24



kwake kiumbe huyu akaingia ndani ya hema la kabila nyingine. Kutokana na hili mtu yule akasema panzi huyu amechukuwa hifadhi kutoka kwao na yeyote anayechukua hifadhi kwetu sisi hatumrudishi kwa adui yake. Yule muwindaji akasema kwamba windo hili ni langu na nina haki juu yake. Mabishano haya yakageuka kuwa mapigano na mmoja wao akamuuwa mwingine kwa mkuki wake, na juu ya hilo mapigano yakaanza kati ya makabila haya mawili ambayo yaliendelea kwa muda wa miaka arobaini. Kama tukikadiria juu ya mpito wa muda basi vita hivi vilichukuwa muda mrefu sana wa miaka arobaini, lakini kama tukitafakari juu ya vita hivi hakuna zaidi ya dakika tano za mazungumzo kuhusu suala hili, kwa sababu hakuna chochote katika vita hivi mbali na suala la kwamba makabila mawili yalipigana kwa sababu ya panzi na vita hivi vikachukuwa miaka arobaini. Kwa upande mwingine kuna vita vingine katika historia kwa jina la Karbala ambavyo vilianza asubuhi na kuisha jioni; ambapo humaniisha kwamba katika mpito wa muda huu ni muda mfupi sana wa vita na huenda juu ya msingi wa muda hakuna vita vingine vyovyote kama hivi ambavyo havikukamilisha hata siku moja.

Sasa linganisha vita hivi viwili; moja kwa muda wa miaka arobaini na vingine kwa muda wa saa chache. Vita vya miaka arubaini havina suala la kufaa kuchukua dakika tano ambapo kwamba vita hivi vya saa chache vina maana sana, mkazo sana, nguvu sana na kina. Vina sababu nyingi sana nyuma yake kwamba hata miaka elfu moja na mia nne haitoshi kutafakari juu yake. Tangu miaka elfu moja na mia nne mwanadamu anajaribu kufahamu ukweli wa kadhia yake lakini bado hayuko katika nafasi ya kusema kwamba amefikia kina chake bali badala yake mpaka sasa mwanadamu anachukuliwa kama mjinga kuhusu mapambano ya Karbala na hajui kitu chochote.

Karbala ni bahari na bahari inamaanisha mkusanyiko ule ambao hauna kingo; hii humaanisha ina kingo lakini kwa kusimama kwenye kingo moja kingo ya upande mwingine haiwezi kuonekana. Bahari ni ule mkusanyiko wa maji ambayo kina chake hakiwezi kufikiwa kirahisi. Kanuni nyingine ya bahari ni kwamba hakuna kinachopatikana kwenye fukwe zake ingawa

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 25



povu la bahari hufikia fukwe zake na wakati mwingine mawimbi ya bahari hutupa baadhi ya viumbe ndani yake kwenye fukwe.

Kama mtu yuko katika kusaka vito, alimasi na lulu basi asizitafute kwenye fukwe na wala hawezi kuzipata kwa kuogelea juu ya bahari kwa sababu hizi zipo kwenye vina vya ndani vya bahari katika sakafu yake. Lakini kwenda chini ya bahari sio kazi ya mtu wa kawaida. Bahari haitoi fursa kwa mtu wa kawaida kufikia vina vyake kwa sababu haifungui sanduku lake na hazina yake kwa ajili ya mtu wa kawaida. Wazamiaji wanahitajika kwenda chini ya bahari; moyo wa kishujaa, ujasiri na watu wa namna hiyo wanahitajika ambao wakati wa kurudi kutoka baharini lazima wawe na lulu mikononi mwao. Lulu hizi za thamani ambazo wamezipata ndani ya bahari zitakuwa ni mtaji kwa ajili yao na vilevile kwa ajili ya umma na jamii yao.

Hii ndio sababu ambayo wale wanaohangaika kwenye fukwe za Karbala tangu zaidi ya miaka elfu moja na kumi na nne wanakaa tu katika fukwe zake. Tofauti pekee ambayo imejitokeza kwao ni ile ambayo kwamba waliacha kundi, vitindamlo na kufikia fukwe hii ya bahari lakini ni mpaka kwenye fukwe tu. Hawakuingia ndani ya bahari kwa sababu kama wangerukia ndani ya bahari hii hali ya umma wa Kiislamu isingelikuwa hivi ilivyo leo. Aina ya alimasi na lulu zilizopo ndani ya Karbala na sifa bainifu zilizopo Karbala zimekuja tu katika mikono ya wazamiaji. Zimekuja katika mikono ya mtu yule ambaye anaweza kufikia kina cha bahari. Mtu anayejua kufikia sakafu yake ya chini na ambaye hana woga na giza na hatari, Karbala huifungua kifua chake kwa ajili yake lakini sio kwa ajili ya watu wa fukweni. Ingawa Karbala haimuachi mtu yeyote na kumtelekeza, hivyo wale ambao wanakaa katika fukwe zake bado wanaweza wakashibisha matumbo yao na kujaza mifuko yao kwa sababu vitu kama hivyo vilevile hupatikana katika fukwe za Karbala. Lakini hatuwezi kusema kwamba mikono yao imefikia vito hivyo vya thamani. Watu wamekwenda kwenye fukwe ya Karbala lakini bado wamerudi wakavu.

Nukta hii lazima iwekwe akilini kwamba Karbala sio bahari ya maji bali ni bahari ya damu. Kwenda chini ya bahari ya damu hatuhitaji wazamiaji wenye kutumia vyombo vya kuvutia hewa ambao wanaweza kwenda kwenye vina virefu vya maji, lakini kwa bahari ya Karbala tunahitaji wale ambao wanaweza kuogelea kwenye damu, kuloweshwa na damu yao wenyewe, anayeza kufanya uzamiaji wa kutumia vyombo vya kuvutia hewa na kuweza kupata lulu iliyomo ndani ya damu. Kama lulu zilizomo ndani ya maji ni zenye thamani sana ambazo ulimwengu wote unazitamani, basi lulu zilizomo ndani ya damu ni zenye thamani kubwa zaidi. Lulu zinazokuja kutoka kwenye maji huwa ni za fahari ya mwili wa mwanadamu, lakini lulu zinazokuja kutoka kwenye damu huwa za hadhi kubwa kwa ajili ya nafsi ya mwanadamu. Inawezekana kwamba mtu kwa kuvaa lulu zilizokuja kutoka kwenye maji shingoni mwake anaweza akatoa fikra kwamba anavyo vito vya thamani. Lakini mtu anayekwenda chini ya bahari ya Karbala hupata fahamu, akili na utambuzi ambao sio kila mtu anayo fursa ya kuufikia. Kama mtu atatoka nje akiwa amevaa lulu hizi katika uhui wake basi uhai wake wote unakuwa jua linalong'ara kwa ajili ya ulimwengu mzima na kwa umma mzima. Miali yake yenye kung'ara hung'arisha ulimwengu wote. Karbala ni chanzo kitukufu cha akili, ujuzi na utambuzi. Bahari hii ina vito vya kudumu ndani yake.

Hii ni kanuni ya kimungu ambayo mwanadamu huelewa vitu mahususi wakati tu mawazo fulani na mifano yake ipo ndani ya mwanadamu. Kwa mfano nini kinamaanishwa kwa (kusema) uwaziri au urais? Hata kama mtu hawezi kuwa waziri au rais bado anaelewa maana ya uwaziri na urais. Lakini kuna baadhi ya vitu ambavyo mpaka mtu avionje, vinginevyo hawezi kuelewa maana yake; kama kwa mfano mtu mpaka aonje ujasiri hawezi kuelewa ujasiri. Vilevile kama kwa muda wa mika mia moja ujasiri unajadiliwa mbele ya mtu mwoga bado hataelewa maana ya ujasiri. Kama kuna mtu asiye na aibu ambaye hajaonja kujiheshimu kamwe hawezi kupendezewa na haiba ya kujiheshimu. Ingawa huenda amekuwa akisikiliza visa vya heshima na kujiheshimu; atatingisha kichwa chake katika mijadala kuhusu ujasiri na ushujaa lakini bado hawezi kuelewa maana ya

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 27



kujiheshimu na heshima. Jumuiya nyingi zimesimamishwa kwa kusikiliza mara kwa mara visa za ujasiri na ushujaa, lakini leo kila kitu kinaonekana kwao isipokuwa ujasiri na kujiheshimu. Kama kwa kusikiliza tu mtu anaweza kuwa jasiri na kujiheshimu, basi mtu ambaye amesikiliza visa na mazungumzo kuhusu ujasiri na kujiheshimu atakuwa mwenye ari zaidi na mtu wa kuheshimika.

Amiru'l-Muminin (as) alitoa hutuba nyingi mjini Kufa, mtu huyu jasiri mwenye mvuto wa ujasiri, alitoa hutuba za kijasiri, zilizowasilisha uthibitisho wa kujiheshimu kwake mjini Kufa, aliwafundisha watu wa Kufa maana ya kujiheshimu, lakini wakati wa tukio la Karbala lilipotukia haukuonekana ushujaa wala kujiheshimu katika watu wa Kufa.

Hutuba nyingi katika *Nahjul Balaghah* zimetolewa na Ali (as) akiwa Kufa. Yeye (as) alizitoa wakati wa swala za Ijumaa, au wakati wa kuelekea vitani, au wakati wa vita, au mwisho wa vita, baadhi katika wakati wa Iddi na baadhi huhusika na matukio na kadhia ngumu na nzito. Katika baadhi ya hutuba aliwafundisha watu *tawhid* (upweke wa Mungu), katika baadhi alifundisha dini, katika baadhi alifundisha Qur'ani, katika baadhi alifundisha sheria na kanuni za dini, katika baadhi alifundisha hadhi ya Ahlul Bayt (as), katika baadhi aliwafanya watu waelewe cheo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), katika baadhi alijaribu kuendeleza ufahamu wa watu, katika baadhi alifundisha ujasiri na katika baadhi aliamsha kujiheshimu kwa watu. Hutuba zote hizi zilitolewa katika mji wa Kufa, lakini kama kwa kusikiliza tu hutuba, mihadhara na mijadala mtu anaweza kuwa jasiri, basi watu wa Kufa wangekuwa wajasiri kupita wote kwa sababu Khatib wa Kufa alikuwa sio mhubiri wa kawaida; kwa kweli ni aliyekomaa zaidi ya wote, fasaha zaidi kuliko wote na jasiri zaidi kuliko wote. Mwanachuoni mmoja wa Sunni alitaja simulizi moja katika kitabu chake kwamba mipaka na ukubwa wa ukomavu wa Amiru'l-Muminin (as), ujuzi na ujasiri ulikuwa kwa kiasi kwamba wakati watu walikuwa wakiona ufasaha wake mara moja walikuwa wakisema:

لا إله إلاّ الله ما أبلغ هذا البشر، لا إله إلاّ الله ما أفصح هذا البشر،
لا إله إلاّ الله ما أشجع هذا البشر.

"Hakuna mungu isipokuwa Allah, mtu huyu amekomaa! Hakuna mungu isipokuwa Allah, mtu huyu ni fasaha mno! Hakuna mungu isipokuwa Allah, mtu huyu ni jasiri mno!"

Anachokusudia kusimulia hapa ni kwamba maneno ya kushangaza huwatoka watu wakati wanapomuona Ali (as). Kila mmoja ana uhakika na kuamini kwamba hakuna Khatibu mkubwa kama Ali (as) ambaye amezaliwa na ambaye atazaliwa. Hakuna shujaa aliye mkubwa kama Ali (as) aliyezaliwa na mtu huyu fasaha zaidi na shujaa alitoa hutuba katika mji wa Kufa, akawafanya watu wajisikie kujiheshimu kwao na ari, lakini wakati wa tukio la Karbala kila kitu kilikuwa kinaonekena kwa watu hawa wa Kufa isipokuwa ujasiri na kujiheshimu. Kwa nini? Huwezi ukaelewa dini kwa kuwa tu msikilizaji wa dini, kwa kusikiliza masimulizi ya kijasiri huwezi kuwa jasiri; kwa kusikiliza tu visa vya kujiheshimu huwezi kufikia hali ya kujiheshimu. Mtu hawezi kuwa wa kuheshimiwa mpaka mambo ya kujiheshimu na ujasiri yamuingie ndani yake. Mtu hawezi kupata ujasiri mpaka apate mambo yale ya ujasiri na ladha ya ujasiri; hivyo mtu muoga kamwe hawezi kuelewa ujasiri. Ni kuanzia muda gani hutuba zinatolewa kwenye jumuiya, kadhia ya Karbala imekuwa ikisimuliwa katika lugha mbalimbali, mtindo na mbinu mbalimbali, lakini wakati wa mtihani unapokuja hapo tunatambua iwapo baada ya kusikiliza hutuba hizi kama tumeelewa kitu au la.

Allah Aza wa Jallah vilevile huchukua mtihani sawa na utendaji tulionao katika mfumo wetu wa elimu. Kwanza tunakaa, kusoma na kusikiliza katika chumba cha madrasa; mwalimu anafundisha na sisi tunasikiliza ambapo baada ya hapo mitihani inatolewa. Wakati mwingine mwalimu yule ambaye amefundisha anaendesha mitihani na wakati mwingine kuna mamlaka (bodi) za mitihani. Mtahini katika mamlaka za mitihani sio mtu

ambaye alikuwa anafundisha; mtu anayeendesha mitihani wakati mwingine ni mkali sana na wakati mwingine anaweza kuwa mtu laini sana. Wakati mwingine anawaruhusu wanafunzi kunakili na wakati mwingine hawaruhusu, hivyo kuna watahini wakali na halikadhalika na watahini laini. Kiasi mtahini anavyozidi kuwa mkali hivyo hivyo na mtihani utakuwa mgumu, lakini wale wanaofaulu kwa kutoa mitihani mbele ya watahini wakali wanakuwa na uwezo zaidi na uhodari. Wala wanaofaulu kwa kunakili kutoka kwa wengine mbele za watahini laini hawakubaliwi na yeyote kwa sababu kufaulu kwa kunakili katika mitihani ni sawa sawa na kushindwa.

Watu wa Kufa walisikiliza hutuba nyingi juu ya ujasiri, kujiheshimu, dini, sheria, Qur’ani na Ahlul Bayt. Katika *Nahjul Balaghah* sehemu tu ya kumi na mbili ya hutuba za Amiru’l-Muminin (as) zipo na kuna sehemu kumi na moja zaidi zinazolingana; au tunaweza kusema kwamba kwa sasa tuna jalada moja la hutuba za Amiru’l-Muminin (as) na majilida kumi na moja zaidi kama hayo yapo. Hutuba hizi zilitolewa na Amiru’l-Muminin (as) kwa ajili ya watu wa Kufa na kisha mtihani kwa ajili ya watu wa Kufa uliendeshwa na mamlaka zile za mitihani. Kwa ajili ya mamlaka hii ya mtihani, mtahini mkali na mgumu alipelekwa kwa watu wa Kufa. Walitahaniwa kupitia kwa Ubaidullah ibn Ziad.

Kila mtu anaelewa kadhia ya jinsi gani Ubaidullah alivyoingia Kufa kwamba aliingia Kufa wakati wa usiku. Alikuwa ameweka ukaya usoni mwake na kwa vile watu wa Kufa walikuwa wanamsubiri Imamu Husein (as) kwani alikuwa awasili wakati wowote. Kwa hiyo, wakati mtu mwenye ukaya akiingia Kufa usiku ule walimfikiria kimakosa kwamba ni Husein Ibn Ali (as). Mara moja wote walikusanyika na wakaanza kutayarisha kwa ajili ya mapokezi haya, walianza kupandisha sauti za kaulimbiu za Maisha Marefu na Kifo Daima (*zindabad*, *Murdabad*). Ubaidullah akamtembeza farasi wake pale kwa muda kidogo na watu wa Kufa wakafikiria kwamba kwa hakika si mwingine bali ni Imamu Husein (as) na mori ukawapanda zaidi; na wakati Ubaidullah alipompeleka farasi wake kwa mbio zaidi

wakafikiria kwamba Imamu Husein (as) amezipenda kaulimbiu zao na kwa hiyo wakapaza sauti zaidi za kaulimbiu zao. Wale waliokuwa ndani ya nyumba zao wakachukulia kwamba Imamu Husein (as) amewasli, hivyo wakatoka nje kwenye uwanja wa Kufa. Kila mtu akajikusanya kumzunguka Ubaidullah na wakaanza kusema: "Ewe Imamu. Ewe Imamu, Ewe Kiongozi, Ewe Kiongozi, Ewe Husein ibn Ali na Ewe Husein ibn Ali." Jina ambalo walikuwa wakiliita sana ni Abu Abdillah ambalo lilikuwa ni kuniyah ya Imamu Husein (as). Walianza kujieleza kwa Imamu wao wa kimakosa: "Ewe Aba Abdillah tulitamani mno kukutana na wewe, kwa muda mrefu tumekuwa tunakusubiri, tulikuandikia barua (nyingi) na tulikuwa tunakuita uje upesi, uje upesi, uje upesi (*Al Ajal, Al Ajal*)."

Watu wa Kufa waliandika barua 9,000 na katika barua zote hizi sentesi iliyoandikwa zaidi ilikuwa ni: "*Al Ajal Al Ajal,*" Ewe Imamu njoo upesi, muda unapita, fursa hii itapotea, tumejiandaa, nafaka zimekomaa, uwanja uko tayari na unakusibiri wewe kuwasili. Walimuomba aondoe ukaya wake ili wauone uso wake. Wote sisi tunataka kuona uso wako mng'avu, baadhi walimuomba awape mkono wake ili wapate kuubusu. Baadhi walimuomba ashuke kwenye farasi wake ili wapate kubusu miguu yake, lakini aliendelea kumtembeza farasi wake huku akiwahesabu na kuwatambua.

Madhumuni yake ya kuweka ukaya ilikuwa ni kutumia muda ili kuwahadaa kwa muda, kuwazunguka na kuwafanya wazunguke kwa muda kidogo ili iweze kuonekana nani miongoni mwao ni wasaliti na nani ni watiifu, nani wenye dini na kwa ajili ya Allah, nani wako kwa ajili ya nafsi zao wenyewe tu. Ubaidullah alipitisha muda bila kuondoa ukaya usoni mwake. Wale wenye madai ya uwongo ya imani walimpa makaribisho mazuri na kusema kwamba ni Imamu wetu na Imamu wetu amekuja. Waliendelea kumuita na kumuomba, chukua hatua tuko pamoja na wewe. Ubaidullah aliendelea kuwatupia macho wote kwa usahihi na wakati jumuiya yote ilipokusanyika aliondoa ukaya usoni mwake. Mikono ambayo ilikuwa imenyanyuliwa kwa ajili ya kaulimbiu na taya zilizokuwa wazi kwa ajili ya kaulimbiu zikabaki wazi na mikono ikabakia pale ilipokuwa. Hawakuwa

na nguvu ile ya kushusha mikono yao chini ili kuifunga midomo yao. Kila mmoja alikuwa amepingwa bumbuazi na kimya, miguu yao ilikuwa inatetemeka, hofu ikiwa imewajaa, rangi zao zikapauka na nafsi zao zikawatoka.

Alikuwa mmoja na walikuwa kundi kubwa; kama wote kwa pamoja wangemchapa tu makofi mara moja angalifariki pale pale. Wale ambao wamesikiliza hutuba nyingi za ujasiri, wameswali nyuma ya Imamu jasiri mno, wameshiriki katika kuwa na Imamu shujaa mno na wenyewe walikuwa Majenerali na makamandoo wakubwa wa jeshi wakiishi katika kambi ya jeshi (Kufa ulikuwa aina ya mji wa kambi ya jeshi); na walikuwa wadai wakubwa wa imani. Lakini Ubaidullah alipoondoa ukaya usoni mwake walianza kutetemeka na sauti zao zikawa hazitoki. Mtu mmoja akasema kwamba kwa nini mko kimya, kwa nini sauti zenu hazitoki, kwa nini sasa hamsemi Uishi Maisha Marefu Husein, kwa nini makoo yenu yamesakamwa; yeye ni mtu tu. Hivyo mtihani wa imani uliendeshwa kwa sababu walikuwa wadai wakubwa wa imani, wenye kujisifia na kujiona wenyewe kama waliopendelewa zaidi katika ulimwengu; ambao wameandika katika barua zao kwamba kwa sasa katika ulimwengu mzima hakuna waumini walio bora kama watu wa Kufa.

Kwa hiyo, Allah Aza wa Jallah akawapelekea mtahini miongoni mwao na sio kwamba Allah Aza wa Jallah amempeleka Ubaidullah kwenda Kufa, bali badala yake Allah Aza wa Jallah alimpa fursa hii. Suala lote lilivunjika kwa kuingia Ubaidullah mmoja, viganja vilifunguka na imani iligeuka kuwa tetemo; ujasiri ulipotea na kujiheshimu kulitoweka. Kama mkusanyiko huo mkubwa wa watu ungemtupia kokoto moja kila mtu, angezikwa chini ya kokoto hizo, pia ilikuwa kuna giza kama wangemchapa mara moja tu, angefia pale pale lakini jumuiya ambayo ilisikia tu kuhusu imani na haina ujasiri wowote, kujiheshimu na imani; kwao wao Ubaidullah mmoja anatosha. Jumuiya ingeweza kuwa katika maelfu na mamilioni ya watu lakini kama Ubaidullah mmoja tu akitoa kauli katika vyombo vya habari nafsi zao huondoka katika miili yao. Ubaidullah aliweka ukaya kwa

muda kidogo kwenye uso wake, kwa kufanana kwa muda wa mwaka mmoja au miaka miwili mwanzoni na akaizunguka jumuiya nzima ili kuona kwamba ni nani anakuja mbele na nani anabakia nyuma. Mpaka muda ambapo bado ukaya uko kwenye uso wa Ubaidullah mtu wa Kufa anamuona kama mkombozi na kumuomba alete mkono wake ili aubusu, wakati ambapo chini ya ukaya ni Ubaidullah. Watu wa Kufa wanamjua vizuri Ubaidullah ibn Ziad na pia wanamjua baba yake Ziad ibn Abih. Wanajua kwamba hawa ni watu makatili sana ambao hawana huruma juu ya mtu yeyote na Allah Aza wa Jallah hakuweka upole wowote ndani yake na hiyo ndio sababu alipelekwa kama mtahini.

Karbala ni jina la Akili, ni jina la Utambuzi na ni jina la uhalisia. Katika Kufa walikuwepo watu elfu sabini na mbili wakati ambapo Karbala kulikuwa na miili sabini na mbili tu; lakini nini ilikuwa tofauti kati ya hawa mashahidi sabini na mbili na wale elfu sabini na mbili? Tofauti ilikuwa kwamba wale elfu sabini na mbili wamesikia tu jina la ujasiri wakati ambapo ujasiri kwa kweli ulikuwepo ndani ya hawa sabini na mbili. Watu wa Kufa walisikia tu jina la kujiheshimu wakati ambapo wasaidizi wa Husein wameonja ladha ya kujiheshimu na heshima. Watu wa Kufa wamesikia tu hotuba wakati ambapo mashahidi wa Karbala walisikia na wakatenda juu ya hotuba hizo. Walikwenda chini ya kina cha Karbala wakati ambapo watu wa Kufa hawakuweza hata kufikia fukwe zake; walishindwa katika hatua ya mwanzo ya mtihani wenyewe.

Karbala ni jina la bahari ya damu. Kwa nini watu wa Kufa waliogopa walipomuangalia Ubaidullah? Hii ilikuwa ni kwa sababu walilielewa hili sana kwamba kusema mbele ya Ubaidullah ni sawa sawa na kukanyaga ndani ya bahari ya damu. Usiku wa kabla ya Ashura Imamu Husein (as) alizima taa na akawapa maswahaba wake haki ya kidini (kuondoka na kumuacha), na ni kawaida kwamba watu hutafuta uhalali wa kidini kuokoa ngozi zao kutokana na jukumu lolote gumu. Hawa sabini na mbili walipata uhalali wa kidini katika usiku wa kabla ya Ashura wakati Imamu Husein (as) aliposema nimewaondoleeni kiapo chenu cha utii kwangu, wale

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 33



ambao wanataka kuondoka wanaweza kunufaika na fursa ya giza hili la usiku na kuondoka; kesho itakuwa ni pambano la mwisho ambamo kila mtu atauawa.

Hii ndio tofauti kati ya watu wa Kufa na Karbala. Hapa Ubaidullah mmoja na dhidi yake watu elfu sabini na mbili wanagwaya; wakati ambapo kule Karbala jeshi la watu sabini na mbili, taa inazimwa na wanaambiwa kwamba Mola wenu amewaridhia na Husein vilevile yuko radhi nanyi, hivyo mnaweza kuondoka. Lakini taa ilipowashwa tena kila mtu akasimama na kusema: "Ewe Bwana! Tumekuja hapa ili tuzame na kufa katika bahari hiyo ya damu na sio kuondoka hapa. Kwa nini unatuondoa kwenye fukwe hii, tumekuja kwenye fukwe hii na sasa tuache tuingie ndani ya bahari vilevile."

Mtu ambaye hayuko tayari kuogelea kwenye damu yake mwenyewe hawezi kuwa mtu wa kutoka Karbala. Mtu kutoka Karbala maana yake ni kuogelea katika damu na mtu wa Kufa maana yake kutingisha kichwa wakati wa kusikiliza hutuba lakini hukimbia wakati wa kuonesha ujasiri na kujiheshimu unapokuja. Mtu kutoka Kufa sio yule tu aliyezaliwa katika mji wa Kufa na katika kitambulisho chake kuandikwa kwamba sehemu yake ya kuzaliwa ni Kufa, bali badala yake mtu wa Kufa ni yule mwenye sifa bainifu za watu wa Kufa (wa zama hizo). Hii ni kwa sababu watu wengi waliokuwa wanaishi Kufa wakati huo hawakuzaliwa Kufa badala yake walizaliwa nje ya Kufa na kulowea katika mji wa Kufa na kwa vile tabia na sifa hizi zilipata kukua ndani yao basi wakawa watu wa Kufa. Imamu Husein (as) hakumlaghai mtu yeyote, hakumleta Karbala mtu yeyote pamoja naye kwa ajili ya kuwapotosha, hakumuambia yeyote kwamba twende pamoja na utapata Pepo, bali aliwaambia hata mkiondoka bado mtapata Pepo, hivyo hakuna haja ya kubakia na sisi hapo. Wafuasi wale wamekuja kwa unyofu wao wenyewe na walijua kuogelea katika damu yao wenyewe na sio mara moja tu hata kama Allah Aza wa Jallah awape maisha mara elfu na wafe mara elfu, na wakatwe vipande pande mara elfu na warudishiwe tena uhai bado watasema: "Tuko tayari kujitoa muhanga

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 34



maisha yetu miguuni mwako."

Leo pia ni wakati wa mitihani, kuna usiku mmoja wa Kufa na usiku mmoja wa Ashura. Ni nini kilichokuwa usiku wa Kufa? Usiku wa Kufa ulikuwa ni usiku ambamo Ubaidullah aliingia Kufa, ambapo usiku wa Ashura ulikuwa ni usiku ambamo Imamu Husein ibn Ali (as) alizima taa. Na sasa lazima tuthibitishe iwapo sisi ni waumini wa usiku wa Ashura au usiku wa Kufa. Iwapo tunataka kuwachukulia wale ambao wamejivalisha ukaya kama Imamu wetu au tunataka kusimama katika safu dhidi ya maelfu ya Ubaidullah na sio tu Ubaidulla mmoja. Iwapo tunataka kusimama dhidi ya madhalimu kama Shimr na Kholi ambao walizidiana wenyewe kwa wenyewe kwa ukatili? Wakati wa asubuhi ambao bila ya shaka tutakufa lakini kifo cha aina gani? Aina ile ya kifo ambacho miili kwanza itajeruhiwa, kisha vichwa vitatenganishwa na viwiliwili na mabibi watafanywa mateka, watachukuliwa kutembezwa mitaani, na pamoja na kufahamu yote haya bado lazima tuoneshe upinzani na uvumilivu mpaka tone la mwisho la damu yetu pamoja na Imamu wetu katika mapambano haya mashughuli. Mikesha hii miwili huja katika kila jumuiya, kwa maana kwamba aina hii ya usiku itakuja katika kila jumuiya, na sasa ni juu ya kila jumuiya kuugeuza usiku huu kuwa usiku wa Ashura au usiku wa Kufa. Watetezi wa imani lazima wafikiri kwamba leo ni usiku uleule, mkesha uleule, zama ileile na waamue ama kuufanya usiku wa Kufa au usiku wa Ashura. Katika usiku wa Ashura ni ukombozi ambapo katika usiku wa Kufa ni mauwaji.

Katika usiku wa Ashura mtu hukoga katika damu lakini kisha huishi milele wakati ambapo katika usiku wa Kufa mtu hupona (kifo) lakini hufa kifo cha fedheha kila siku. Katika usiku wa Ashura mtu hufa mara moja lakini huja katika uhai wa milele ambapo katika usiku wa Kufa mtu huishi mara moja na kufa milele. Hivyo, sasa ufumbuzi uko katika mikono yetu. Katika usiku wa Ashura hawakuambiwa kwamba kesho lazima mtauwa badala yake waliambiwa kwamba kesho lazima mtauawa. Hii ni Ashura na hili ni somo ambalo inalitoa kwa ajili ya jumuiya. Inatoa ujumbe huu kwa watu na wafuasi wa Ashura na Karbala. Ashura na Karbala inarudia rudia kuita

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 35



na kusema kwamba jumuiya ambayo hujifundisha kufa kamwe haiwezi kuuawa na yeyote na hakuna awezaye kuwaangamiza. Lakini wale wanaojaribu kuokoa maisha yao na kufanya juhudi kwa ajili ya ukombozi wao katika usiku wa Kufa wakidhania kwamba watapona, wala hauwezi kuwahifadhi kutokana na kifo. Leo lazima tuoneshe tofauti ya usiku wa Ashura na usiku wa Kufa. Madai ya imani peke yake hayatoshi na badala yake imani itatahiniwa na kujaribiwa. Mtihani mkali wa imani yetu unafanywa kupitia Ubaidullah; Allah Aza wa Jallah ameweka Ubaidullah katika kila zama na kuumba mtu mwenye ukaya kwa kila zama ili kwamba watu wawekwe chini ya hadaa kwa muda lakini siku moja anakuja kuvua ukaya wake. Kwa siku kadhaa watu walifikiri alikuja kuwauwa maadui zetu, lakini katika siku ya Ashura anaondoa ukaya wake na anasema amekuja kwa ajili ya kumuuwa nani; amekuja kuwauwa watu na wafuasi wa Ashura na Karbala.

Adui halisi sio yule aliyejifunga bomu au yule aliyedondosha bomu kutoka kwenye ndege; anaweza kuwa mfanyakazi aliyekodishwa au mtu ambaye amedanganywa, anaweza kuwa gaidi lakini kimsingi mtu ambaye anafanya yote haya ni Ubaidullah. Ulimwengu wote unagwaya kutokana na hofu juu yake, kambi za jeshi nazo pia zinagwaya, makao ya jeshi nayo vilevile yanagwaya na hata baada ya kutengeneza mabomu ya atomu bado wanagwaya. Tunahitaji Karbala na miili sabini na mbili dhidi ya Ubaidullah; wale ambao wamejifunza kukoga katika damu yao wenyewe. Ujumbe wa Karbala unatoa kipaumbele kwenye kifo pamoja na heshima kuliko maisha ya fedheha. Ujumbe wa Karbala ni wa kuondoa hofu ya kila mtu kutoka nyoyoni mwetu na kuiweka hai hofu juu ya Allah Aza wa Jallah tu. Kuishi maisha ya hofu juu ya watu wengine sio msingi wa heshima. Majeshi ya majivuno na ukiburi ya Yazid yanatawala Waislamu kwa kuwafanya waathirika wa hofu na woga. Karbala inatoa ujumbe huu kwa kila mwanadamu kwamba kama wewe ni Mwislamu na unayo imani juu ya Allah basi kamwe usiwe na woga wa majeshi haya yasiyo na kitu.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 36



Ujumbe wa Ashura ni kwamba chini ya mazingara yoyote hutakiwi ukae bila kuhusika kwenye dini yako, itikadi na kuhusiana na Waisilamu wengine. Ili kuwafanya msihusike na dini mashambulizi ya mabomu ya kujitolea muhanga hufanywa kwa ajili yenu, kwenye mikusanyiko yenu ya kidini na maandamano yenu yanapigwa mabomu, lakini hata kama vichwa vyenu vikikatwa kamwe usiache uwanja huu.

Ashura inatoa ujumbe huu kwa wanadamu wote na hususan Waislamu kwamba hata kama utajilowesha katika damu kamwe usijisalimishe kwa Yazid au dhalimu yeyote, usije ukatumbukia kwenye kisingizio na ulaghai wa Yazid yoyote, usiwafanye watu wenye ukaya kama Imamu na viongzi wako na wale wanyama (watu waovu) ambao kwa kuvaa shungi za upole, usitawi, uhuru na demokrasia wanaudanganya ulimwengu wote. Kamwe usiamini kaulimbiu zao za ulaghai.

Vilevile Karbala inatupa somo hili kwamba tusiifanye dini kama sehemu ya kukimbilia (kwa ajili ya hifadhi), bali badala yake wewe uwe ngao kwa ajili ya dini. Usichukue vitu kutoka kwenye dini na kuvitumia wewe mwenyewe na watoto wako badala yake toa muhanga mali yako, bidhaa, watoto na maisha yako katika dini.

Huu ni ujumbe wa Ashura kwamba ukweli na unyofu unakanyagwa na uwongo na uovu unaendelezwa, basi kamwe usiachilie majukumu yako kwa kuunga mkono ufafanuzi na uthibitisho. Pia Ashura hutuambia kwamba usiutoe muhanga ukweli na uhalisi kwa ubwana au kwa uthibitisho wa kimazingira hata ikiwa katika mazingira ya kinguvu. Karbala sio jina tu la kukata vichwa bali badala yake toa muhanga ubwana wako wote.

Ujmbe wa Karbala unatuambia kwamba badala ya kupoteza umri wako kwa ajili ya kungojea hali iwe nzuri na kuwa yenye kufaa, lazima usimame na kuchukua hatamu za zama katika mkono wako; kuliko kupigwa viboko na mazingira na kunyakuwa hatamu hizo kutoka kwenye mikono ya mazingira.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 37



Ashura inasihi ili kusikiliza kutoka kwa warithi wake kuliko kusikiliza kutoka kwa waigizaji wa tamthilia na walaghai. Wito wa Karbala ni imma kuwa shahidi kwa kuingia katika msafara wa Husein (as) au ubebe ujumbe wa mashahidi kwa kuingia katika msafara wa Zainab (as).

# SURA YA TATU

### *Hamasa -e- Husain*

*Hamasa -e- Husain ni* jina la Karbala, na shakhsia ambayo iliwasilisha tukio hili kwa jina hili na kulifanya kuwa mashuhuri, shaksia hiyo ilikuwa ni Shahidi Shia Mkubwa, Shahid wa Uislamu Allama Murtaza Muttahari (r.a.). Ni mkusanyo wa hutuba zake zinazohusiana na utambuzi wa Karbala, Ashura na Husein, kimeitwa *Hamasa-e-Husaini.* Hamasa sio neno la kawaida katika Urdu, fasihi ya Kiingereza, na kwa mahususi katika mazungumzo ya kawaida ya mtu ni nadra kutumika.

*Hamasa* inatokana na msingi uleule ambako Hamasa imetengenezwa, yaani ni chama cha Wapalestina (jina ambalo) leo ni kawaida kabisa katika vyombo vya habari.

*Hamasa* ni neno la Kiarabu ambalo hutumika kwa maana mahususi. *Hamasa* hurejea kwenye hatua mahususi au kitendo ambacho kina taaluma mahususi ndani yake:

Taaluma ya **Kwanza** ni kwamba ni kitendo na hatua.
Taaluma ya **Pili** katika maana ya Hamasa ni kuwepo kwa harakati katika hatua au kitendo; na lazima kisiwe na utuliaji. Ni dhahiri kwamba wakati wowote kunapokuwa na harakati vitu vyote muhimu kwa harakati hiyo lazima viwepo:

Kwa ajili ya harakati kuna haja ya mtu ambaye hutia hamasa au mtu ambaye huanzisha kitendo au mtu ambaye huingia katika kitendo.

Kitu cha pili ni ujuzi wa lengo ambalo kwalo harakati inafanywa.

Kitu cha tatu ni njia ambayo kwamba huhitaji kupitia ili kufikia lengo hilo. Hivyo harakati ni jina la kupitia njia ili kufanikisha lengo mahususi. Kwa hiyo, taaluma ya pili ya *Hamasa* ni kwamba hutokana na kabila la kitendo na hatua ya harakati. Lazima itokane na familia ya harakati na lazima ichukuliwe kama harakati, lazima isiwe na utuliaji na udororaji, kwa sababu kwa kawaida utuliaji na udororaji vilevile huchukuliwa kama aina fulani ya matendo. Kama vile mtu akiulizwa: unafanya nini siku hizi? Jibu ni siku hizi tuko kimya; hivyo kuwa kimya na bila kufanya kitu vilevile huchukuliwa kama kitendo cha mwanadamu, lakini nafsi na utambulisho wa *Hamasa* unakuwa na harakati.

Kitu cha **tatu** cha *Hamasa* ni ujasiri. Kitendo kitatajwa kama *Hamasa* wakati tu kitapokuwa na elementi za ujasiri ndani yake; hii ina maana kwamba kitendo cha kijasiri na hatua ya kijasiri ni *Hamasa*.

Matendo na hatua ni ya aina tofauti; baadhi ya matendo yanakuwa kiasi kwamba ujasiri hupata udhihirisho wa wazi ndani yao ambapo katika baadhi ya matendo woga huonekena kwa wazi. Halikadhalika kuna baadhi ya wanadamu ambao wana ujasiri ambapo kuna wengine ambao hawana elementi za ujasiri ndani yao. Halikadhalika na maneno pia; baadhi ya maneno huwa na matokeo ya sentensi zenye ujasiri na baadhi ni ya woga, kama vile unaposoma makala kwenye magazeti kuna baadhi ya waandishi ambao huandika makala za ujasiri ambapo baadhi huandika makala za woga. Hata katika mazungumzo ya kawaida ya watu wawili, kama mjadala unahusu unyofu na haki, na kama mtu anataka kuchukua haki yake kutoka kwa mtu fulani basi atafuata aina mbili za sauti; anaweza kufuata sauti ya ushujaa au sauti ya woga. Anaweza kuongea kwa lafudhi ya ujasiri au lafudhi ya woga. Utakuwa umeona kwamba katika mazungumzo ya kawaida halikadhalika baadhi ya watu wana mijadala na mazungumzo ya ujasiri na yenye ari, ambapo baadhi ya wengine wanajiingiza katika mijadala ya woga na yenye fedheha. *Hamasa* ni hatua ile ambayo kwayo ujasiri, ari na

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 39



ushujaa unapatikana ndani yake.

Elementi ya **nne** ambayo hufanya kitendo kama Hamasa ni elementi ya mapambano (*Moqawamat*) na msimamo (*Istiqamat*). Kitendo kile ambacho kina elementi ya msimamo ndani yake kitatajwa kama *Hamasa* au katika maneno mengine kitendo hiki kimefanywa kuzuia kitu fulani (au kupinga kitu fulani). Mtu hufanya vitendo vingi ambapo kati ya vitendo hivyo ni vya kufika sehemu fulani, baadhi ni vya kutambua vitu fulani, baadhi ni vya kupata kitu fulani, baadhi hufanywa ili kutoa kitu fulani kumpa mtu fulani, lakini baadhi ya vitendo vilevile ni vya kupinga au kuzuia kitu fulani. Kwa mfano, kama mafuriko ya maji yanakuja mtu huchukua hatua fulani kuyasimamisha yasisonge mbele. Hiki ni kitendo ambacho hutajwa kama cha mapambano (*Moqawamat*). Hii humaanisha kwamba unaweza kutengeneza kizuizi kama hicho mbele yake ambacho kitasimamisha maji kupita, na kitendo hiki kitatajwa kama mapambano (*Moqawamat*) na msimamo (*Istiqamat*).

Wakati elementi hizi nne zikijikusanya katika kitendo, kitendo hicho kitatajwa kama *Hamasa*. Hivyo, kwa mukhtasari kitendo cha *Hamasa* kina elementi nne: Kitendo, Harakati, Ujasiri na Mapambano.

*Hamasa* ni neno la Kiarabu lakini mara kwa mara hutumika katika Kiajemi na sio la kawaida katika Urdu na Kiingereza.[1] Kwa vile neno *Hamasa* haliwezi kutafsiriwa katika neno moja katika Urdu na Kiingereza huhitaji maelezo na kuna haja ya kulifungua neno hili. Ni muhimu kuelewa idadi ya maana na vipengele vya kuelewa vilivyofichwa ndani ya *Hamasa*.

Ili kuifanya akili yako iwe na ujuzi wa neno *Hamasa*, ili uelewe *Hamasa* ni nini, ngoja tuingie ndani ya neno la ushairi na uhutubu. Katika ushairi neno *Hamasa* hutumiwa mara kwa mara. Ushairi na uhutubu ni wa aina mbili; uhutubiaji wa *Hamasa* na uhutubiaji usio wa *Hamasa* au wa ushairi.

1. Neno Hamasa hutumika sana katika Kiswahili na ni neno lililoazimwa kutoka lugha ya Kiarabu na mnyambuliko wake katika Kiswahili mfano wake ni: Hamasisha, hamasika nk. (Mtarujuma)

Ingawa kuna aina mbali mbali za mashairi ambayo ni mashuhuri kwa watu wa fasihi na mashairi, wanajua vizuri sana aina tofauti za tenzi na mashairi. Katika aina hizi mahususi za ushairi hujulikana kama ushairi wa Hamasa; hilo shairi ambalo lina elementi za ujasiri ndani yake, shairi ambalo hutolewa kwa ajili ya kumuamsha mtu fulani. Shairi kama hilo litatajwa kama shairi la *Hamasa* ambalo liko kinyume na mtindo mwingine wa shairi ambao ni wa kuficha, usitiri au kutiisha kitu fulani. Mashairi yanayosomwa wakati wa mapambano ili kuwanyanyua na kuwatayarisha wapiganaji wa vita takatifu hujulikana kama mashairi ya *Hamasa*. Kwa ujumla haya pia hujulikana kama nyimbo za kizalendo ambazo hutolewa kama mashairi yaliyotengenezwa kwa ajili ya kuwasifia askari na watu mashujaa. Hivyo shairi ambalo lina mwito wa kuchukua hatua na ile hatua ya kiujasiri pia ni shairi la *Hamasa*. Katika Urdu washairi wengi wamefariki ambao mashairi yao yana elementi hii ya *Hamasa* ndani yake na katika lugha nyingine pia washairi kama hao walikuwepo, kama katika lugha ya Kiarabu pia walikuwepo washairi ambao mashairi yao yalikuwa na elementi za *Hamasa* ndani yake.

Halikadhalika makhatibu na wazungumzaji pia ni wa aina mbili; baadhi ya wazungumzaji wapo ambao hutuba na lafudhi zao zina Hamasa ndani yake. Kwa mfano, kama ukiangalia katika *Nahjul Balagha*. Kama unataka au unatamani kuona na kuelewa hutuba ya Hamasa basi lazima usome *Nahjul Balagha*; chukua hutuba yoyote na utaona kiini cha Hamasa; na mtu wakati anasoma atahisi mabadiliko ndani ya nafsi yake, na kwa kusoma hutuba hizi atapata mwelekeo wa kuchukua hatua kadhaa. Hili ndilo linalomaanishwa na hutuba ya *Hamasa*. Hivyo, sehemu kubwa ya hutuba za Amirul Muminin (a.s) katika *Nahjul Balagha* ni za aina ya *Hamasa*.

Ili kutambua cheo cha Karbala ni muhimu kuelewa aina ya uasi wa Wakuu wa Mashahidi. Mtu yeyote ambaye anavutiwa na tukio la Karbala katika hali yoyote lazima kwanza aangalie ni aina gani hii ya uasi ilikuwa, ilikuwa ni aina gani ya harakati ili kwamba aweze kufikiri na kutafakari kutokana na kadiri ile ile. Mtu ambaye hawezi kutambua ni uasi wa aina

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 41



gani huo uliokuwa atabakia amechanganyikiwa mpaka mwisho. Anakuwa amechanganyikiwa juu ya suala la Karbala na hawezi kuelewa kile anachosoma na kile anachosikiliza. Wakati mwingine anasikiliza aina moja ya mtazamo na akili yake huenda upande huo, kisha anasikiliza mtu mwingine akili yake huenda upande huo, na kisha kutoka kwa mtu wa tatu anasikiliza kitu fulani akili yake inaenda upande huo. Ni vigumu sana mtu kuelewa kitendo mpaka awe anafahamu kuhusu aina ya kitendo hicho. Kwa mfano, kuna mikusanyiko ya aina mbali mbali iliyoandaliwa ambayo kwayo baadhi ni ya aina ya semina, mikutano au aina ya kisomi ya wanachuo. Ni muhimu kwanza kuelewa ni aina gani ya mkusanyiko huo ili kwamba mtu aweze kuutazama kwa uoni huo na lazima aoneshe matumaini kwa mujibu wa aina ya mkusanyiko. Watu wengi wamejaribu kutambua ni aina gani ya tukio lililokuwa kwa tukio la Karbala. Pia tunaweza kusema kwamba wale ambao walijaribu kuitambua Karbala au aina yake wamekuja na uoni (visheni) ishirini tofauti juu ya tukio la Karbala.

Ishara kuelekea kwenye hizi visheni ishirini zimo kwenye chapisho letu la hapo awali kwa jina la "*Philosophy of Qayam-e-Hussain*". Katika kitabu hiki pia ni orodha tu ya hizi visheni ishirini pamoja na maelezo mafupi hutajwa kwamba ni aina gani ya majina ambayo watu wameiita Karbala kwa fikra na uchambuzi wao. Bani Umayyah wameipa (Karbala) jina moja, Bani Abbas wameipa jina moja lingine, baadhi ya wachambuzi wasio Waislamu wameipa jina moja lingine, wanahistoria kama vile Ibn Khaldun ameipa majina fulani, baadhi wameipa kitu kingine kama hiki madhehebu ya Imamiya (wafuasi wa Maimamu 12), na wasio wafuasi wa Imamiya kila mmoja amesema kitu ambacho ni cha kiutambuzi kama tutahesabu kufikia majina ishirini tofauti. Miongni mwa moja ya majina haya ni kwamba tukio la Karbala ni Hamasa na jina hili linawafikiana na Karbala na linafaa kwa tukio hili. Kwa majina mengine pia kuna udhihirisho, uthibitisho na kuna maelezo, lakini jina la kutosheleza zaidi ambalo huipaka rangi picha ya kweli ya tukio hili ni hili la Hamasa, kwa sababu jina lazima lichukuane na muktadha na lengo. Kwa kawaida tunaweka majina mazuri kwa vitu ambavyo kwa kweli sio vizuri kama jina lenyewe.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 42



Tunajenga kibanda na kuandika juu yake Chuo Kikuu. Chuo kikuu ni sehemu (changamani) kubwa ya kitaaluma, basi ni nini hiki ambacho umekipa jina la Chuo Kikuu? Kama hivi kuna majina mengine mengi ambayo hayaoani na suala lenyewe wala na muktadha. Kwa njia hiyo hiyo mwanadamu pia huweka jina zuri kwa ajili yake ambalo si stahiki yake. Tunawapa majina mazuri watu ambao hawafai ingawa jina na muktadha havina uhusiano. Jina zuri na lenye kufaa ni lile ambalo linaafikiana na muktadha wake.

Hamasa ni neno ambalo lina elementi iliyotajwa awali. Sasa tunahitaji kupima iwapo uasi mtakatifu wa Wakuu wa Mashahidi na Karbala ni Hamasa. Lakini kabla ya kuonesha na kuelekea kwenye uhusiano huu kwamba ni kwa nini uasi huu unatajwa kama Hamasa na iwapo unabeba ndani yake elementi ya Hamasa, kwanza tunahitaji kuona ni aina ipi ni Uislamu? Uislamu ni dini ya aina gani? Hii ni kwa sababu Karbala ni uasi wa kidini, ni uasi wa Kiislamu, kwa hiyo, hatuwezi kutenganisha Karbala na Uislamu na kuliita kwamba ni tukio au ajali. Tunahitaji kuangalia kwenye uasi wa Karbala na Wakuu wa Mashahidi katika mtazamo wa Uislamu, dini na Qur'ani. Hivyo kabla ya Karbala kwanza lazima tuangalie jina la Uislamu ni lipi? Uislamu ni aina gani ya dini?

Kuna dini mbalimbali zilizopo hapa duniani na kuna wafuasi wengi wanaofuata dini hizi ambao pia wapo hapa ulimwenguni. Leo tunaweza kuona dini zenye kumuamini Mungu na halikadhalika zisizoamini Mungu. Zile zisizoamini Mungu ni zile ambazo uhusiano wao na ufunuo bado haujathibitishwa, bado haujathibitishwa iwapo kuna kitabu chochote cha Mungu au Mtume mwenye kuhusiana na dini hizi, kama vile Uhindu na Ubudha, ingawa pia katika mafundisho ya dini hizi vitu fulani huonekena ambavyo kwavyo tunafahamu kwamba kuna elementi za ufunuo ndani yao; lakini hakuna ushahidi ulio sahihi ambao unaoweza kuthibitisha hili kuwa hizi ni dini za mbinguni, na hakuna kitabu cha kimungu au Mtume ambaye ametajwa kuhusiana na dini hizi. Amma kwa baadhi ya dini kuna ushahidi kwamba hizi ni dini za mbinguni, kama dini ya Wayahudi ambayo

ina misingi ya kimbinguni, Ukiristo ni dini ya kimungu na Uislamu ambao huweka msingi wa kimungu ambao kwa usahihi huhusika na ufunuo, ingawa kuna uwezekano kwamba upotofu umejipenyeza ndani ya Ukristo na Uyahudi. Mafundisho yao yamepitiwa na ufisadi na kubadilishwa, lakini kuanzia mwanzo msingi wao ulikuwa juu ya ufunuo.

Katika dini hizi mbali mbali ambazo leo zipo hapa ulimwenguni tunaweza kuona aina mbali mbali za dini na tunaweza tukapendekeza majina yafaayo kwa ajili ya dini hizi kama vile Useja. Jina hili la Useja linafaa kwa baadhi ya dini ambazo kwa mujibu wa Allama Iqbal ni dini ya Sufi au dini ya utawa. Kuna dini fulani na sura za dini ambazo kwazo jina hili linazifaa na huweza kuitwa hivyo. Allama Iqbal amewasilisha sura mbali mbali za dini katika vitabu vyake. Moja ya majina hayo ni dini ya Mbweha ambayo ni dini ya ulaghai. Kuna sura fulani za dini ambazo kwa asili ni za umbweha (ulaghai) wakati ambapo baadhi ni kama zile za Simba. Katika vitabu vya Allama Iqbal kuna dini ya Simba. Vivyo hivyo kuna dini ya kutiishwa au dini ya watumwa. Sura fulani za dini zipo kwa namna kwamba jina bora linalofaa kwa dini hizo ni Dini ya Watumwa. Dini ya Watumwa imo kwenye vitabu vya Allama Iqbal. Amezungumzia kuhusu dini ya watumwa, sala za watumwa, ibada ya watumwa, jinsi ya kusujudu kwa watumwa, madhehebu ya dini za watumwa, misikiti ya watumwa, kila kitu ni cha kitumwa. Kama ni dini utawa basi hali ni hiyo hiyo ambapo kuna madhehebu ya utawa, misikiti ya utawa, elimu ni ile ya utawa.

Halikadhalika mafundisho ya Imamu Khomein (r.a) vilevile mna dalili za kuelekea kwenye sura mbali mbali za dini. Dini ya mabeperi ni jina la sura moja ya dini, dini ya ubadhirifu ni jina la sura nyingine ya dini; dini ya ubadhirifu maana yake ni dini ya anasa. Jina moja zaidi ambalo Imamu Khomein (r.a) amelitoa ni dini ya watu ambao wenyewe hujiona kama watakatifu (kama wanaojiita walokole huku kwetu) na bora zaidi (kama wanavyojiona Mayahudi). Dini moja ni ile ambayo huamini Mungu Mmoja asiye na mshirika ambayo Allama Iqbal anaitaja kama dini ya Mujahidina. Kwa mujibu wa maneno ya Allama Iqbal Adhana ya Kuhani

(Sheikh-kilemba) ni tofauti na Adhana ya Mujahidina. Maneno ni sawa kwa wote, wote huanza na "*Allahu Akbar* (Mungu ni Mkubwa) na kuishia na *La ilahaa ila llahu* (hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu-Mmoja), lakini jina linalofaa kwa maneno hayohayo ya Adhana ni tofauti. Wakati mwingine huu ni wito (Adhan) wa watumwa au wito (Adhana) wa makuhani, lakini wakati mwingine ni Adhana ya Mujahidina. Kwa mujibu wa Allama Iqbal Adhana ya Kuhani sio Adhana ya Swala ya Mujahidina, vipi basi tutajua aina ya Adhana hii ni ipi? Inatambulika kutokana na athari inayoiacha; je, kutokana na athari na dalili za dini inaweza kutambulika ni aina gani hiyo ya dini? Ni aina gani hiyo ya itikadi?

Baadhi ya dini na itikadi zaweza kuchukuliwa kama za kikuhani kwa sababu zina mwelekeo zaidi kwenye ukuhani. Mafundisho ya Ukristo yameelekezwa kuelekea kwenye ukuhani na dini yote imeelekea kwenye ukuhani. Dini ya Wayahudi ni ya kuabudu matabaka. Qur'ani Tukufu imejadili kuhusu dini zote hizi na kuelezea jinsi walivyo Mayahudi, walivyo Wakristo na walivyo Waislamu na walivyo Mazorostan.

Sura ambayo Mayahudi wanayo imeifanya dini kuwa na matokeo yaliyopo ya dini ya Uyahudi kutoka katika hali ya udini na kuigeuza kuwa kwenye sheria za jumuiya. Leo dini ya Uyahudi ni katiba na sio dini; na tunaweza kusema kwamba imekuwa ya tabaka sio dini. Kwa kawaida jina la jumuiya linawafaa vizuri sana na ni jina linalofaa kwa ajili yao. Kosa ambalo watu wa Magharibi (Ulaya) wamelifanya katika kuuelewa Uislamu ni kwa kuwaangalia Waislamu na hivyo kamwe hawawezi kutoa hitimisho sahihi. Kwa kawaida kwa kuwaangalia Waislamu Uislamu lazima uweleweke, lakini inasikitisha kusema Waislamu sio chanzo sahihi au cha kutegemea kwa kuuelewa Uislamu. Hivyo lazima uufahamu Uislamu kutokana na chanzo chake ambacho ni Qur'ani Tukufu, Sunnah ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kutoka kwenye sifa bainifu na simuluzi za Maimamu maasumu, kwa sababu hawa ndio vyanzo sahihi vya kutegemewa. Kama tutauangalia Uislamu kutoka kwenye vyanzo hivi, Uislamu uliowasilishwa na Qur'ani au Uislamu uliowasilishwa wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na picha

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 45



ya kimatendo ya Uislamu iliyowasilishwa na Maimamu maasumin, hauchukuani na majina mengine yoyote. Jina la utawa halifai kwa Uislamu huu wa kweli, jina la useja pia halifai kwa Uislamu uliowasilishwa na Qur'ani na sifa bainifu za maasumin. Jina la utaalamu halifai kwa ajili yake, jina la ubadhirifu halifai, mfumo wa ubepari haufai kwawo. Majina haya yako nje ya muktadha.

Jina kwa ajili ya Uislamu ambalo liko katika asili yake lazima litoke katika maisha ya Waislamu. Kuna umbali mkubwa kati ya Uislamu wa Qur'ani na Uislamu wa Waislamu.Uislamu wa Qur'ani uko katika chanzo chake, kama ilivyo kuna madini na maliasili kama tulivyo na gesi, petroli lakini bado haikutoka kwetu. Kama katika nchi nyingi kuna petroli chini ya ardhi lakini mpaka sasa hakuna serikali yenye nguvu au mhandisi ambaye amekuja anayeweza kuleta maliasli hizi majumbani kwa kuchimba ardhini. Halikadhalika Uislamu haukutoka kwenye Qur'ani, Hadithi na kwa wabainifu na kuingia kwenye maisha yetu. Imamu Khomein (r.a) alisema kwamba Waislamu wameupoteza Uislamu kutoka mikononi mwao na unahitaji kufanyiwa utafiti. Leo majina mengine mengi yanafaa kwa Uislamu uliopo mikononi mwa Waislamu ambayo yamejadiliwa na Allama Iqbal na yanaonekana katika simulizi za Imamu Khomein (r.a); lakini tunahitaji kutafuta lile jina lenye kutosheleza ambalo liko katika Qur'ani, Hadithi na wabainifu. Jina ambalo hupatikana kutoka katika chanzo na asili ya Uislamu ni kwamba Uislamu ni dini ya *Hamasa* na kimatendo, Uislamu ni wa aina ya *Hamasa*. Sio dini ya useja, utawa, udororaji na utuliaji; badala yake Uislamu ni wa aina ya Hamasa, yaani ina elementi nne ndani yake. Katika hali hiyo hiyo Ushia vilevile ni Hmasa na sio madhehebu. Hulichukulia hilo kama mafanikio makubwa katika kuufanya Ushia kama madhehebu; madhehebu maana yake ni kitu ambacho kimetenganishwa na kuondolewa. Kama matokeo ya kutokuelewana na utengano, kundi moja huenda sehemu fulani, lingine huenda sehemu nyingine na kundi moja likapata jina la Ushia na kundi lingine likapata jina lingine fulani.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 46



Hili ni dhana katika kuelewa misingi ya Ushia. Ushia sio madhehebu ya Uislamu, kwa kweli ni jina la kimatendo la Uislamu, Ushia ni Qur'ani, Ushia ni ubainfu wa Maasumin. Wakati mwingine watu wanauliza Ushia ulianza lini. Ulianza siku ileile Uislamu ulipoanza. Kutoka siku ile yenyewe Ushia ulianza kama sura ya Uislamu, sio Ushia ule ulioanzishwa baadae. Sio wakati ule wa baadae ambapo mlango ulifunguliwa au dirisha lilipofunguliwa ambapo ulipewa jina la Ushia. Amri ya kwanza ya Uislamu ambayo ilikuja katika siku ya kwanza ya Uislamu ilikuwa kwa sura ya Ushia.

Ushia ni jina la kipengele cha kimatendo ya Uislamu; yaani ili kuonesha ni aina gani ya dini ya Uislamu; ulipewa jina la Ushia ili mtu yeyote asipate taabu katika kuelewa aina hii ya Uislamu. Kwa kawaida bidhaa ambazo ziko sokoni zina alama fulani zilizoandikwa katika kifurushi chake ili kwamba aina ya vitu vilivyomo ndani ya kifurushi hicho vijulikane. Iwapo mna vitu vya kuvunjika au visivyovunjika, iwapo ni kitu ambacho kinaweza kunyanyuliwa kwa urahisi au huhitaji tahadhari. Huweka juu yake alama yoyote au kuandika kitu fulani ambacho huwa jina lake ili kuonesha aina gani ya kitu kimo humo ili kwamba ukichukulie kwa kadiri kilivyo.

Ushia maana yake ni sura ya kimatendo ya kuufuata Uislamu, ni jina la Uislamu ambalo lilichaguliwa na mwenyeji wa Uislamu, Mtume wa Uislamu. Hivyo Uislamu utakuwa katika aina mbili, moja ni aina ya Uislamu ambayo ni kama lilivyo jina lake ambalo ni la Uislamu wa kimatendo na aina ya pili itakuwa ni Uislamu usiokuwa wa matendo.

Jina la Uislamu wa kimatendo ni Ushia, hivyo, popote ambapo Uislamu hauko katika muundo wake wa kimatendo vilevile hakuna ushia ambapo humaanisha Uislamu uliopo sio Uislamu wa ushia. Sio Uislamu wa kimatendo, ni Uislamu wa mawazo tu, Uislamu wa kufikiria, Uislamu wa fasihi, Uislamu wa maneno na Uislamu wa ulimi ambao humaanisha kuzungumza tu na kujikomba.

Kuna kauli maarufu ya Kiongozi wa Mashahidi:

النّاس عبيد الدّنيا والدّين لعق على ألسنتهم

"Watu ni watumwa wa ulimwengu; na dini iko tu kwenye ndimi zao kwa ajili ya muonjo."

Ladha ni ya muda tu katika ulimi, na mbali na ulimi hakuna kiungo kingine kinachohisi ladha na haikukusudiwa kwa ajili ya kiungo kingine chochote. Hisia ya kuhisi ladha imewekwa tu kwenye ulimi, yaani kama kitu kikipita kwenye ulimi basi ladha yake inajulikana. Ladha inaweza tu kuhisiwa mpaka muda wa kuwepo kwenye ulimi na ndani ya kinywa.

Baadhi ya watu wameuweka Uislamu kwenye taya chini ya ulimi na ladha vilevile huendelea kubadilika. Wakati mwingine kwa muda kidogo ladha huwa chungu na wakati hili likitokea vitu vya ladha hiyo hutemwa chini. Hiki ndicho ambacho Kiongozi wa Mashahidi alichokusudia kusema kwamba Dini imeingia kwenye ndimi zao kama muonjo tu.

إذا محصّوا بالبلاء قلّ الدّيانون

Wakati ladha ya dini inapokuwa chungu kwa haraka wanaitema.

Je, umewahi kuona watu wakiitema dini? Utakuwa umeona watu wakitema tumbaku, lakini je, umewahi kuona watu wakitema dini? Watu wanatema dini kwa wingi sana, fungua tu macho yako utaona watu kila mahali wakitema dini, uchungu wowote ule unaowapitia upesi sana huutema. Hiki ndicho anachosema Kiongozi wa Mashahidi, anachosema kwamba aina moja ya dini ni hii na halikadhalika ambako dini iko kwenye ncha za ulimi, mara ikiwa chungu wanaitema; kwa njia ambayo watu wa Kufa walifanya. Walikaa kimya ndani ya nyumba zao na hawakuenda Karbala; hii maana yake ni kuitema dini. Kuitema dini sio kama kutema tumbaku ambako wekundu wa tumbaku unaweza kuonekana sehemu yote. Maana ya kutema dini ni kuwa kimya, kutojihusisha na lolote kuhusiana na dini, kutema dini ni kutowajibika, kuwa kimya bila vitendo, kuwa muoga, kutema dini ni

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 48



kufunga midomo yenu na kukaa kimya ndani ya nyumba zenu na kuwaacha viongozi wa dini wakiwa wametengwa. Wakati watu wakiwa wamevaa *Ihram* (vazi la Hijja) wakienda kuhiji Kiongozi wa Mashahidi aliwataka wavue *Ihram* zao na waungane naye kwa sababu kesho anakwenda sehemu nyingine. Umma unakwenda kuhiji, wakati ambapo Kiongozi anatoka kwa ajili ya kuilinda Hijja. Aliwataka wavue *Ihram* zao kwa sababu siku hizi hazikuwa za kuhiji bali kuilinda Hijja. Lakini walikataa kuungana naye, hivyo, nini maana ya wao kutoungana naye?

Walivaa *Iharam* zao na wakaenda Arafa; Walivaa *Iharam* zao na wakaenda Mina ambapo maana yake wanaitema dini. Sio kwamba mtu anayeswali, kufunga, kuhiji na kufanya Azadari hatemi dini. Kama mtu anakwenda kuhiji kwa kumpa mgongo Imamu, basi hii ina maana ameitema dini. Watu wa Kufa walikuwa wakitekeleza swala zao baada ya kumuacha Imamu wao na hakuna swala yao iliyokuwa kadha, lakini bado walitema dini. Hivyo, je, Uislamu ni kwa ajili ya muonjo tu ambao hufika kwenye ulimi ukihitajika na wakati ukigeuka kuwa mchungu unatemwa?

Aina ya Uislamu ni ile ya *Hamasa*, Uislamu ni *Hamasa*, nafsi ya Uislamu iko kwenye *Hamasa* lakini kuna baadhi ya watu waliozaliwa wenye vipaji, ujuzi na uwezo ambao wamefanya maajabu miongoni mwa Waislamu. Ajabu moja kubwa waliyoifanya ni kwamba waliivua nafsi ya Uislamu kutoka kwenye muungo wake. Allama Iqbal anao utenzi mmoja kwa jina la Amri ya Iblis kwa watoto wake wa kisiasa. Ni utenzi wenye beti chache:

"Dawa ya Waislamu ni kuwaleta kwenye misikiti na sehemu za kuabudia, lakini uondoe nafsi ya Muhammad kutoka kwenye nyoyo zao, yaani nafsi ya Muhammad na roho ya Qur'ani lazima iondoke kwenye nyoyo za Waislamu. Lazima waondokane na nafsi ya Husein ndani yao."

Ubeti wa mwisho ameuandika kuhusiana na yeye mwenyewe:

"Moto wa Tulip unawaka pamoja na nafsi ya Iqbal. Muondoe msomaji wa

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 49



utenzi huu kutoka bustanini."

Iqbal ameandika ubeti huu kama utenzi wa kifo chake cha kishahidi, lakini kwa vile Pakistan haijaundwa wakati huo, hakufanikiwa kupata kifo cha kishahidi. Kama Pakistan ingelikuwa imeundwa basi hamu hii ya Iqbal vilevile ingeliweza kutekelezwa.

Shetani anaagiza kuondolewa kwa nafsi ya Uislamu. Ajabu kubwa ambayo watoto wa kisiasa ya Shetani wameifanya ni kwamba wameondoa nafsi ya *Hamasa* ya Uislamu na badala yake wakawasilisha Uislamu usio na *Hamasa* na kuwaambia Waislamu watengeneze kibweta kutokana na Uislamu huu usio na *Hamasa* na kuvaa shingoni mwao (ili kupata malipo).

Uislamu wa *Hamasa* ni huu ambao una mambo manne:
Jambo la kwanza ni **kitendo,** na kitendo hiki ni Ushia huu huu. Ushia na kitendo ni maneno mawili ya shukurani, kama ukisema kitendo au Ushia ni tafsiri ya kitu hicho hicho.

Jambo ja pili ni **harakati**. Sababu ya Uislamu kuwa ni *Hamasa* ni kwa sababu Uislamu sio dini ya udororaji; ni dini ya itikadi na harakati. Haitaki udororaji mahali popote na hauridhiki na udororaji na utuliaji. Kamwe hauhubiri kusimamisha au kuwa wenye kutulia iwe katika swala au katika matendo, au katika nia, au katika elimu, katika malezi ama katika mahusiano, hausemi katika sehemu yoyote kwamba wewe kusimama hapa ndio bora. Uislamu hauchukui jina la kusimama; ni jina la harakati ya kudumu. Hauna hata uwezekano mdogo wa udororaji. Kuna hadithi moja isemayo:

من استوى يوماه فهو مغبون

"Ni mwenye hasara mtu ambaye siku zake mbili zimelingana."

Katika sehemu nyingine neno mlaniwa linatumika:

من استوى يوماه فهو ملعون

"Ni mlaaniwa mtu ambaye siku zake mbili zimelingana."

Katika harakati hakuna siku mbili za mtu zinazopita hivi hivi kwa sababu mtu mwenye harakati siku moja anakuwa sehemu moja, na siku ya pili anakuwa sehemu nyingine. Mtu anayekaa hivyo hivyo kwa muda wa siku mbili sio Mwislamu. Mwislamu ni yule ambaye siku moja yuko kwenye kitu fulani na siku ya pili amesonga mbele. Hili ndilo linalomaanishwa na harakati; gari linalotembea linakuwa sehemu moja katika dakika moja na katika dakika inayofuata liko katika sehemu nyingine. Uislamu humuangalia mtu kama mwenye kuhangaika huko na huko.

Jambo la tatu ni **ujasiri,** na katika mafundisho yote ya Uislamu elementi ya ujasiri iko mbele. Katika mafundisho ya kawaida kama ya maadili vilevile kuna ujasiri. Maadili ya useja ni tofauti na maadili ya Uislamu. Maadili ya maseja au watu wanaopendelea utawa huyeyusha ujasiri wa watu mashujaa. Kwa kuwasilisha maadili ya useja wanajaribu kuwafanya watu kuipa nyongo dunia (*Zahid*). *Zahid* (zuhudi ni mtu anayependa kujitenga,) na useja humaanisha ubinafsi tu.

Sheikh Saadi anaandika kwamba Sufi mmoja alitoka kwenye sehemu yake ya utawa na akaja kwenye shule ya dini. Watu walishangazwa ni kwa nini ametoka kwenye sehemu yake ya utawa wa ibada na kuja shuleni. Wakati alipoulizwa alijibu kwamba watu ambao wanakaa kwenye sehemu za utawa za ibada ni wachamungu sana na wenye Zuhudi, hawali chakula cha haramu, hawasengenyi, hawatendi dhambi, si kwa macho yao, wala kutokana na ndimi zao, wala sio kwa mikono yao; kwa hakika wao ni malaika na unaweza kuwa malaika kwa urahisi sana. Ili kuwa malaika huhitaji kufanya juhudi kubwa. Allama Iqbal anasema kwamba ni bora mwanadamu kuliko kuwa malaika, hivyo kuwa malaika ni rahisi, lakini

kuwa mwanadamu ni vigumu.
Sufi huyu alisema: “Nimeondoka kwenye sehemu ya utawa wa ibada kwa sababu pale watu ni wazuri sana na hawafanyi dhambi yoyote lakini pamoja na hayo sikuweza kukaa pale kwa sababu lengo lao kubwa ni kupata wokovu kwa namna fulani kwa wao wenyewe, wanakesha siku arobaini za mafunzo ya ibada ili kwamba waweze kufika sehemu fulani. Na nilikiona kitendo hiki kama cha kibinafsi. Nimekuja kwenye shule hii kwa sababu shule ni sehemu ambako kuna ujamaa na elimu. Tofauti kati ya mwanachuo na *Zahid* ni kwamba *Zahid* hujipa ukombozi yeye mwenyewe ambapo mwanachuo hujikinga yeye mwenyewe na halikadhalika hutoa ukombozi kwa umma wote.”

Uislamu sio dini ya utawa katika muundo wake wa kimatendo, hakuna utawa na useja katika Uislamu na kuna hadithi ya wazi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba hakuna nafasi katika Uislamu kwa ajili ya useja.

Uislamu ni harakati na ujasiri; kila fundisho la Uislamu lina ushujaa na ujasiri ndani yake. Sio jihadi tu ambayo ina ujasiri ndani yake, kwa kweli kila kitendo kina ujasiri. Kuwa shupavu (ukaidi) sio ujasiri, ushupavu ni tofauti na ujasiri. Watu waoga mara nyingi huwa washupavu. Ujasiri mkubwa sio kumpiga mtu ngumi bali kitendo kikubwa cha ujasiri ni kukiri kwamba nimefanya kosa. Kwa hakika Uislamu hutoa na kulea watu majasiri. Mtu ambaye anakuwa na ujasiri wa kujilaani mwenyewe anaweza kumlaani mtu mwingine yeyote. Tatizo ambalo alikuwa nalo Ghazali ilikuwa kwamba hakuwa na ujasiri wa kujilaani mwenyewe, hakuweza kujilaani ingawa alikuwa mwalimu wa maadili, hivyo hakuwa na ujasiri hata wa kumlaani Yazid. Uislamu huo ni tofauti ambao unanyang’anya ujasiri kutoka kwa wanadamu kwamba kama nikimlaani Yazid huenda nikaenda motoni. Uislamu hauzai watu waoga kama hawa; ni itikadi ya ushujaa. Jina la ujasiri pia limo ndani ya vitendo vya Uislamu vya ibada; hakuna ibada ambayo iko tupu bila ujasiri. Katika ibada lazima uvunje majivuno yako na kuwa mfungwa na mtumwa; na kwa hili unahitaji

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 52



ujasiri.

Jambo la nne ni **upinzani** na uvumilivu. Kuna hadithi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliyosimuliwa na wengi:

شيبتنى سورة هود

"Surat Hud imenifanya mimi mzee."

Katika Surah Hud kuna kitu kama hicho ambacho pia kinajadiliwa katika sehemu nyingine ya Qur'ani Tukufu, lakini kimetajwa katika hadithi na pia wanachuoni wameandika kwamba kuna aya kama hiyo katika Surat Hud ambayo haipo mahali popote na hii ni aya ambayo imemfanya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aseme kwamba Surat Hud imenifanya mimi kuwa mzee. Aya hii ni:

فَٱسۡتَقِمۡ كَمَآ أُمِرۡتَ ﴿١١٢﴾

**"Basi (endelea kuwa mvumilivu) kama ulivyoamriwa juu yako." (11:112)**

Ni rahisi sana kusema "Hakuna mungu isipokuwa Allah" lakini kuonesha uvumilivu juu yake ni vigumu sana. Ni rahisi kusema kwamba Allah ni Mola wetu lakini kuwa imara juu ya hili ni vigumu sana. Kuna maelezo ya busara sana kutoka kwa Imamu Khomeini (r.a) kwamba ni rahisi kuleta mapinduzi lakini ni vigumu sana kuyalinda. Ni rahisi kuwa mwanamapinduzi lakini kubakia mwanamapindizi ni vigumu sana. Ni rahisi kusema "hakuna mungu isipokuwa Allah," lakini kuliendeleza hili ni vigumu sana. Mtu ambaye anasema Mola wangu ni Allah Mmoja hebu naajaribu kuliendeleza hili kwa muda fulani. Hii maana yake ni kwamba… baba yangu sio Mola wangu; ni baba yangu lakini sio Mola wangu………usimfikirie baba yako kama Mola wako…….usizifanye serikali kama Mola wako…….usiwafanye wateja wako kama Mola wako…….usiwafanye wakandamizaji kama Mola wako. Ni rahisi kusema kwamba Mola wangu ni Allah lakini kuonesha uvumilivu juu ya hilo ni vigumu sana. Ni rahisi kuifanya nchi

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 53



kwa jina la Uislamu lakini kuihifadhi nchi hii katika Uislamu ni vigumu sana, wanachosema leo ni kwamba kama tukitenda kinyume na matakwa ya Marekani tutakufa kwa njaa, kama tukitoa laana yoyote kwa Marekani na kama tukitoa kaulimbiu dhidi ya mtu fulani tutakufa kwa njaa.

Kwa nini ufe kwa njaa? Mungu aepushie mbali, je, dhati ya Allah haipo? Wewe ni Mwislamu? Una mategemeo juu ya Allah? una imani juu ya Allah?

Wanasema kile ambacho kitatokea Iran! Kila mtu katika ulimwengu ana wasiwasi wa kile kitakachotokea Iran! Ulimwengu wote hata wale ambao wanatishia wana wasiwasi kwamba tunatoa vitisho, lakini ni matokeo gani yatakayokuwa? Lakini kama utauliza uongozi wa Iran juu ya nini kitakachotokea; wanasema: “Mola wetu ni Allah.” Kama mtu ataelewa hili kwamba Mola ni Allah Peke Yake na hakuna uongozi wa yeyote yule mbali na Allah, na anaonesha uvumilivu juu ya hili hakuna mtu atakayemtisha. Aya moja zaidi ambayo Imamu Khomein (r.a) mara kwa mara ameisema katika hotuba zake ni kwamba: Allah anasema:

۞ قُلْ إِنَّمَآ أَعِظُكُم بِوَٰحِدَةٍ ۖ أَن تَقُومُوا۟ لِلَّهِ مَثْنَىٰ وَفُرَٰدَىٰ ﴿٤٦﴾

**“Na nawawaidhi tu kitu kimoja, kwamba simameni kwa ajili ya Allah mkiwa wawili wawili na mmoja mmoja.” (Sura Sabai: 46)”**

Imamu Khomein katika muktadha wa aya hii anasema: “Allah anawaambia tu kitu kimoja; sisemi maneno makubwa, na kwamba kitu kimoja ni kwamba simameni tu kwa ajili ya Allah. Simameni kwa ajili ya Allah, hata kama uko peke yako, hata kama mko wawili simameni kwa ajili ya Allah, hata kama kumi wakisimama kwa ajili ya Allah; kama ninyi ni umma mmoja pia simameni kwa ajili ya Allah, na kama mko katika mamilioni basi pia simameni kwa ajili ya Allah.”

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 54



قولوا لا إله إلاّ الله تفلحوا

Sema “*La ilaha ila llahu*” (hakuna mungu ila Allah) na mtapata uogofu.

“*La ilaha ila llahu*” sio kitu cha maneno matupu, ni kitu ambacho lazima kifanywe na sio kusemwa tu. Kutenda “*La ilaha ila llahu*” maana yake ni mapambano (*Moqawamat*) na msimamo.

Kuna mambo fulani ambayo kudumu kwake hutegemea juu ya mapambano na uvumilivu. Kudumu kwa Uislamu, kudumu kwa Waislamu, kudumu kwa umma wa Kiislamu kwa uhalisi kumefichwa ndani ya mapambano (*Moqawamat*) na uvumilivu. Hii ndio sababu Uislamu ni aina ya *Hamasa*. Mapambano (*Moqawamat*) yapo katika kila mshipa wa mafundisho ya Uislamu, ni sawa na kuufungua mshipa wowote wa mwanadamu ambako ni damu tu huonekena. Ingawa kama ukifungua mishipa ya Waislamu vitu vya ajabu na kushangaza vitaonekana, lakini kutoka kwenye mishipa ya Uislamu kitakachotoka ni Mapambano na Uvumilivu. Jina la pili la Uvumilivu ni Uislamu na hii ndio sababu kwamba Uislamu ni wa aina ya *Hamasa*.

Picha ambayo Ukristo umeionesha kwa Mtume Isa (a.s) ni kwamba alikuwa mtu mzuri sana, kwa nini alikuwa mtu mzuri? Hii ni kwa sababu katika mafundisho ya Ukristo inafundishwa kwamba kama mtu akikupiga kofi shavu la kulia basi mgeuzie na shavu lako la kushoto. Hii ni kwa sababu mtu ambaye anapiga kofi shavu moja lazima ageuke ili akuchape kwenye shavu lingine na hivyo mtu yule anayekuchapa atapata taabu, hivyo lazima ugeuze upande huo wewe mwenyewe ili wakati akikuchapa upande huo wa pili asipate shida hii. Lakini picha ambayo Allah ameionesha kwa Mtume Isa (a.s) katika Qur’ani ni kitu tofauti kabisa. Isa wa Qur’ani ni kitu kingine wakati ambapo Isa wa Wakristo ni mtu mwingine. Qur’ani imewasilisha picha ya Isa (a.s) kama ile ya *Hamasa*, wakati ambapo Ukristo umemuonesha kwa picha ya useja na utawa. Kuna aina

tofauti za umma, baadhi ya jumuiya ni jasiri na zenye moyo; utamaduni wao una ujasiri, lakini baadhi ya jumuiya zina woga na zilizodhalilishwa na hakuna ujasiri katika utamuduni wao. Na kwa kuwa kwao hivyo wako mbali na dini bali pia waoga katika utamuduni wao. Hakuna *Hamasa* ndani yao, na *Hamasa* itatoka kwenye Qur'ani na Uislamu kwa sababu *Hamasa* ipo ndani ya Uislamu.

Hivyo kuasi kwa Kiongozi wa Mashahidi kulikuwa kwa *Hamasa* ambayo humaanisha kwamba wakati ukimya na udororaji ulikuwepo juu ya umma wote, Kiongozi wa Mashahidi alianzisha uasi. Udororaji wa umma ni kosa kubwa mno; ukimya wa umma ni utovu mkubwa mno wa utii. Imamu Husein (a.s) anasema kwamba miongoni mwa ibada zote iliyo tukufu ni jihadi na jihadi tukufu zaidi ni kusema ukweli mbele ya mfalme dhalimu.

Kiongozi wa Mashahidi hakusema kwamba nimelazimishwa kuondoka Madina, alisema ninaondoka Madina. Karbala ile ambayo Husein ibn Ali aliianzisha ni tofauti na Karbala ya makhatibu na wahubiri. Karbala ya wanahistoria ni tofauti, Karbala ya waandishi ni tofauti, Karbala ya wataalamu ni tofauti, Karbala ya wale wanaouza mikate (kwa ajili ya sadaka ya Azadari) ni tofauti, Karbala ya wale wanachukua ada ni tofauti na kila mmjoa anayo Karbala yake mahususi, lakini kuna Karbala moja ya Husein ibn Ali. Sasa je, tunahitaji kutafuta Karbala ambayo ni yetu? Je, leo tuko kwenye Karbala ipi?

Tutaielewa Karbala ya Husein ibn Ali (a.s) kutoka kwa Husein ibn Ali (a.s) mwenyewe. Khatibu na Mhubiri wa Karbala hii ni Husein ibn Ali (a.s) mwenyewe. Khatibu wa Karbala hii alitoa hutuba na kuwajulisha watu kuhusu Karbala yake na kama wanataka kuelewa Karbala hii basi wanapaswa kuilewa kutoka kwa mwanawe Imamu Sajjad (a.s), kutoka kwa dada yake Mheshimika Zainab (a.s) kwa sababu wamewasilisha Karbala ya kweli ya Husein (a.s). Kiongozi wa Mashahidi anasema:

ألا ترون أنّ الحقّ لا يعمل به وأنّ الباطل لا يتناهى عنه

"Je, hamuoni kwamba haki haitekelezwi na upotovu haukatazwi?"

Je hamuoni kwamba wakandamizaji na watu waovu wameuchukua utawala kutoka kwa Waislamu? Imamu (a.s) alitambulisha maana ya Uyazid na kuondoa pazia kutoka kwenye uso wa Yazid na akasema kwamba Yazid ni dhalim, mkandamizaji na muuwaji. Yazid ni sawa na uliberali wa leo. Yazid ni mliberali wa kwanza miongoni mwa Waislamu na uliberali wa Kiislamu ni Uyazidi.

Suala ni kwamba fikra na kaulimbiu za Uyazid hulingana na itikadi za uliberali. Uyazid haukuwa bendera kwa ajili ya udikteta; udikteta na ufalme ni tofauti na Uyazid. Wakati uliberali ulipojitokeza ndipo Husein ibn Ali (a.s) alipoingia uwanjani kwa sababu uliberali si kwamba tu unatumikisha wanadamu bali pia huzivunja haki. Ufalme hutawala na kuwashinikiza Waislamu lakini uliberali hutoa kaulimbiu za msaada kwa ajili ya wanadamu na kuukandamiza ubinadamu kwa kutoa kaulimbiu za elimu ya ubinadamu. Uliberali ni msaada kwa ajili ya mtu lakini adui wa haki. Ni msaada wa Waislamu lakini adui wa Uislamu. Leo inasemwa kwamba wanadamu lazima wawe Waislamu lakini bila Uislamu, huu ni uliberali. Wakati dhulma na ukandamizaji ulipokuwa waziwazi Kiongozi wa Mashahidi alikataza kukaa kimya. Hakusema nalazimishwa kuondoka, bali alisema naondoka. Naanzisha uasi huu:

وإنّى لم أخرج أشراً ولا بطراً ولا مفسداً ولا ظالماً.....

"Siendi kama mkandamizaji; siendi kama dhalimu, siondoki kwenda kufanya vurugu na siondoki kwenda kusababisha dhiki; bali badaka yake naondoka sio ninalazimishwa kuondoka. Kama ningetaka kubakia ningeweza kubakia nikifanya ibada katika *Masjid Nabawi*. Kama ningetaka ningeweza kuchukua hifadhi katika Kaaba. Ningeweza pia kukaa kwa amani nyuma ya kuta za sala. Ningeweza vilevile kuchukua msaada wa ibada na kukaa kwa ukimya. Vilevile nilikuwa nafahamu njia nyingi za kuishi kwa amani."

Wakati watu wakubwa wa Makka na Madina walitoka kumzuia Imamu Husein (a.s) na wakamuomba asiondoke; watu maarufu wawili Abdullah ibn Zubair na Abdullah ibn Umar (mtoto wa Khaifa wa pili) walimuendea na wakajiingiza katika majadiliano. Mukhtasari na kiini cha majadiliano yalikuwa kwamba tutaingilia katika mapambano yako na Yazid na tutazungumza kuhusu majadiliano na maongezi ya pamoja. Kiongozi wa Mashahidi alisikiliza kila kitu na baada ya hili alisema: "Ole juu ya mambo haya mnayoyasema. Mnanionesha njia hii dhidi ya Yazid! Badala ya kuja kwangu na kuniuliza njia ya wokovu kwa vile mimi ni Imamu wenu, kinyume chake mnanifundisha ni kitu gani cha kufanya! Ole juu ya mazungumzo yenu haya."

Kuna mazungumzo fulani ambayo yanalaaniwa na Kiongozi wa Mashahidi; mazungumzo ambayo hayo hayana *Hamasa*, mazungumzo ya woga, yale ambayo hayana ushujaa ndani yake; anasema kwamba badala ya kunisadia, badala ya kunishawishi, badala ya kusimama nyuma ya mgongo wangu, badala ya ninyi kuwa mikono na mabega yangu, badala ya kuniamrisha, badala ya kushiriki katika jeshi langu pia mnanizuia kuchukua hatua za ujasiri. Inashangaza kwamba umma badala ya kumsaidia Imamu wao wanaanza kumzuia Imamu wao.

Ushia ni matokeo ya uvumilivu na uimara na unahakikishiwa kwamba Ushia umefikia hatua hii kwa sababu ya uvumilivu huu na mapambano (*Moqawamat*) na msimamo *Istiqamat*. Ushia ni dini ya mapambano, na wokovu wa Uislamu uko katika uimara na mapambano (*Moqawamat*). Ushia utakufa kama utaacha mapambano hayo. Mzigo wa paa upo juu ya nguzo na wakati nguzo zikiacha upinzani na ulinzi, paa huporomoka chini. Maana ya mapambano (*Moqawamat*) ni ulinzi. Mwili wako uko hai kwa ajili ya ulinzi, na kama ulinzi huu ukifa basi mwili nao vilevile utakufa. Pamoja na yote haya, viini vya maradhi na magonjwa yanayotushambulia kutoka kila upande na hata baada ya kula chakula kibaya kilichochafuliwa, kwa nini bado tunaishi? Hii ni kwa sababu tu ya mfumo pekee wa ulinzi ndani ya mwili. Maradhi hutokea tu wakati mfumo wa ulinzi wa mwili

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 58



unapokuwa dhaifu. Daktari hutoa dawa kusadia kadiri ya ulinzi katika mwili. Uko hai muda tu ulinzi upo katika mwili wako. Siku ambayo ulinzi utasimama utalala chali. Mwili wa mwanadamu ambao ulinzi wake husimama kaburi lake liko wazi. Hii pia ndio hali ya umma; umma ule ambao hauna mfumo wa ulinzi makaburi yao pia yako wazi.

Dini ambayo kwayo ulinzi umefikia mwisho, uwanja wa makaburi uko tayari kwa ajili yake, na mchimba kaburi amekaa akiwa amejitayarisha na muoshaji pia yuko tayari. Dini ambayo mfumo wake wa ulinzi umefikia mwisho ulimwengu uko tayari kuizika dini hiyo, jumuiya na umma. Uislamu ni matokeo ya Karbala leo, kwa sababu uko hai leo kwa ajili ya hatua ya ulinzi wa Kiongozi wa Mashahidi na mapambano ya maswahaba zake. Uislamu uko kwenye huruma ya Husein ibn Ali (a.s). kama unataka kuuliza kuhusu ujumbe wa Karbala katika sentensi moja, basi ujumbe wenyewe ni Ulinzi, Mapambano (*Moqawamat*) na msimamo.

Imamu Khomein (r.a) anasema kwamba Mapinduzi ya Uislamu ni matokeo ya Karbala, Azadari na Muharram. Sio kwamba tulipika vyungu vingi vya chakula na kula na hivyo kusababisha mapinduzi. Ni kitu gani kilichokuwa ndani ya Muharram na Safar ambacho kilisababisha mapinduzi? Kulikuwa na nini mikononi mwako ambacho kiliupindua ufalme wa ubeberu, ni kitu gani kilichokuwa pamoja na wewe ambacho mataifa makubwa yanaweza kuchapwa nacho usoni mwao? Hiki kilikuwa kitu kimoja tu:

“Chochote tulichokuwa nacho kilitokana na Kiongozi wa Mashahidi (a.s).”

“Chochote tulichokuwa nacho ni kwa sababu ya Muharram na Safar.”

Hii ina maana kwamba kutokana na Muharram na Safar tulijifunza Mapambano (*Moqawamat*), Msimamo (*Istiqamat*) na ulinzi. Ilikuwa ni kwa sababu ya Muharram na Safar kwamba:

قمنا وأقمنا واستقمنا

"Tulianzisha mageuzi, tuliwaamsha wengine na tukawa imara wakati wote."

Haya ni maneno ya siri ya Mapinduzi. Simama, amsha na kuwa imara. Ni kutoka wapi umejifundisha huu uasi, kuamsha na uimara? Imamu (r.a) alisema ni kutoka Karbala. Hivyi ndivyo *Hamasa* ilivyo, kusimama, kuamsha na kuwa imara sio kurudi nyuma; kwa muda gani? Mpaka muda vichwa vitakapokuwa juu ya mabega lazima uendelee na hakuna kurudi nyuma, na iwe ukatwe kichwa lakini kamwe usije ukainamisha kichwa chako, hili ni jina la Karbala. Hiki ndicho kinachomaanishwa na ulinzi ambacho humaanisha kwamba mbele ya Yazid endelea kuweka ulinzi mpaka muda kichwa chako kitakapokatwa. Hata baada ya kichwa kukatwa kamwe kichwa kisije kikainama. Isiwe kwamba umekatwa kichwa halafu familia inaanza kumsihi Yazid. Bali badala yake unakatwa kichwa na wale waliobakia nyuma lazima wawe wajumbe wa hawa waliokatwa shingo. Lazima wauamshe ulimwengu; lazima wauamshe ulimwengu kwa kwenda masokoni na mitaani. Wakati ulimwengu wote unapokuwa huko Kufa na Sham, lazima muende huko na mjulishe kwamba hakuna matatizo yenu yoyote yatakayosuluhishwa kwa kuwa watazamaji.

Kulikuwa na *Hamasa* moja ambayo ilitengenezwa na Husein ibn Ali (a.s) na kulikuwa Hamasa moja zaidi iliyotengenezwa na Bibi Zainab (a.s). Allah ni shahidi kwamba wakati mtu akiangalia kwenye Hamasa zote hizi inakuwa vigumu kupima ni Hamasa ipi ambayo ilikuwa bora. Kwa ukweli Hamasa zote hukamilishana kuelekea kwenye ukamilishaji. Kama *Hamasa* ya Bibi Zainab isingekuwepo, *Hamasa* ya Husein ingepotea. Hii *Hamasa* ya Bibi Zainab iliilinda *Hamasa* ya Husein. Watu walishuhudia uvumilivu na ulinzi wa Kiongozi wa Mashahidi; aliulinda Uislamu chini ya sime, aliulinda Uislamu wakati Shimr amekaa juu ya mgongo wake, akachukua watoto wake mpaka sehemu ya machinjioni kwa mikono yake kwa ajili ya kuulinda Uislamu. Je, ulinzi wa Uislamu ni mgumu sana au kwenda kati ya

wanaume (wa kando) bila ushungi na mikono ikiwa imefungwa nyuma ya mgongo na kutoa khutba; na kuwaambia kwamba mtu ambaye mnamuita muasi ni Imamu wa dini yenu. Hii ndiyo *Hamasa* ambayo iliulinda Uislamu, wale wanaojitenga kwenye utawa hawakuulinda Uislamu, udororaji na utuliaji haukuulinda Uislamu; Uislamu ulilindwa na uvumilivu wa Zainab na Hamasa ya Zainab (a.s).

"Bila ya Zainab Karbala ingelikufa. Bila ya Zainab Ushia ungetoweka."

Bila ya Zainab dini ingetoweka. Zainab ni wa aina gani ya haiba? Zainab ni jina la Mapambano (*Moqawamat*) na ulinzi. Zainab sio jina la bibi aliyechoka na mchovu. Alifungwa kwa kamba lakini hakuitumia hali hiyo kama kisingizio; ushungi wake ulichukuliwa lakini hakutangaza hali hii ya kutokuwa na ushungi kama kisingizio; vichwa sabini vilitungikwa kwenye mikuki mbele yake lakini hakulifanya hili kama kisingizio. Alitoa khutba ambayo ilitikisa baraza la Yazid na jibu la papo hapo lilikuwa kwamba mzee mmoja alisimama na akamuomba Yazid kumfidia kwa jinai hiyo. Daraja la ujasiri na ari katika khutba yake ilikuwa kwa kiasi kwamba watu walikumbuka khutba ya Bibi Zahra (a.s) kwa sababu mama yake pia alikuwa Bibi wa *Hamasa* na bint halikadhalika. Hapa tunajadili tu kuhusu *Hamasa*, lakini ilikuwa ni *Hamasa* ya Zainab ambayo ililinda *Hamasa* ya Husein.

Inashangaza kuona kwamba wale watu pamoja na ubora walio nao, waliitoa nafsi ya Hamasa nje ya Uislamu, waliondoa roho ya Hamasa kutoka Karbala na kutoka kwenye uasi mtakatifu wa Kiongozi wa Mashahidi. Karbala na Ashura ni Hamasa kutoka kwenye kichwa mpaka kwenye vidole vya miguu kama tu ulivyo Uislamu; Qur'ani inaanza kuonyesha Hamasa. Kwa ukweli kama nafsi ya Qur'ani ingelikuwa ndani ya Waislamu, wasingeliweza kukubaliana na fedheha. Yafuatayo ni maneno ya Bibi Zainabu: "Yazid, unafikiri kwamba kwa kutulazimisha na kutufunga kamba na kutufanya tusimame katika baraza na kwa kuwa kwako kiburi unajipa fikra kwamba umetufedhehesha na unajiona wewe mwenyewe

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 61



kwamba umekaa kwenye kiti cha utukufu?" Alimuambia Yazid: subiri, usifanye haraka, na usitembee kwa haraka sana (hivi punde utaona).

Jumuiya yenye mwenendo huu kamwe haiwezi kufedheheka; hata kama wamefungwa kamba, minyororo na kupatwa na maumivu makali hawakubali kudhalilishwa. Je, ni zipi kaulimbiu za Kiongozi wa Mashahidi (a.s) katika Karbala? Hazikuwa zile kaulimbiu ambazo kwa kawaida tunazisoma leo; zilikuwa kaulimbiu ambazo hata kama tukizifikiria tunaona ugumu na changamoto kutoa kaulimbiu kama hizo.

إنّى لا أرى الموت إلاّ سعادة والحياة مع الظالمين إلاّ برما

"Nayaona maisha chini ya wakandamizaji ni udhalili na nakiona kifo na kuuawa shahidi katika njia ya Allah ni fahari na upendeleo."

إنّ الداعى ابن الداعى قد ركزنى بين اثنتين بين السلّة

والذلّة، هيهات منّا الذلّة

"Mtoto huyu wa zinaa wa mzinifu amenifikisha njia panda ya utukufu na fedheha. Lakini hana habari kwamba Husein kamwe hatatembea kwenye njia ya fedheha. Nitatembea njia ya mapanga. Nitatembea kwenye njia ya mateso lakini kamwe sitavumilia fedheha."

هيهات منّا الذلّة

"Nasema fedheha hapana."

Husein na fedheha haviwezi kujikusanya sehemu moja. Na hata kama kuna watu wakubwa lakini ambao maneno yao yananuka fedheha, basi Husein ibn Ali (a.s) anasema: "Ole kwa mazungumzo kama hayo."

## Karbala ni Hamasa kiuhalisia

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 62



# SURA YA NNE

## Msimamo (*Istiqamat*)
## Somo kutoka Karbala

Kitu muhimu zaidi kinachohusiana na tukio la Karbala ambacho tunapaswa kutafakari, kuchambua na kujadili juu ya kila jambo ni madhumuni ya kuasi kwa Kiongozi wa Mashahidi (a.s). Nini yalikuwa madhumuni ya Imamu Husein (a.s) ya kuanzisha uasi huu na je, alikamilisha harakati hii takatifu? Iwapo uasi huu ulianzishwa na Imamu Husein (a.s) au alishawishiwa kwa ajili ya hili? Wakati mwingine kutokana na mijadala na maandishi ya vitabu tunapata mawazo kwamba Imamu Husein (a.s) alilazimika bila ya kupenda kujitumbukiza kwenye masaibu haya. Kama ambavyo kwa kawaida inasemwa kwamba kama amri ya kutakiwa ale kiapo cha utii isingetolewa, kama wasingemfanyia bughudha na wasigemtishia na chaguo la kutoa kichwa chake au kusalimu amri kwa Yazid, basi kadhia hii isingetokea. Aina hii ya sababu hutokezea kwa ajili ya matukio fulani au harakati katika zama zetu na wanadamu hupotoshwa na kutoka kwenye njia yake ya haki na kuelekea upande mwingine. Pia sasa hutokea kwamba tukio fulani hutokea na papo hapo matukio fulani mengine pia hutokea na tunayahusisha pamoja tukidai kwamba tukio hili ambalo limetokea ni matokeo au athari ya kadhia zingine na matukio.

Hakuna shaka kwamba kulikuwa na madai ya kiapo cha utii yaliyofanywa kutoka kwa Imamu Husein (a.s) lakini pia lazima tufahamu kwamba hata kama Yazid asingefanya madai haya bado uasi huu ungetokea. Hata kabla ya Imamu Husein (a.s) kupata fursa ya kuanzisha uasi huu kwa matayarisho kamili, Yazid alianzisha uasi huu. Yazid au washauri wake waliamua kufanya haraka juu ya suala hili ili kudhoofisha matayarisho yoyote yaliyopangwa na Imamu Husein (a.s) kuanza uasi dhidi ya Yazid. Hii ni kwa sababu kama tunachambua khutba za Imamu Husein (a.s) kuanzia

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 63



Madina mpaka Karbala na hata kabla ya Yazid kushika madaraka, tunaweza kuelewa kwa urahisi na jambo hili liko kwa uwazi linadhihirisha kwamba Imamu (a.s) alikuwa na nia hii ya kuasi na harakati tangu zamani. Lakini alikuwa akingojea fursa na wakati muafaka ambako angeweza kukamilisha makusudio yake katika njia ya hali ya juu iwezekanayo. Wakati wa kipindi hiki tukio hili la madai ya kiapo cha utii yalitokea na hiki hakikuwa kitu cha ajabu au kipya kwa Imamu (as) kwa vile alikuwa amejitayarisha tayari kwa ajili ya tukio hili. Imeandikwa na wanahistoria wengi kwamba wakati Walid alipomuita Imamu Husein (as) ofisini kwake mjini Madina, Imamu (as) aliposikia wito huu mara moja alisema kwamba *Amir-e-Sham* (Mua'wiya) amefariki na mwanawe ameteuliwa kuwa mrithi wake na ananitaka mimi nile kiapo cha utii kwake. Hii huonesha kwamba hata kabla ya mtu yeyote kumpa taarifa yeye mwenyewe Imamu (as) alihisi kwamba tukio hili limekwisha tokea na alielezwa kitu kama hicho hicho wakati alipokwenda kwa Walid na kumuuliza sababu ya kumuita. Alielezwa kwamba tukio hilo limetokea huko Damascus na amri imekuja kutaka kiapo chako cha utii. Imamu (as) alikuwa amekwisha jitayarisha na hilo na tangu zamani alikuwa anajaribu kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya watu kushiriki kwa urahisi katika maasi wakati utakapofika.

Uthibitisho wa habari hii unayohusu uasi huu vilevile hupatikana kwenye maandishi mengine ya kihistoria yaliyosimuliwa kwetu yajulikanayo kama Khutba ya Mina. Mwaka wa 59 A.H., mwaka mmoja kabla ya tukio la Karbala na hata kabla Yazid hajashika madaraka, Imamu (as) alitoa khutba hii yenye maelezo marefu katika uwanda wa Mina wakati wa msimu wa Hijja. Imamu Husein (as) aliwakaribisha watu wote mashuhuri wa ulimwengu wa Kiislamu wa wakati huo, wanachuoni na wakuu wa makabila ili kuwahutubia kwa khutba hii. Imamu (as) alivuta nadhari zao kwenye vitu vingi na mwishowe alieleza nia yake ya uasi. Hata kama Imamu (as) asingewalingania kwa uwazi nia yake hiyo ya uasi, bali pia kutokana na maandalizi aliyokwishaandaa na kutokana na khutba yenyewe ni dhahiri ni nini makusudio na matilaba ya Imamu Husein (as) na sababu ya kwa nini aliwaita watu hawa.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 64



Katika khutba hiyo Imamu (as) aliwaeleza ni kwa nini Allah Aza wa Jallah aliwalaani wanachuoni wa Kiyahudi wa Bani Israil. Sababu aliyowaambia ni kwamba hawakutekeleza *Amr Bil Maruf* na *Nahi Anal Munkar*. Walikuwa hawazuii watu kujiingiza katika maovu, walikuwa hawalinganii watu katika maadili ya kimungu, na walizoea kukaa kizembe kama watazamaji, na walikuwa wakilipwa na serikali na mahakama. Kwa hiyo, ama kwa sababu ya uroho au hofu walizoea kujizuia kuonesha haki na ukweli. Hii ndio sababu ya Allah Aza wa Jallah ya kuwalaani kwa maneno makali katika Qur'ani Tukufu. Baada ya kusema haya Imamu (as) aliwageukia wasikilizaji wake na akasema kwamba wakati tamaduni na mila za wahenga wenu wa zamani zinapovunjwa mnafanya makelele mengi, lakini wakati mipaka ya Mungu inapokanyagwa hamuoneshi upinzani wowote kwa hili. Baada ya kauli hii Imamu (as) alisema: "Ewe Mola wangu! Shuhudia kwamba sifanyi uasi kwa ajili ya ulimwengu, madaraka, fahari au hadhi, bali badala yake ninafanya uasi kwa ajili ya kuitetea *tawhid*." Yote haya yalisemwa katika khutba ambayo ilitolewa mwaka mmoja kabla ya tukio la Karbala.

Baada ya tukio hili kuna ushahidi mwingine uliopo katika mtindo wa barua iliyoandikwa na Imamu (as) kwenda kwa Mu'awiya. Kwa kweli hili lilikuwa ni jibu la barua iliyoandikwa na Mu'awiya kwenda kwa Imamu (as) ambayo kwayo alijaribu kumtisha Imamu (as). Katika barua hii Mu'awiya kwanza alitaja matatizo ya kimaadili ambayo yangejitokeza kama Imamu (as) atazungumza dhidi yake, kwamba itasababisha mtafaruku na mtengano ndani ya umma wa Kiislamu. Alimshauri Imamu (as) katika barua hiyo kwamba lazima tufanye kila kitu kwa ajili ya umoja wa Waislamu na tusilete vurugu na tuache umma wa Kiislamu uishi kwa amani. Baada ya kuandika kuhusu haya, kisha katika barua yake alianza kumtisha Imamu (as) kwamba kama ukianzisha uasi basi utakabiliana na matokeo mabaya sana, na wewe (Imamu) na umma mtapata hasara kubwa. Alihitimisha barua yake hiyo kwa mukhtasari kwamba haifai kwa Imamu kufikiria kitu kama hicho. Imamu (as) aliijibu barua yake hiyo neno kwa neno, kama vile juu ya suala la umoja, Imamu (as) alisema wewe ndiye

uliyekuwa wa kwanza kuugawa umma, ama kuhusu hasara, Imamu (as) alisema kwamba wewe ndiye uliyekuwa wa kwanza kuusababishia umma huu hasara. Imamu (as) alijibu kila nukta iliyotajwa na Mu'awiya katika barua yake. Hii ina maana kwamba hata Mu'awiya alikuwa anafahamu kwamba Imamu (as) anazo fikra zinazohusiana na uasi, na hii ilikuwa kweli kwani alikuwa na wapelelezi waliokuwa wakitoa taarifa ya kila kitu kinachohusiana na Imamu (as). Walichunguza kwa karibu sana kila mkutano, mkusanyiko, khutba, kauli, shughuli na matayarisho ambayo Imamu (as) alikuwa akiyafanya kwa ajili ya uasi huu.

Kitu muhimu ambacho Imamu (as) alifanya ilikuwa ni kuwaandaa watu binafsi kwa ajili ya uasi huu. Hili lilikuwa muhimu kwa sababu muda ambao umepita tangu kuuawa shahidi kwa Amirul Muminin (as) mpaka tukio la Karbala umekuwa wakati mgumu sana kwa umma wa Kiislamu. Kwa sababu baada ya kifo kitakatifu cha Imamu Ali (as), Bani Umayya walipata udhibiti wa ukhalifa na serikali kutoka Damascus. Zama hizo zilikuwa sawa sawa na zama za leo ambazo tunaishi. Ilikuwa ni katika kipindi hiki ambacho kwacho kwa msaada wa udanganyifu, hila na ugaidi watu watendaji waliolengwa waliuawa kishahidi. Na kwa upande mwingine watu mashuhuri waliuawa ima wakiwa safarini, katika biashara zao au katika nyumba zao na kwa upande mwingine wengi walidanganywa na tamaa za ulafi. Wakati wa kipindi hiki tukio la mkataba wa amani wa Imamu Hasan (as) ulifanyika ambao kwawo sababu kubwa ilikuwa ni tamaa hii na ulafi ambao kwawo masahaba wengi wa Imamu Hasan (as) walishawishika. Baadhi walishawishiwa na vyeo, baadhi kwa mali na baadhi wakashawishika kwa wanawake. Kwa bahati mbaya haya yalitokea na watu mashuhuri katika kambi ya Imamu Hasan (as) walidanganyika kwa silaha hizi tatu.

Kuna kitabu kilichoandikwa na Marehemu Tabrisi kwa jina la "*Al-Ihtijaj*" ambacho ni mkusanyiko wa aina mbali mbali na mifano ya kisiasa na upinzani wa kielimu na upinzani ambao Maimamu wetu wameupitia. Kitabu hiki lazima kisomwe, lakini sio kwa nia ya kupata thawabu bali kwa kweli

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 66



matukio na harakati za Maimamu (as) lazima yachambuliwe kulingana na mambo na hali za sasa za zama zetu. Katika kitabu hiki imeandikwa kwamba baada ya mkataba wa Imamu Hasan (as) ulipofanyika baadhi ya wafuasi wa Imamu Hasan (as) walijitokeza na kubishana naye katika namna ambayo ni ya matusi na isiyo ya kimaadili, huku wakimuuliza Imamu (as) kuhusu kuukubali mkataba huu, Imamu (as) alijibu kitofauti katika mazingira tofauti, kwa kiwango cha ulewa wa muulizaji. Alitoa sababu moja kwa mtu fulani na nyingine kwa mtu fulani mwingine, lakini sababu zilizotolewa na yeye zilikuwa ni sehemu ya sababu za kukubali mkataba huu. Moja ya sababu ngumu na chungu alizozitaja kwa maneno yake mwenyewe ilikuwa: “Wamenunua baadhi ya watu wa jeshi langu na mpango wao ni kuwatumia watu hawa walionunuliwa kunifanya mfungwa, wanifunge mnyororo na kunikabidhi kwa maadui.” Kwa maneno mengine waliambiwa kwamba kama wakilifanya hili watalipwa vizuri sana na wameona kwamba kabla ya hili masahaba wengi sana wamemuacha Imamu (as) kwa ajili ya malipo mazuri kutoka kwa maadui. Hata kamanda mkuu wa jeshi la Imamu (as) alishanunuliwa kabla. Kamanda huyu ambaye watoto wake waliuawa kabla ya hapo na adui huyo huyo, familia yake ikaporwa na kukandamizwa alikuwa anatokana na Bani Hashim na ndugu wa karibu wa Imamu Hasan (as). Ubdullah ibn Abbas, ambaye jina lake ni maarufu sana katika Uislamu. Alikuwa kamanda mkuu wa jeshi la Imamu Hasan (as) na alikuwa miongoni mwa wa mwanzo kabisa kununuliwa na jeshi la Damascus. Alihongwa maelfu ya dinar za dhahabu na dirham. Alipewa nusu na akaahidiwa kupewa nusu nyingine wakati atakapojiunga na jeshi la Mu’awiya. Alipewa cheo kilekile alichokuwa nacho katika jeshi la Imamu (as) na walimpa msichana mrembo wa Damascus (kwa vile watu wa sehemu hiyo ya Syria na Lebanon walikuwa watanashati na warembo), yote haya kama atamsaliti Imamu Hasan (as) na kuja upande wa jeshi la Mu’awiya. Alimuacha Imamu (as) na kuondoka pamoja na kundi lote na kujiunga na jeshi la Mu’awiya. Ingawa nyingi ya ahadi baadae hazikutekelezwa lakini kama hivi wengine wengi walidanganyika kwa zawadi na wakamuacha Imamu (as).

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 67



Baadae muda ukaja wakati maadui wakawa washari mno na wakaanza kugawa pesa kwa kila mtu katika kambi ya Imamu Hasan (as), wakatoa ahadi nyingi, vitisho, kusambaza umbea na wakatengeneza misukosuko katika kambi ya Imamu Hasan (as). Hali hiyo ilikuwa kiasi kwamba wanajeshi wengi wa Imamu (as) walitaka kuchukua faida nyingi iwezekanavyo kutoka kwa maadui na kuwa karibu nao. Kadhia hii ya bahati mbaya ilitokea na katika kitabu hiki "*Al-Ihtijaj*" Imamu (as) baadae alisema kauli ambayo imeandikwa katika kitabu hiki tangu karne nyingi lakini hakuna aliyeielezea. Ni kauli chungu sana na fasaha ambayo hutia uchungu kwa mwanadamu na moyo wake kuvuja damu baada ya kuisikiliza. Katika kitabu hiki imeandikwa kwamba wakati watu walipokuja na kumuuliza kuhusu sababu za kufikia mkataba na Mu'awiya, Imamu (as) kwanza alifafanua kuhusu mipango yao ilivyokuwa na jinsi nia yao ilivyokuwa kuhusiana na yeye (as), na kisha kwa uwazi kabisa akitumia neno Shi'a kwa ajili ya wafuasi wake, alisema: "Natoa upendeleo kwa Mu'awiya dhidi ya Mashi'a wangu hawa." Hii ni kwa sababu Mu'awiya ni adui yangu na ninamfahamu vya kutosha kwa kile anachokusudia kunifanyia, ambapo kwa masahaba wangu wamepanga kuniuza kwenye mikono ya Mu'awiya." Haya ni maneno ya Imamu (as). Alielekeza kidole kwenye jeshi lake na masahaba zake na akasema kwamba wenyewe wanajiita Mashi'a wangu lakini fikra zao mbovu zimebuni mpango wa kuniuza kwa Mu'awiya.

Kadhia ya Karbala ilikuwa bado haijatokea lakini misingi yake ilikuwa imeanza kuwekwa, na tukio hili la mkataba wa amani linatokea. Watu wanasema Mu'awiya alimlazimisha Imamu Hasan (as) kwenye mkataba huu, lakini ukweli ni kwamba wafuasi wake mwenyewe ndio waliomlazimisha Imamu (as) kusaini mkataba huu wa muafaka na Mu'awiya. Hii ndio sababu Kiongozi wa Mashahidi (as) alisema kwamba aina ya masahaba niliopata sio wale waliokuwa wa babu yangu (s.a.w.w.) wala baba yangu (as) au wa kaka yangu Hasan (as). Hao walikuwa ni wasaliti wakubwa na wabaya, kwa sababu yao mkataba huu ulifanyika na baadae wakaja kwa Imamu (as) katika hali ya matusi, utovu wa maadili na ya aibu wakimtaka atoe ufafanuzi na kumtangaza Imamu (as) kuwa ndiye mwenye

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 68



kuhusika na mkataba huu. Mpaka hata mtu mmoja alimkaripia na kumuonya, na matokeo yake kusababisha kipigo cha mwili. Kuna majina makubwa miongoni mwao, kwa sababu majina ya watu wakubwa yanapojikeza watu hunyamaza kimya. Hili pia liko kwa ndugu zetu katika imani wakati majina ya watu wakubwa yanapojitokeza katika hali ya kinyume hupenda kunyamaza kimya na huwa hawataki kuzungumza kupita mipaka hii. Lakini huu ni ukweli kwamba mtu mmoja mashuhuri wa Kufa, Salman ibn Surade Khazai ambaye alikuwa mtu wa ajabu mwenye tabia za kigeugeu, ambaye alizoea kuandaa mikutano nyumbani kwake ili kumkaribisha Imamu Husein (as) kuja Kufa na yeye mwenyewe alituma barua kwenda kwa Imamu (as), lakini baadae muda ulipokuja hakuonekana mahali popote. Mtu huyu alimfuata Imamu Hasan (as) na akamsalimia kwa maneno makali: “Salamu kwako wewe uliyewadhalalisha Waislamu (*Asalaamu alaika Ya mudhalal Muslimin*). Na mtu huyu anaangaliwa kwa heshima kubwa mpaka leo na kuhesabiwa miongoni mwa watu wanaoheshimiwa.

Hali yote hii ilitokea mbele za Imamu Husein (as) na haiwezekani kwamba baada ya kifo cha kishahidi cha Imamu Hasan Al-Mujtaba (as), Imamu Husein (as) angetoka nje ya mawazo haya hata kwa siku moja. Hivyo tunaweza kutambua hali zilizokuwa wakati wa Imamu Hasan (as). Shahid Baqir Sadr (ra) anasema kuhusu zama za Imamu Hasan (as) kwamba jumuiya maana yake masahaba wanajeshi wa Imamu (as) walikuwa ni wahenga wa migogoro mingi, migogoro aina mbali mbali ilikuwepo miongoni mwao, na jumuiya hii ambayo ilikuwa muhanga wa migogoro haina thamani na ilifanya hivyo hivyo. Walikuwa katika hali ya kutokuwa na uaminifu na kiusaliti. Migogoro ilivunja makusudio ya jumuiya, ilivunja ari yao na kuvunja migongo yao. Migogoro ilivunja imani ya jumuiya iliingilia makusudio yao na kuwafanya wazembe na wachovu. Hivi ni vidokezo vya kupendeza ambavyo Shahid Sadr amevitoa kuhusiana na hali ya kisaikolojia na ya kijamii ya jumuiya hii.

Imamu Husein (as) alikuwa anatambua kwamba mgogoro huu umeukumba jumuiya hususan wafuasi wake mwenyewe walikuwa muhanga wa mgogoro huu, na jumuiya iliyokumbwa na migogoro haiwezi kuanzisha uasi kwa urahisi na kwa wepesi. Kwa hiyo Imamu Husein (as) alilazimika kufanya juhudi za muda mrefu, lakini bado tunaona kwamba wakati alipotangaza matayarisho makubwa ya mipango yake ya kuanzisha uasi watu wachache sana walijitokeza kumsaidia. Kusema kweli baadhi yao walirudi nyuma katikati ya njia na imesemekana kwamba hata katika dakika za mwisho baadhi yao walimuacha Imamu (as). Kwa mfano wakati kila mtu alipouawa Shahid na Imamu (as) peke yake tu ndiye aliyebakia, bado walikuwepo baadhi ya watu wa aina hii, na hili hapa ni tukio la kushangaza lililopatikana la mfanyabiashara msafirishaji wa ngamia ambaye kutoka kwake Imamu (as) alikodisha baadhi ya ngamia kutoka Makka na ilikuwa abaki naye mpaka mwisho wa safari. Mtu huyu alikuwepo mpaka jioni ya siku ya Ashura. Wakati mtu huyu alipoona kwamba sasa kila mtu ameuawa kishahidi na muda wa kuuawa kishahidi kwa Imamu Husein pia unakaribia, alimfuata Imamu (as) na kumuambia kwamba kuwepo kwangu mimi na wewe sasa hakuna maana na muda mfupi ujao na wewe pia utauawa kishahidi, hivyo ingekuwa ni vyema ukanilipa. Alimtaka Imamu (as) amlipe kabla hajauawa kishahidi ili arudi alikotoka. Imamu Husein (as) alimlipa pesa zake na akamruhusu aondoke. Alichukua pesa zile na akaelekea kwenye kijimsitu cha mitende ambako amewafunga ngamia wake ili akimbie zake. Wakati alipofika pale baadhi ya wavamizi au watu kutoka katika jeshi la Umar ibn Saad walimnyang'anya pesa zile pamoja na ngamia wake na kumuuwa pale pale Karbala. Huu ndio ubaya wa mwanadamu wakati ambapo hakutoa msaada kwa Imamu (as) hakupata shahada pamoja na Imamu (as), lakini bado kauliwa pale pale Karbala. Alimuacha Imamu kwa ajili ya pesa, kwa ajili ya kuipenda dunia hii, kwa ajili ya ngamia wake lakini bado aliuawa kwa mikono ya wavamizi. Kuna matukio mengi kama haya yaliyotokea pale Karbala na yanastahiki umuhimu wa aina yake, lakini kwa bahati mbaya hakuna hata moja lililochambuliwa, kujadiliwa na kusimuliwa. Matukio haya yana masomo na mafundisho mengi.

Hivyo migogoro huharibu jumuiya, na wakati wa zama hii tangu kuuawa kishahidi kwa Amiru'l-Muminin (as) mpaka tukio la Karbala umma wa Waislamu umeathiriwa na migogoro mikali ambayo imekuwa ni sababu ya kuvunjika kwao na kudhalilika. Ilikuwa ni muhimu kabisa kusimulia kuhusu matukio haya ya kihistoria ili tuweze kuyalinganisha na hali iliyoko sasa ya zama yetu hizi. Kama unataka kufahamu yaliyojiri katika kipindi kile cha miaka kumi ya Uimamu wa Imamu Husein (as), basi hali ya miaka ile ni sawa na kile kinachotokea leo katika nchi hii (**ya Pakistan**) na vilevile katika ulimwengu wote wa Kiislamu. Ingawa ulimwengu wote wa Kiislamu hauko sawa. Kuna hali tofauti katika sehemu tofauti, hali iliyoko Iraq ni tofauti kabisa na hali iliyoko Iran, halikadhalika katika nchi ya Lebanon hali ni tofauti na sehemu nyingine za ulimwengu wa Kiislamu. Hatuwezi kusema kwamba hali ya aina moja ipo katika sehemu zote za ulimwengu wa Kiislamu, kila nchi ina hali zake mahususi, lakini inapokuja kwa Pakistan hali ni ya tofauti ya kipekee. Hali katika Pakistan haifanani na umma mwingine wowote wa Waislamu, kama kuna ukaribu katika mazingira, basi itakuwa ni pamoja na Iraq. Lakini bado hali katika Pakistan ni tofauti sana hata na Iraq. Kama tukiiweka hali iliyopo sasa ya Pakistan chini ya kioo cha historia, basi hali iliyopo sasa ya Pakistan ni sawa sawa na ile miaka kati ya kifo cha kishahidi cha Amiru'l-Muminin (as) na tukio la Karbala. Zama zile zilikuwa za migogoro ambayo ilichukuwa kila kitu kutoka kwenye umma. Zilichukua heshima na ghera yao; iliwaondolea mbali utambuzi wa kuelekea kwenye kuwepo kwao na kuwaondolea mbali kila kitu.

Ama kwa kifo cha kishahidi cha Sadr migogoro hii imepasua vipande vipande makusudio ya umma na kuvunja mgongo wake. Imeondoa ari, ushujaa, ujasiri na hata uwezo wao wa kufikiri. Wakati mwingine jumuiya imekuwa mateka kwa kiasi kwamba imesahau kuhusu jukumu la kuanza uasi, hata pia kupoteza ari ya kufikiri kuhusu kuanzishwa kwa uasi. Pia huogopa hata kuhofia kufikiria kuhusu kufanya uasi hata katika faragha. Hali hizi zilitengenezwa na maadui kupitia udanganyifu, ulaghai na ugaidi. Waliwauwa kishahidi watu mashuhuri na kuzitesa familia zao.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 71



Walikuwepo wengi ambao walilazimika kukabiliana na misukosuko mikali ya kifedha, mafao yao kutoka kwenye hazina ya serikali yalisimamishwa, na wengi waliishia kuishi chini ya umasikini. Wengi walikuwa wanakaribia kifo kwa sababu ya umasikini na kwa kweli wengi walikufa kwa ajili ya umasikini. Hizo ndio zilizokuwa hali ambazo walizitengeneza, na hizi ndizo hali ambazo kwazo wataalamu fulani walikuja nazo na kuvunja ari ya jumuiya. Kuna wataalamu mafundi ambao kazi yao ni kukandamiza ari ya jumuiya na kitu kama hicho kinatokea leo katika nchi hii (ya Pakistan).

Kwa upande mmoja kuna mgogoro wa kisiasa ambao umefikia kilele chake katika nchi hii. Ingawa ungeuita kwa jina lingine, itakuwa ni sahihi zaidi kuutaja kama mchezo wa kisiasa unaochezwa na wanasiasa. Kwa upande mmoja mchezo huu ni wa kisiasa na kwa upande mwingine migogoro mingine yote imekusudiwa kuvunja mgongo wa umma na kuzivunja nia zake. Mapambano ya kisaikolojia yanapiganwa wakati hali nyingine ziko kwenye udhibiti, lakini hapa Pakistan hali ni zaidi ya vita ya kisaikolojia. Kama ilivyo leo unaweza ukaona vita vya kisaikolojia kati ya Magharibi na Iran. Vita vya kisaikolojia ni vita vya kuumbuana kama ilivyo kati ya Magharibi na Iran ambako wote wanajaribu kushambulia neva za kila mmoja, ambayo ni zaidi kutoka Magharibi na kidogo kutoka Iran, na katika aina hii ya vita yule ambaye ana neva imara atafanikiwa. Mtu ambaye hapotezi udhibiti wa neva zake, hawi na mhemuko na mapigano ya kihisia katika hali ya busara. Hali hii ya vita vya kisaikolojia ni ngumu kuliko vita vya silaha, lakini vita vya migogoro ni vigumu zaidi kuliko hivi vita vya neva.

Kama tukishuhudia vita vya silaha, kunakuwa na upigaji wa mabomu mazito, maadui huja na silaha na kuchana chana vijana wa umma. Lakini bado mateso hayo ni mepesi kwa umma kuyavumilia, na sio wepesi tu kwa kweli mateso haya, vifo vya kishahidi hunyanyua ari ya jumuiya, huwahuisha na kuwarudishia ari yao. Ilitokea huko nyuma wakati ambako jumuiya zimeshambuliwa kwa ukatili na wakapatwa na vifo vingi vya kishahidi na matokeo yake wakapatwa na hisia ya heshima, kujiheshimu na

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 72



hadhi, na hapo wakafikia hatua ya kuheshimika; kama tulivyoona katika mashambulizi ya hivi karibuni huko Gaza. Lakini zile jumuiya ambazo zinajiingiza katika migogoro ambayo inavunja migongo yao, kuvunja ari yao na hata kugandisha uwezo wao wa kufikiri katika mwelekeo sahihi; jumuiya kama hizo kamwe haziendelei na kamwe hazinyooshi migongo yao.

Tunaweza kusoma *Nahjul-Balaghah* khutba za Amiru'l-Muminin (as) ili kukadiria juhudi zake alizofanya kuurudusha umma kwenye *Muqawamat* (mapambano); ili kuleta tena uvumilivu kwao na kwa mara nyingine kuwarudisha tena kwenye viwango vilevile kama umma ulivyokuwa wakati wa kipindi cha Mtume (s.a.w.w.). Mwishowe Amiru'l-Muminin (as) alisema kwamba licha ya juhudi zangu zote sikuweza kupata matunda mazuri yoyote kutoka kwenye umma huu. Amiru'l-Mumini (as) aliomba kwa Allah Aza wa Jallah kwamba: "Ewe Mola wangu! Waondolee mbali kutoka kwangu na niondolee mbali kutoka kwao." Imamu, Kiongozi na mlinzi kama Amiru'l-Mumini (as) hakuweza kupata matokeo ya mafanikio ya kuunyosha na kuurudisha umma kwenye miguu yake kwa sababu huu ni umma ulioshindwa, umma ambao mgongo wake umevunjika, umma ambao umepoteza moyo wake na umma ambao umepoteza ushujaa na ari yake yote. Na kisha mwishowe yeye (as) alilazimika kuomba kwa Allah Aza wa Jallah kuuondoa umma huu mbali na yeye na kumuondoa yeye mbali na wao na akasema: "Siwezi kubadilisha hali ya migogoro iliyoikumba jumuiya hii." Migogoro hiyo hiyo ilihamia kwenye zama za Imamu Husein (as) wakati wa Uimamu wake. Wakati mwingine watu wanauliza kwa nini Husein (as) hakuanza uasi mapema au kwa nini ausi huu usitokee wakati wa kipindi cha baba yake. Imamu Husein (as) alijaribu sana kuitoa jumuiya hii katika migogoro lakini wote wamekuwa wasio na akili na wazembe na hii inaweza kuonesha kwa urahisi kutoka kwenye khutba ya Mina na vilevile kutoka kwenye khutba mbali mbali nyingine na simulizi za Imamu (as) wakati wa safari yake kutoka Madina kwenda Karbala. Kama alivyosema Imamu Husein (as):

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 73



**ألا ترون أنّ الحقّ لا يعمل به وأنّ الباطل لا يتناهى عنه ليرغب المؤمن فى لقاء ربّه حقاً حقاً**

"Je, hamuoni kwamba haki haitekelezwi, je, hamuoni kwamba batili haizuiwi."

(*Mausuwata Kalemate Imam Husein* (as) uk. 356)

Anawahutubia watu wa kawaida na kuwaambia kwamba hamuoni kwamba ufisadi unafanywa kwa wazi. Aina hii ya sentesi hutumiwa wakati wa ufisadi unapokuwa wazi. Kabisa na bila kizuizi, na watu huulizwa iwapo ni vipofu, hawawezi kuona kile ambacho kinatokea kwao. Na huu ulikuwa ni ukweli kwamba umma haukuweza kuona kinachotokea. Wamefumba macho yao na walikuwa wanahusika tu na kazi zao ndogo ndogo za kila siku. Kila mtu yuko katika kujichukulia mwenyewe binafsi na kama siku moja ikipita kwa amani wakati wakiwa wanaweza kupata chakula walikuwa wakionesha shukurani kwamba siku hiyo ilikuwa nzuri kwa vile wamepata chakula na hakuna baya lolote lililotokea. Hali kama hiyo inaonekena leo halikadhalika kama mfano wa jioni ya siku ya Ashura, jumuiya yetu yote ilionesha shukurani kwamba Alihamdulillahi, hakuna kilichotokea leo. Hii maana yake ni kwamba wale ambao wameamua akilini mwao kwamba mambo mengi mabaya yatawatokea, basi kwa wao kama siku moja itapita kwa amani huonesha shukurani kwa Allah. Hii vilevile ilikuwa ndio hali katika wakati huo, kwamba kama hakuna kilichotokea siku hiyo, ambapo heshima ya wanawake wao haikuumizwa au kushambuliwa basi huonesha shukurani kwamba siku hiyo imepita vizuri.

Imamu Husein (as) alijaribu sana kuwatoa katika hali hii, kwa kweli kama sio kufanyika kwa madai ya kiapo cha utii, Imamu Husein (as) angeweza kutumia muda zaidi kutayarisha mazingira mazuri kwa ajili ya safari hii, na akiwa safarini Imamu (as) alikusanya kiasi maalumu cha masahaba 72 au 100 au zaidi, ambao Imamu aliwaamini vya kutosha kwa sababu wanatokea kwenye migogoro. Hii ina maana kwamba hata kama watu hawa wengi hawakuguswa na migogoro na kutokea humo, wanaweza kubadil-

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 74



isha mengi na kubadilisha historia. Wanaweza kuwa kigezo kwa vizazi vijavyo, jumuiya zijazo na walio bora katika kuondosha migogoro iliyoikumba jumuiya kutokana na migogogro hiyo. Hii ndio sababu Imamu (as) alipendezewa sana na masahaba hao na Imamu maasum (as) ametangaza kwamba wakati tunapomtolea salamu Imamu Husein (as), kwanza tuwakumbuke masahaba hawa, na Maimamu wote maasumu (as) walikuwa wakifanya hivyohivyo.

Masahaba hawa wameheshimika sana na ni wenye hadhi ya juu sana, lakini sio tu kwa sababu walitoa maisha yao. Kama maisha ni sababu kwa ajili ya utukufu na hadhi yao, basi masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pia walitoa maisha yao; kama vile Hamza (as) alitoa maisha yake katika njia ya kishujaa sana, kisha kuna mashahidi wa Badr, Uhud, Khandaki na katika vita vingine ambapo wote wanaheshimika sana na ni watu wakubwa. Mashahidi hawa pia wana thamani kubwa na lazima tuwatambue na kuwa na habari nao vilevile, kwa vile nao pia wana utukufu huo na hadhi kubwa. Mashahidi hawa wana hadhi kubwa sana kwa sababu wakati Uislamu ulipowahitaji walijitokeza na kutoa muhanga maisha yao na kuacha nyuma yao kila kitu. Hata wale waliofuatana na Amiru'l-Muminin (as) katika vita mbali mbali vya Siffin na Nahrwan wakauawa kishahidi hawa pia walikuwa watu wakubwa, lakini bado wote hawa hawalingani kwa hadhi ya mashahidi wa Karbala.

Ni sababu ipi ya ukubwa wao huo wa kipekee? Sababu yenyewe ni kwamba wale ambao walikuwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hawakuingia kwenye uwanja wa mapambano baada ya kutokea kwenye migogoro, bali badala yake walikuwa sehemu ya waliotayarishwa kuamshwa na jumuiya makini. Mtu ambaye hutokea kwenye jumuiya iliyoamka ni mtu mkubwa, lakini hadhi yake haiko sawa na yule ambaye anatokea kwenye jumuiya ambayo imekumbwa na migogoro na kuwa sawa kihadhi na mtu ambaye anatokana na jumuiya iliyoamka na iliyotayarishwa. Kama vya kutolewa vya wote hawa vinapimwa kwa pamoja, kutakuwa na tafauti nyingi. Chukua mfano wa pigo la Amiru'l-Muminin (s) katika vita vya Khandaki

na katika vita vya Khaybar vyote ilikuwa ni pigo kutokana na upanga uleule lakini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipendezewa zaidi na pigo la upanga katika vita vya Khandaki na akasema:

ضربة علي يوم الخندق افضل من عبادة الثقلين

"Pigo la Ali katika (vita vya) Khandaki ni bora zaidi kuliko ibada za vizito viwili (*Thaqalain*)."

Hii ni kwa sababu katika vita vya Khaybar hali ya migogoro haikuwepo, wakati ambapo katika vita vya Khandaki ilikuwepo. Katika vita vya Khaybar Waislamu walikuwa katika nafasi ya kujitawala kwa vile waliwashambulia Wayahudi, lakini katika vita vya Khandaki makafiri ndio waliowashambulia Waislamu na mji wa Madina ulikuwa katika hali ya mgogoro, kila kitu kilikuwa katika hali ya hatari na kila mtu alikuwa katika shinikizo kubwa na kulikuwa na hali ya hofu. Mungu aepushilie mbali, kama Waislamu wangeshindwa katika vita vya Khaybar, Uislamu usingetoweka au kusambaratika. Waislamu walikuwa imara sana kwa vile walitembea kutoka Madina kwenda kuiteka ngome ya Khaybar. Hata kama wasingefanikiwa katika kuiteka ngome ya Khaybar bado wangerudi Madina na Madina ilikuwa salama na chini ya udhibiti. Lakini kama wangeshindwa katika vita vya Khandaki kila kitu kingepotea. Si Madina, Uislamu wala Qur'ani ingelibakia. Hii ina maana kwamba Waislamu katika vita vya Khandaki walikuwa wameathiriwa na migogoro. Ilikuwa ni pigo la Amiru'l-Muminin (as) ambalo liliwapa ahueni kutokana na mgogoro huu na migongo yao ikanyooka tena. Hii ndio sababu ambayo kwamba kauli iliyotolewa na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) haikuwa kwamba Mujahid mmoja amekwenda kwa ajili ya makafiri bali badala yake alisema: "Imani yote inatoka dhidi ya ukafiri wote."

Aina ya migogoro iliyokuwepo katika vita vya Khandaki haikuwepo katika vita vingine na sio hata katika vita vya Badr. Watu waliokufa kishahidi wakiwa pamoja na Mtume (s.a.w.w.) na wale waliokufa kishahidi wakiwa

pamoja na Amiru'l-Muminin (as) katika vita na wao vilevile ni watu wakubwa na wanayo hadhi kubwa na ya hali ya juu. Hata baadhi yao walikufa kishahidi katika hali ya ukatili sana, kama Misam-e-Tamar (ra) aliuawa shahidi katika hali ya ukatili sana ambao haukukisiwa na mtu yeyote yule, lakini bado hadhi ya mashahidi wa Karbala ikilinganishwa na mashahidi wengine ni ya juu sana. Kwa kweli wakati wowote tunapoomba kwa ajili ya mashahidi siku zote tunasema kwamba Allah awaweke mashahidi wote wa Uislamu pamoja na mashahidi wa Karbala. Hii ni kwa sababu ya hali na mazingira ya zama zile ambayo kwayo walijitolea na kuingia katika uwanja wa mapambano.

Wale ambao walikuwa na Imamu Husein (as) walitokana na jumuiya hiyo hiyo moja; ilikuwa ni muda tu wa miaka kumi tangu kuuawa shahidi kwa Amiru'l-Muminin (as). Walikuwa chini ya aina zote za mashinikizo na migogoro kutoka Damascus, walikuwa waathirika wa aina mbali mbali za hofu kubwa na uvamizi kama vile uvamizi katika mali zao. Mu'awiya alikuwa akiwatuma watu wake kwa makabila na kuwapa pesa ili kuisaidia na kuiunga mkono serikali ya Damascus kama ikiwezekana na kama haiwezekani kuisaidia Damascus basi pia wanaweza kuchukua pesa hizo lakini kwa masharti kwamba wanyamaze kimya na wasisaidie kundi lolote (la Kufa au Damascus). Huu ulikuwa mgogoro ambamo pesa zilikuwa zikitolewa kwa kukaa kimya na bila ya kumsaidia Ali (as) wala kumsaidia Mu'awiya. Kwa kutoa pesa ili kukaa kizembe zembe katika hali ya kutohusika na lolote lile, kwa kuwatisha watu wengi na kuwarubuni wengine, waliufanya umma wote kuathirika na migogoro mikubwa mno. Jumuiya hii haiwezi kunyoosha mgongo wake kutokana na migogoro hii; na chini ya hali kama hii Imamu Husein (as) alianzisha uasi na watu hawa wachache wakamuunga mkono na kumsaidia.

Itakumbukwa kwamba nia ya kuanzisha uasi huu ilikuwa yake mwenyewe (as), Yazid alifanya ujinga na alichukua hatua mapema mno kabla haijahitajika kuchukuliwa na yeye. Kulikuwa na kiwango fulani cha utayari mji wa Kufa lakini bado walikuwa hawako katika hali ya kuvumilia shinikizo

hili. Utayari wao unaweza kuonekana katika barua ambazo wamemuandikia Imamu Husein (as) wakimkaribisha mjini Kufa, waliandika barua zilizojaa utajiri wa fasihi, na nyingi ya barua hizo zilikuwa zimetumia maneno "*Al Ajal Al Ajal*," (njoo haraka njoo haraka), na nyingi ya barua hizi zimehifadhiwa na historia hata majina ya wale walioandika barua hizo. Ujumbe na mada ya barua zote hizo ilikuwa ni moja kwamba tuko tayari na tunajiandaa na hatuna kiongozi yeyote na wewe (as) lazima uje upesi. Mwisho wa kila barua kila mtu alitumia maneno "*Al Ajal Al Ajal thummal Ajal*," (njoo upesi sana).

Huu ulikuwa ushahidi wa utayari wao, lakini utayari huu ulikuwa hautoshi kuvumilia shinikizo hili. Ni kawaida kwamba kama jumuiya ikisimama (kuasi) na kujitokeza mbele basi lazima upitie miundo mingi ya mashinikizo. Katika mapigano ya siku 33 ya Hizbullah (2006) ambako msaada mkubwa na ushindi wa dhahiri wa Hizbullah, wachambuzi wamesema kwamba kiwango cha shinikizo ambacho Hizbullah walikipata kilikuwa cha kuvunja mgongo. Shinikizo hili liliwafanya kuwa imara na kuwepo fursa ya kuonesha na kuthibitisha uwezo na uimara wao. Hii hutokea wakati wanakabiliana na adui halisi kuliko maadui wakala, kwani hii hukupa nafasi halisi ya kuthibitisha uwezo wako. Kwa hiyo siku hizi 33 za shinikizo zilikuwa sio za kuvunja mfupa wa mgongo, bali shinikizo ambalo Hizbullah wanalipata sasa ni la kuvunja mgongo. Kama utaangalia Mapinduzi ya Kiislamu katika Iran, huhitaji ari ya hali ya juu ya kuvumilia kumuondoa Shah lakini bado shinikizo hili sio la kulinganishwa na kilele cha shinikizo la leo. Shinikizo kama hilo linajitokeza juu ya nchi yetu (Pakistan) ingawa hatujafanya lolote ambalo lingekuwa ni sababu ya shinikizo. Lakini bado kama ilivyo katika sehemu nyingi nyingine shinikizo linafanywa kwetu vilevile, lakini si jumuiya, umma au viongozi wanaweza kuvumilia shinikizo hili hata kwa dakika tano. Hii ni kwa sababu wakati jumuiya inapokuwa muathirika wa migogoro na ikiwa wamekumbwa kwenye shinikizo hili la kuvunja mgongo huwa vigumu kulivumilia hili.

Watu wa Kufa walijitayarisha kwa kiasi kwamba kama Imamu (as) atafika kwao bila ya vikwazo au pingamizi katika safari yake, basi walikwa tayari kumsaidia kwa hali moja mahususi au muhula. Lakini kama vikwazo au pingamizi fulani kama vile Ubaidullah ibn Ziyad akiingia kati na kutuzuia akaweka vikwazo na kuanza kuwachapa watu viboko na kuwakamata au kwa istilahi za kisasa, mashushu watatufuata, basi tutafanya nini? Tulikuwa hatukujiandaa kwa mazingira haya au mabadiliko ya namna hiyo ya kimuhula. Hivyo muda Ubaidullah alipoingia mjini Kufa, muhula ulibadilika na shinikizo likazidi juu yao, na hawakuweza kuvumilia shinikizo hili hata kwa dakika tano. Kama Imamu (as) angefika Kufa na kwa kiasi fulani akaweza kuwatoa kwenda kwenye uwanja wa mapambano, huenda wangeweza kuvumilia shinikizo la vita, lakini walikuwa hawakujitayarisha kuhimili shinikizo hili la kisaikolojia la kabla na baada ya vita vilivyopiganwa. Wale ambao walijitokeza katika uwanja wa mapambano kwao wao aina hiyo ya utayari na utayarishaji ni lazima na hii haiji kwa kuzaliwa. Utayari huu hauji tu kwa kukaa nyumbani, unahitaji kuandaliwa juu yetu wenyewe na hapa ndio pale uleaji na ufundishaji unapokuwa lazima. Qur'ani Tukufu inatufanya tutembee juu ya njia mbili, moja ni elimu na ya pili ni mafunzo. Elimu hutupa tu utambuzi na taarifa; haimtayarishi mtu kustahimili shinikizo. Sio kwamba kama mtu ana elimu ya hali ya juu basi anaweza kuhimili shinikizo zaidi. Kwa kweli mara nyingi hutokea kinyume chake, mtu ambaye ana elimu zaidi anakuwa laini sana na hawezi hata kuvumilia shinikizo kidogo, wakati ambapo asiye na elimu huenda akavumilia shinikizo zaidi. Sababu yenyewe ni kwamba kustahimili shinikizo kunahitajika malezi, mafundisho, matendo na paredi.

Ni muhimu kufanya juhudi kwenye shinikizo. Hii ina maana kwamba lazima tuende kwenye zile sehemu ambazo zina mashinikizo ili tuweze kujizoesha mashinikizo hayo. Wakati mwingine lazima tukae kwenye sehemu zenye joto kali na kwenye baridi kali ili tupate kuzoea kustahimili shinikizo la joto kali na baridi kali. Wakati mwingine lazima kwa hiari yetu wenyewe tukae na njaa ili tujifunze shinikizo la njaa. Wakati mwingine lazima tutembee ili tuhisi shinikizo la uchovu na kuchoka, wakati

mwingine fanya kazi fulani bila kupata pesa yoyote ili upate kuzoea shinikizo la umasikini. Kama ambavyo imetajwa katika hadithi kwamba umasikini ni hatua ya kuelekea kwenye ukafiri. Hii ni kwa sababu kuna shinikizo kubwa katika umasikini zaidi hata kushinikizwa (kugandamizwa) na jiwe kubwa.

Kama mbingu inamuangukia mtu, anaweza asivunjike, lakini kama mtu anakuwa katika kipindi cha umasikini huvunjika. Walikuwepo watu mashuhuri ambao waliweza kuvumilia shinikizo la panga na kuuawa kishahidi, lakini hawakuweza kuvumilia shinikizo la umasikini. Kwa ajili hii matayarisho na utayari unahitajika; watu wa jumuiya lazima wajiandae na kujifunza wenyewe ili wapate kuvumilia mashinikizo hayo. Hatuwezi kusema wala hatuna ushahidi kwamba wale waliokuwa na Imamu Hasan (as) walikuwa na imani bandia, bali tatizo lao lilikuwa kwamba walikuwa hawajajitayarisha na kuwa tayari kustahimili shinikizo hata kwa muda mfupi. Amiru'l-Muminin (as) alikuwa amepatwa na tatizo kama hilo. Tatizo halikuwa imani ya jumuiya kama tunavyoweza kuona katika *Nahjul Balaghah* kwamba yeye (as) hakuwalaumu katika hali yoyote kwa tabia yao mbaya. Wakati wote alilaumu kujitayarisha kwao na akasema kwamba hamko tayari kukabiliana na mihula minne (ya mwaka), ninyi ni watu wa muhula mmoja tu ule wa majira ya kuchipua, wakati kila kitu ni kizuri na freshi. Wakati kuna usalama na amani kila mahali; huu ndio wakati wanajitokeza uwanjani. Lakini wakati hali ikibadilika na matatizo yakija, basi wanasema kwamba hawakutengenezwa kwa matatizo kama hayo. Hili ndilo ambalo Ali (as) alikuwa akiwaeleza kwamba ninyi sio watu ambao mnaweza kukabiliana na mazingira magumu na matatizo kwa vile hamko tayari na hamkujitayarisha.

Hivyo migogoro huvunja mgongo. Athari kubwa inayoachwa na migogoro juu ya watu ni kwamba hupora utayari wao. Wakati huu hali kama hiyo ipo hapa nchini kwetu (Pakistan). Wakili (mwanasheria) mmoja alikuja Lahore na kulalamika. Kama tujuavyo kwamba ilikuwa ni mawakili tu ndio waliothubutu na kujitokeza katika uwanja. Wakili huyu alikuwa anasema kwam-

ba hatushangai kwa kutopata msaada kutoka kwa wanasiasa kwa vile wakati wote wamekuwa hivyo hivyo, lakini malalamiko na chuki zetu ni dhidi ya watu ambao tunafanya kila kitu kwa ajili yao na bado hawatusaidii. Hawasimami, hawajitokezi na hata msaada kwetu pia hawana. Hili ni kweli lakini swali ni kwa nini hawasaidii, ni msiba gani umeipata jumuiya hii. Hii ni kwa sababu watu wako kwenye shinikizo kubwa; shinikizo la kupata unga, sukari, gesi na umeme. Haya ni mashinikizo ambayo huvunja mgongo na kuwavunja watu mioyo. Kwa makusudi wameitengeneza migogoro hii na kuiweka chini ya shinikizo ili wale ambao wanamudu kuondoka nchini wafanye hivyo na wale watakaobakia wakae kimya ndani ya nyumba zao.

Mwanachuoni mmoja alitoa usuluhisho wa kidini katika kukabiliana na hali hii. Aliwasilisha usuluhisho huu katika namna nzuri sana pamoja na rejea kutoka kwenye Qur'ani Tukufu na hadithi. Anasema kwamba Qur'ani imetaja vitu viwili vyenye sifa sana katika Uislamu. Moja ni uhamaji (*Hijrat*) na nyingine ni kuficha uhalisia wako (*Taqiya*). Huu ni utaalamu kwa baadhi ya watu na makhususi kwa wanachuoni ambao hutoa majina mazuri ya kidini na majina ya vitendo vyao. Kama katika suala hili kutoroka kwa ajili ya hofu hupewa jina la *Hijrat*. Umekuwa ukisikia kwamba baadhi ya Waislamu walikimbia katika vita vya Uhud, hivyo yatupasa vilevile tuwaambie kwamba walifanya *Hijrat*. *Hijrat* katika maana ya kilugha maana yake ni kwamba unaondoka eneo moja ambalo halina usalama na kwenda kwenye eneo lenye usalama. Na kwa vile uwanja wa vita wa Uhud umekuwa sio salama, hivyo waliondoka na kukimbilia milimani, hivyo na wao walifanya *Hijrat*, sasa kwa nini tuwaite kama ambao wamekimbia kutoka kwenye uwanja wa mapambano. *Hijrat* ni kitu tofauti sio kukimbia matatizo. Kukimbia matatizo sio ufumbuzi, jinsi unavyozidi kuyakimbia matatizo ndivyo yanavyozidi kuwa nyuma yako, yatajaribu kukuzunguka kila upande.

Pili amesema ilikuwa ni *taqiya* ambayo pia imepotoshwa maana yake. Taqiya haina maana ya kukaa kimya ndani ya nyumba zenu. Matokeo ya

aina zote za ufumbuzi huu uliowasilishwa ni woga ambao maana yake ni udhaifu na unyonge wa kuhimili mashinikizo. Kwa vile hatuwezi kuvumilia shinikizo basi ufumbuzi ni amma kukimbia au kukaa kimya ndani ya nyumba zetu.

Vilevile wakati wa Imamu Husein (as) baadhi ya watu walitumia mbinu hii kutuliza shinikizo lililowekwa na Yazid. Walikuwa wakimshauri Imamu wakati alipokuwa Madina na Makka afanye kama walivyofanya wao na afuate mbinu yao hiyo. Walimshauri kwamba amma afanye mazungumzo na Yazid badala ya kula kiapo cha utii kwake na kutoka na ufumbuzi kwamba unafanya kazi yako ya dini na muache Yazid afanye kazi yake ya siasa. Usihusike na Yazid wala yeye asiingilie shughuli zako za dini. Kwa njia hii tatizo litakuwa limetatuliwa kwa ajili yako na unaweza kuja Makka na kuchukua hifadhi ndani ya Ka'ba na kujishughulisha na ibada na Hijja. Hizi ndio kauli walizozitoa kumshauri ili kutoka kwenye shinikizo lililojengwa juu ya Imamu (as). Wakati mwingine makhatibu wetu vilevile huyasema haya kwamba Imamu (as) alikuwa anasihi kwamba aachwe na aruhusiwe kwenda Yemen, India au sehemu nyingine. Na watu wa India na Pakistan walijisikia wenye furaha sana kwamba vilevile Imamu (as) alitamani kuja India. Lakini Imamu (as) aliposikia yote haya, alisema:

"اف لهذا الكلام"

"Ole wenu kwa maneno yenu, ole wenu kwa fikra na nia zenu hizo. Mnaangalia kwa njia hii chini ya mazingira haya. Wakati mwingine maadui hawatupi maumivu makali kama haya ukilinganisha na maumivu ya hisia tunayopata kwa kusikiliza mawazo ya mtu aliye chini ya shinikizo, ima kwa mwelekeo wa aina gani na ufumbuzi gani anaofikiria."

Imamu (as) aliumizwa sana na majina yale kwa ajili ya Waislamu ambao walijionesha wenyewe kama mahujaji, lakini kwa mawazo yao walikuwa katika upungufu wa hali ya juu na udhalili, na kwa hiyo Imamu (as) akawalaumu sana. *Hijrat* na *Taqiya* zote hazina maana ya kukimbia au

kujificha, kwa kweli zote hizi ni mbinu mbili zilizopo kwa ajili ya mapambano. Hizi ni mbinu mbili ambazo mtu anaweza kuzifuata wakati mwingine kwa kuzibadilisha katikati yao na sio zana za kupunguzia shinikizo, kwa kukimbia au kujificha sehemu fulani. Wakati huu kama ukiona shinikizo lenye kuvunja mgongo nchini Iran juu ya suala la nyukilia na shinikizo hili huongezwa kila siku, hii ni kwa sababu serikali iliyokuwepo kabla ya hii iliyopo sasa ya Rais Ahmedinajad ilinywea kwenye shinikizo hilo na kwa muda wa miaka mitatu walisimamisha urutubishaji wa nyukilia.

Kutokana na hili wale ambao walikuwa wakitoa shinikizo hili wakapata matumaini kwamba kama tukitoa shinikizo zaidi umma huu utavunjika. Lakini kitu cha kwanza ambacho serikali iliyopo ilifanya baada ya kuingia madarakani ni kuanza kufanya mchakato wa urutubishaji wa nyukilia. Waliamua kwamba hata kama hawapangi au hawakusudii kutengeneza silaha za nyukilia, na hata kama wasipofanikiwa katika malengo ya kurutubisha nyukilia bado hawatanywea kwenye shinikizo katika mazingira yoyote. Matumaini ya maadui siku zote huongezeka wakati wakiona jumuiya inakuja chini ya shinikizo na kutafuta njia za siri za kutoka kwenye shinikizo. Hapo tena maadui hawaiachi jumuiya hiyo, huiandama jumuiya hiyo ili kuipiku na kuitawala kikamilifu. Kwa upande mwingine maadui hukata tamaa kwa jumuiya ambayo hainywei kwenye shinikizo katika hatua yenyewe ya kwanza.

Kuna tukio la shahidi wa mapinduzi ya Kiislamu ambaye alichukuliwa kutoka katika mkusanyiko wa kidini. Mkusanyiko huu ulikuwa mkusanyiko wa kawaida wa waumini, walikuwa wamekaa huku wakisoma tenzi za maombilezo, ulikuwa sio mkusanyiko wa kimapinduzi au wa kisiasa. Mtu huyu alikuwepo katika mkusanyiko huu ambako Polisi waliushambulia na wakamchukua pia mtu huyu. Tukio hili lilikuwa kabla ya Mapinduzi ya Kiislamu na mtu huyu pia alikuwa mwanachuo. Wakati walipomchukua na kumsaili ndani ya chumba kidogo cha magereza, kwa swali la kwanza walimuuliza kwamba yule aliyekuwa akitoa khutba na

kusoma tenzi za maombilezo pale kwenye mkusanyiko ni nani? Yule mtu mwenye kuheshimika alijibu kwamba hamjui mtu huyo aliyekuwa anasoma tenzi za maombilezo, ingawa kila mtu anamjua kwa vile ulikuwa mkusanyiko wa hadhara. Khatibu huyo pia alikuwa mtu mashuhuri ambaye hashughuliki na mambo ya siasa na alikuwa mwanataaluma tu, hivyo ilikuwa hakuna madhara yoyote katika kutaja jina lake. Lakini bado shahidi huyu hata hakulisema.

Waliamua kumpiga na bado hakulitaja jina la khatibu yule, ingawa hata Polisi wanalijua jina lake. Hili lilikuwa ni swali lao la kwanza na alikuwa hawajibu. Waliendelea kumpiga mpaka akazimia, kisha walimwagia maji, alipozindukana wakamuuliza tena swali lile lile, naye alikuwa akitoa jibu lile lile. Walikuwepo baadhi ya rafiki zake ambao alikuwa amefungwa nao, walianza kumlaumu vikali sana kwamba kwa nini unapata kipigo kisicho cha lazima, huu ni upumbavu; waambie tu jina la khatibu yule kwa vile kutakuwa hakuna madhara katika kutoa taarifa hii. Alikataa kwa kuthibitisha kwamba kama nikitoa jibu la swali lao hili la kwanza basi watapatwa na matumaini ya kuniuliza maswali zaidi. Nataka niwakatishe tamaa kwenye hatua ya mwanzo, yaani wasiweke matumaini yoyote kwangu. Pamoja naye wengine walikuwa wanajibu kwa kutaja jina la khatibu yule, jina la mtayarishaji na kwa njia hii waliweza kufikia taarifa muhimu ambazo walitaka kuzipata. Lakini Mujahidina huyu aliwakatisha tamaa katika hatua yenyewe ya mwanzo kabisa kwamba ikiwa mtu huyu hatoi taarifa nyepesi kama hizi hatuwezi kutegemea kwamba atatoa taarifa yoyote muhimu.

Mtu ambaye anaweza kuvumilia shinikizo anaweza kufanya lolote. Mtu anayeweza kuvumilia shinikizo la kisiasa, shinikizo la umasikini, shinikizo la kisaikolojia na kubwa la yote shinikizo la hofu mtu huyu hatasalimu amri kwenye kitu chochote. Imamu Khomein (ra) alikuwa akisema kwamba hakuna kulipa kodi halali kwa askari wanaotisha watu. Watu wa mji kama Karachi wanatambua kinachomaanishwa na kodi halali ambapo mtu anakuja na fimbo au silaha na kuzungumza tu kwa sauti kali mbele ya

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 84



muuza duka na kila wiki muuza duka humpa pesa. Wale waliozoea kunywea kwenye shinikizo kama hili na kulipa kodi hiyo, waliishia katika kutoa pesa nyingi zaidi baadae, hata wanawake wao huenda wakanywea chini ya shinikizo hizi zisizo vumilika. Kama wakati wanapokuja na bunduki na wakataka simu yako ya mkononi na mara utoapo simu hiyo hawaondoki na kukuacha watataka na gari lako pia.

Jumuiya isiyoweza kuvumilia shinikizo hupoteza kila kitu. Imamu Khomein (ra) alikuwa akisema kwamba maadui huweka tu shinikizo; hawana nguvu ya kufanya lolote kwako. Kauli hii ya Imamu Khomein (ra) kwamba "Amerika haina kiasi cha moyo ule na uwezo wa kuchukua hata hatua ya kimakosa dhidi yetu," kosa pekee wanaloweza kufanya ni kutuangusha kwa kutuwekea shinikizo juu yetu, vinginevyo kuja kwa ajili ya kupambana na sisi ni kitu kisichowezekana kwao. Huu ulikuwa ujumbe ambao Imamu Khomein (ra) aliutoa kwa watu wa taifa la Palestina juu ya kifo cha kishahidi cha Shahid Arif Husein. Katika ujumbe wake Imamu Khomein (ra) alisema kwamba ninatamani kwamba Amerika ingekuja kwa uwazi kwa ajili ya mapambano na sisi, wanafanya operesheni ya siri kupitia kwa mawakala wao. Ninatamani kwamba kama Urusi ilivyofanya kwa uwazi dhidi yetu nataka Amerika pia ije katika mapambano ya wazi na sisi. Kwa taifa hili kutaka kupambana pamoja na adui huyu haliwezi kufanywa liwe chini ya shinikizo. Kosa hili lilifanywa na maofisa wa serikali iliyopita ambapo walifuata njia ya kuomba radhi kwa ajili ya suala hili na matokeo yake Iran ikapatwa na mateso mengi mno.

Nguvu za Hizbullah pia ziko chini ya hili; sio kwamba nguvu za Hizbullah ni kwa ajili ya silaha fulani. Hizbullah ina silaha za kawaida ambapo aina ya silaha za kisasa ambazo Israil inazo Hizibullaha hawawezi hata kuota kuwa nazo, lakini bado Israil inawaogopa Hizbullah, kwa nini? Sababu ni kwamba mataifa ya Kiarabu na viongozi wao kwa urahsi wamekuwa chini ya shinikizo, lakini Hizbullah hawanywei kwenye aina au kiwango chochote cha shinikizo. Hata kama nchi yao inateketezwa, watoto na wanawake wao wanauawa kishahidi; mateso yanafanywa juu yao, lakini

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 85



hawanywei chini ya shinikizo lolote; hata lililo dogo. Jumuiya ambazo husalimu amri kwenye shinikizo zimefedheheka mno katika historia kwa sababu kwa kuifanya jumuiya kuwa chini ya shinikizo kunaweza kuwafanya watu wake kufanya kitu chochote unachotaka. Unaweza kuona kwamba umma wa Pakistan leo uko chini ya aina mbali mbali za mashinikizo, shinikizo la kukosa amani, shinikizo la ukosefu wa ajira, shinikizo la ukosefu wa bidhaa muhimu; migogoro ya kisiasa ni shinikizo lingine na mpasuko wa kimadhehebu. Kuna shinikizo kutoka pande zote za jumuiya hii. Kama jumuiya hii itavunja mgongo wake chini ya shinikizo hili, basi kamwe hawawezi kuwa na heshima, hivyo wanahitaji kushinda shinikizo hili na kutoka nje yake.

Tutafanikiwa siku hiyo wakati ulimwengu utakaposhawishika kwamba jumuiya hii haitasalimu amri kwenye aina ya mtindo wowote wa shinikizo. Wanawaita maofisa wetu na wanafukuzana kwenda kwenye ofisi zao, hukaa na wakandamizaji hawa na kupiga picha pamoja nao, na kuona fahari kutembelea Balozi zao. Yote haya ni matokeo ya shinikizo. Mtu mmoja alisema kwamba tunafanya kila linalowezekana kuokoa jumuiya hii, tulikwenda kwa wanasiasa, watu wa dini na sehemu nyingine na sasa hakuna chaguo lililo baki isipokuwa kwamba kwenda Balozi za nje na kuwaambia wafanye mipango kwa ajili ya usalama wa jumuiya ya Shi'a, na kwa mujibu wa kundi hili pia walifanikwa. Balozi fulani zilitangaza kwamba watatoa kinga maalumu kwa Mashia na Makadiani kama wanataka kuondoka nchini kwa muda na kuja kwenye nchi zao. Walitekeleza sera hii kwa muda fulani. Je, hii sio fedheha na udhalili kuomba kwenye Balozi za nje?

Kama nilivyotaja kabla kwamba ni muhimu kuelewa madhumuni ya Karbala, na hicho ndicho ninachomaanisha kusema hapa kwamba shahidi na damu yake hutoa ujumbe kwamba lazima ufe, lakini sio kusalimu amri kwenye shinikizo. Hii ndio tofauti kati ya shingo iliyokatwa na shingo iliyoinama. Shingo iliyokatwa ni ile ya mtu ambaye hakusalimu amri kwenye shinikizo, wakati ambapo shingo iliyoinama ni ile iliyosalimu amri kwenye

shinikizo. Shingo ambayo haiinami hukatwa; hadhi yake, ubora wake na umashuhuri wake uko katika kukatwa shingo, lakini sio kusalimu amri kwenye shinikizo. Huu ndio ujumbe wa watu wa Karbala kwamba kamwe usinywee kwenye shinikizo. Hata kama kuna mtu mmoja tu aliyebakia kuweni wenye nguvu kifikira, iweke imara nyuma shingo yako na amsha ari yako. Hata kama ulimwengu mzima unakushinikiza tangaza kwamba mimi sitakuwa chini ya shinikizo na sitatoa hongo ili kutoka nje ya shinikizo. Ulimwengu huu umejaa wapokeaji hongo, kuna wapokeaji hongo wa kidini, wapokeaji hongo wa kisiasa na kisha kuna wapokeaji hongo wa kiulimwengu kama Pakistan ambayo hutoa hongo kwenye nchi za Magharibi na udhalili kutokana na hili hubebwa na taifa zima.

Shinikizo kama hili hili waliliweka kwenye mataifa mengine na wakakataa kuwapa hongo kwa sababu mara unapowapa hongo basi hiyo inakuwa kigezo kwa vizazi vijavyo. Lakini kama shingo hazisalimu amri na badala yake zikakatwa, basi hupata ujumbe kwamba shingo hizi haziwezi kuwa chini ya shinikizo. Ni jinai gani ambayo kwayo Iraq leo inapatishwa adhabu? Jinai yao ni kwamba walisalimu amri kwenye shinikizo na hawakuweza kuvumilia migogoro ambayo iliwekwa juu yao. Matokeo yake yalikuwa kwamba waliamua kukaa, kuunga mkono na kuchukua msaada kutoka kwa wavamizi hao ambao kabisa ulikuwa hautamaniki na hali za kimatokeo ni hizi zinazoshuhudiwa leo wakati ambapo kila siku takriban maiti mia moja hupatikana. Kama wangeuawa kwa kukataa kuonewa kwenye shinikizo, basi idadi ya vifo ingelikuwa kidogo ukilinganisha na mauaji yanayotokea leo kwa matokeo ya kusalimu amri kwenye shinikizo. Kama ilivyo kauli ya Shahidi kwamba mtu ambaye hasalimu amri kwenye shinikizo hufa mara moja, wakati ambapo wale ambao hunywea kwenye shinikizo hufa mara mia moja kwa siku na kwamba pia ni kifo cha fedheha na udhalili. Kama mtu ana hiari ya kuchagua aina ya kifo basi lazima achague kifo cha Karbala, yaani kifo cha heshima. Tusisahau kwamba kwa hali yoyote tutakufa na kwa vile wameahidi kutuuwa, kwa nini basi tukubali kifo cha kukimbia, kwa nini tusikubali risasi juu ya vifua vyetu kuliko kukimbia. Kwa vile tutakufa, basi kwa nini tufe kizembe,

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 87



badala yake lazima tufe tukiwa katika hali ya kuamka na utambuzi wa lengo.

Imamu Khomein (ra) alisema: "Kama hatima yetu ni kufa basi kwa nini tusife kama Shahidi Mustafa Chamran." Hivyo inathibitishwa kwamba lazima tutakufa, basi kwa nini tufe kwa kisukari, chini ya gari katika ajali, katika hali ya ugonjwa kuliko kifo cha heshima na cha kupendelewa. Hili ni somo la Karbala kwamba Karbala sio uwanja wa mauaji badala yake ni uwanja wa kuwapa watu uhai katika njia iliyo sawa na sahihi. Wakati Kiongozi wa Mashahidi (as) alipoona katika ndoto kwamba msafara huu unaelekea kwenye kifo, alipopanda kwenye mgongo wa ngamia alisema: "Kwa Allah tunatoka na Kwake hatuna budi tutarudi." Mtoto wake Ali Akbar (as) alikuja mbele na kumuuliza sababu ya kusoma aya hiyo. Imamu (as) akasema kwamba nilimuona mjumbe kutoka ulimwengu wa ughaibuni akaniambia katika ndoto yangu kwamba msafara huu unaelekea kwenye kifo na kifo kinakuja kuelekea kwenye msafara huu. Ali Akbar (as) akasema:

"Je, sisi hatuko katika haki?"

Imamu (as) akasema kwamba bila ya shaka sisi tuko kwenye njia iliyonyooka. Ali Akbar (as) akasema kwamba basi haiwi tofauti iwapo kifo kitakuja juu yetu au tunaangukia kwenye kifo. Hili ndilo lililotokea kule Karbala ambako kifo hakikuwajia juu yao badala yake waliangukia juu ya kifo. Ni kanuni ya kawaida kwamba kitu kinachoangukia juu ya kingine hukiuwa. Katika Karbala ilikuwa ni watu hawa ambao waliuwa kifo na kwa kukiangukia kifo nao wakawa hai daima. Ali Akbar (as) bado yungali hai, kifo ndicho kilichoshindwa na kikafa. Kifo hakiwezi kuwauwa Mashahidi wa Karbala. Jumuiya yoyote ambayo ina mfano huu wa Karbala haiwezi kukidhi hadhi yake kwa kuwa chini ya shinikizo na kuanza kutafuta njia za kutokea na kutafuta ufumbuzi mwingine ili kudhibiti mazingira ya shinikizo. Wakati mwingine tunaona kwamba wale ambao hawana Karbala, hawanywei kwenye shikizo, basi vipi wale ambao wana shule,

chuo kikuu na kituo cha mafunzo kama Karbala waweze kuwa chini ya shinikizo? Hii ndiyo njia ya haki, ujumbe na filosofia ya Azadari iliyo sawa. Hii ndio sababu kwamba Maimamu Maasum (as) wametuamrisha kuliweka hai tukio hili la Karbala kwa kufanya Azadari. Ilikuwa ni kuhakikisha kwamba nukta hii ya kuonesha msimamo kwa kutonywea kwenye shinikizo hata kama kutagharimu maisha yetu inabakia hai kama somo na ujumbe kutoka Karbala. Na kama ilivyotajwa kabla kwamba ubora huu wa kuvumilia shinikizo sio ubora wa kuzaliwa, huhitaji kuendelezwa pamoja na juhudi za mwanadamu. Sifa hii ya kutokusalimu amri kwenye shinikizo imetajwa na Qur'ani Tukufu kama "*Istiqamat*" (Msimamo) na sifa hii haiji kwa mtu kutoka kwenye tumbo la uzazi la mama, huhitaji kuendelezwa katika uwanja wa harakati na ujahidina. Elimu ni kitu kinachotamaniwa na bora, lakini kuwa tu na elimu haimaanishi kwamba mtu huyo pia anayo "*Istiqamat*." Tunaona katika mifano mingi ya watu wenye elimu ya hali ya juu, ya dini na ya kisekula, lakini hawana "*Istiqamat*."

"Istiqamat" huandaliwa kwa gwaride katika mazingira magumu. Hata kama umejaaliwa starehe basi vilevile wakati mwingine ingia kwenye maeneo magumu na yenye shida. Wakati mwingine licha ya kuwa na chakula lakini usile na hii nimoja ya falsafa za Saumu kwani huongeza uwezo wa "*Istiqamat*." Umasikini, njaa, kiu vyote hivi ni mashinikizo ambapo kwa kufunga saumu pamoja na chakula kuwepo mtu anaweza kushinda mitihani yote hii. Kwa muda huu tulionao tuko katika aina nyingi za mashinikizo kama tunavyosema kwamba hatuna njia na rasilimali ya kufanya kitu. Wakati mwingine tunafanya kitu bila njia zozote na rasilimali. Tunasema hatuwezi kuja kwa sababu hatuna usafiri, wakati mwingine tunaonesha uvumilivu kwa kutembea umbali mkubwa. Hii ndio njia ya kujithibitisha mwenyewe kwamba haupo katika aina yoyote ya shinikizo. Kama ambavyo utakuwa umeona wanajeshi wamefanywa watembee kwa miguu licha ya kuwepo kwa magari. Hii ni kwa sababu wanatayarishwa na uvumilivu unajengwa ndani yao. Hizi Azadari na Majalis zina madhumuni haya ndani yake. Ingawa zimeumganishwa na

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 89



taratibu nyingine za kiibada na itifaki ambazo pia ni nzuri kuzifanya kama hazivunji Sharia, lakini kiini cha ibada hizi ni madhumuni ambayo hayatufanyi tupotee. Tunaomba kwamba insha-Allah jumuiya ambayo inastahiki maisha ya heshima siku moja itakuwa na "*Istiqamat*" ndani yao na kutoka kwenye mashinikizo yote haya na watu kuishi maisha ya heshima na yenye hadhi kwenye ulimwengu huu kwa njia ambayo Hizibullah wanafanya hivi sasa.

# Khutba ya Mina
# {Imamu Husein (as)}

Enyi watu chukueni somo kutoka kwenye ushauri wa Allah (alioutoa) kwa rafiki zake wakati alipowakemea marabbi kwa kusema:

لَوْلَا يَنْهَاهُمُ ٱلرَّبَّـٰنِيُّونَ وَٱلْأَحْبَارُ عَن قَوْلِهِمُ ٱلْإِثْمَ وَأَكْلِهِمُ ٱلسُّحْتَ ۚ

لَبِئْسَ مَا كَانُوا۟ يَصْنَعُونَ ﴿٦٣﴾

**"Mbona watawa wao na maulamaa wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi na uadui na ulaji wao wa haramu? Hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyafanya." (5:63)**

Na Allah Aza wa Jallah anasema:

لُعِنَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِنۢ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ عَلَىٰ لِسَانِ دَاوُۥدَ وَعِيسَى ٱبْنِ مَرْيَمَ ۚ

ذَٰلِكَ بِمَا عَصَوا۟ وَّكَانُوا۟ يَعْتَدُونَ ﴿٧٨﴾ كَانُوا۟ لَا يَتَنَاهَوْنَ عَن مُّنكَرٍ فَعَلُوهُ ۚ

لَبِئْسَ مَا كَانُوا۟ يَفْعَلُونَ ﴿٧٩﴾

**"Walilaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israil kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryam. Hayo ni kwa sababu waliasi, nao walikuwa wakiruka mipaka. Walikuwa hawakatazani**

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 90



**mambo mabaya waliyokuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu waliyokuwa wakiyafanya.” (5:78-79)**

Allah Aza wa Jallah aliwalaumu kwa sababu waliona kwa macho yao wenyewe wakandamizaji wakitenda uovu na vitendo vya ufisadi, lakini hawakuwazuia kutokana na mapenzi na kwa ajili ya upendeleo wanaopata kutoka kwao halikadhalika na hofu ya kuteswa na kuumizwa. Hata hivyoAllah Aza wa Jallah Anasema:

إِنَّآ أَنزَلۡنَا ٱلتَّوۡرَىٰةَ فِيهَا هُدٗى وَنُورٞۚ يَحۡكُمُ بِهَا ٱلنَّبِيُّونَ ٱلَّذِينَ أَسۡلَمُواْ
لِلَّذِينَ هَادُواْ وَٱلرَّبَّٰنِيُّونَ وَٱلۡأَحۡبَارُ بِمَا ٱسۡتُحۡفِظُواْ مِن كِتَٰبِ ٱللَّهِ
وَكَانُواْ عَلَيۡهِ شُهَدَآءَۚ فَلَا تَخۡشَوُاْ ٱلنَّاسَ وَٱخۡشَوۡنِ وَلَا تَشۡتَرُواْ بِـَٔايَٰتِي
ثَمَنٗا قَلِيلٗاۚ وَمَن لَّمۡ يَحۡكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ٤٤

**“Hakika tuliteremsha Tawrat yenye uongozi na nuru, ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha na watawa na wanazuoni, waliwahukumu mayahudi; kwani walitakiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu.Nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu bali niogopeni mimi. Wala msiuze Aya zangu kwa thamani chache. Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio Makafiri.” (5:44)**

Na anasema:

وَٱلۡمُؤۡمِنُونَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتُ بَعۡضُهُمۡ أَوۡلِيَآءُ بَعۡضٖۚ يَأۡمُرُونَ بِٱلۡمَعۡرُوفِ
وَيَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَيُطِيعُونَ
ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓۚ أُوْلَٰٓئِكَ سَيَرۡحَمُهُمُ ٱللَّهُۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٞ ٧١

**"Na waumini wanaume na waumini wanawake ni mawalii wao kwa wao. Huamrishana mema na kukatazana maovu. Na husimamisha swala. Na hutoa zaka. Na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu mwenye hekima." (9:71)**

Allaha Aza wa Jallah anataja jukumu la kuamrisha mema na kukataza maovu (*Al-amr bi al-ma'ruf wa al-nahy al-munkar*) kabla ya majukumu yote kwa sababu anajua kwamba kama linatekelezwa na kuimarishwa katika jamii, majukumu mengine yote mepesi na magumu yataimarishwa. Sababu yake ni kwamba '*Amr bi al-ma'ruf wa nahy al-munka'* humaanisha kulingania watu kwenye Uislamu, halikadhalika upinzani dhidi ya dhulma, kupinga na kupambana dhidi ya wakamdamizaji na kufanya juhudi kuhakikisha kwamba utajiri na mapato yanayopatikana kutokana na vita yanagawanywa kwa mujibu wa sheria za Kiislamu na kwamba kodi inakusanywa, inatumika na kutumiwa katika mfumo wa haki na kwa usahihi.

Enyi wanachuoni ambao mnafurahia na kufaidi sifa nzuri kwa sababu ya elimu yenu! Mmepata jina zuri katika jamii kwa sababu ya nia yenu nzuri. Ni kwa sababu ya Allah kwamba watu wanawaheshimu na kuwastahi sana, na kwamba hata wenye nguvu wanakuogopeni na wenyewe wanakuheshimuni na wale ambao hawapasiki na ninyi na kwa wale ambao hamna mamlaka nao wanakupeni upendeleo wanaojinyima wenyewe. Wakati watu hawapati haki zao, wanatafuta utetezi wenu, ninyi mnatembea mitaani kwa nguvu za wafalme na za malkia.

Je hamkupa heshima yote hii na sifa kwa sababu ya matumaini ya watu kwamba mtazitekeleza sheria za Mwenyezi Mungu? Hata hivyo katika mifano mingi mmeshindwa kufanya hivyo.

Ninyi kama viongozi mmeyachukulia majukumu yenu kwa wepesi sana. Mmepuuza haki za wenye kukandamizwa na za walio chini, lakini kwa uangalifu mmeshughulikia kile mnachokiona kama haki zenu binafsi.

Hamkutumia pesa zenu au kuhatarisha maisha yenu kwa ajili ya Yule Aliyewapa uhai, wala hamkupigana dhidi ya kundi lolote au kabila kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo mnatamani – na mnaona hiyo haki yenu – kwamba Yeye (Allah) lazima awape Pepo kwa pamoja na Mtume (s.a.w.w.) na kinga kutokana na adhabu ya Akhera. Mnayo matumaini kama hayo kwa Mungu, nina wasi wasi kwamba uzito uliojaa ghadhabu Yake unashuka juu yenu, kwani ingawa ni kwa uwezo na utukufu Wake kwamba mmepata cheo cha juu, hamuoneshi heshima kwa wale ambao kwa kweli wanamjua Mwenyezi Mungu, ambapo ninyi wenyewe mnafaidi heshima miongoni mwa viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa sababu Yake.

{Pia nina wasiwasi nanyi kwa sababu nyingine}. Mnaona mktaba uliowekwa na Mungu unavyovunjwa na kukanyagwa chini ya miguu, bado ninyi hamuoneshi wasiwasi, wakati ikija kwenye mikataba iliyowekwa na baba zenu ikivunjwa sehemu yake tu mnachanganyikiwa sana na kuwa na wasi wasi mkubwa, lakini ahadi mlizotoa kwa Mutuku Mtume (s.a.w.w.) ni suala la tofauti kabisa kwenu.

Vipofu, mabubu na wenye magonjwa sugu kila mahali wanakosa hifadhi katika miji na hakuna huruma inayooneshwa kwao. Lakini kamwe hamtendi kwa mujibu wa shughuli zenu na vyeo vyenu, wala hamuwasaidii wala kuwalipa wale ambao wanafanya shughuli hizo, mnanunua usalama wenu kutoka mamlaka kandamizi zenye nguvu pamoja na sifa za uwongo za kupachikana na maafikiano. Shughuli zote hizi zimekatazwa kwenu na Mwenyezi Mungu, na zaidi sana Amewaamrisha kukatazana wenyewe kwa wenyewe kujihusisha nazo, lakini hamzingatii.

Msiba uliowapata ni mkubwa kuliko ule ambao umewapata wengine, kwani hadhi halisi na kiwango cha “Umma” kimeporwa kutoka kwenu. Utawala wa nchi na utoaji wa sheria na hukumu, kwa hakika lazima vikabidhiwe kwa wanachuoni wa kidini ambao ni walinzi wa amri za Mwenyezi Mungu kuhusiana na kipi kinaruhusiwa na kipi kinakatazwa.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 93



Lakini nafasi yenu hiyo imeporwa kutoka kwenu, kwani hakuna sababu nyingine ila ni kwamba mmeitupa haki, na mmehitilafiana kuhusu asili ya Sunnah, licha ya kuwepo ushahidi wa wazi.

Leo mngekuwa na uvumilivu wa kuhimili dhiki na shida kwa ajili ya Allah Aza wa Jallah basi taratibu zote zilizokusudiwa (mambo wa Mungu) zingeletwa kwenu kwa ajili ya kuzithibitisha na kwa ajili ya ninyi kuzitoa kwa watu; mamlaka yangekuwa mikononi mwenu. Lakini mmewaruhusu wakandamizaji kupora shughuli zenu, na mambo ya Mungu (serikali) yakaangukia mikononi mwao, hivyo kwamba wanayaendesha mambo kwa utata na kufanya mambo kiholela na kwa ajili ya kukidhi matamanio yao, mwenendo wa desturi. Kilichowawezesha kupata udhibiti wa serikali ni kutokana na ninyi kukimbia kwa hofu ya kifo na mapenzi yenu juu ya ulimwengu na maisha ambayo kwa hali yoyote ile yatakutokeni. Kwa matokeo ya fikra hiyo mmeutoa umma huu usio na nguvu na kuukabidhi kwenye makucha ya wakandamizaji. Ambapo baadhi wamejikunyata kama watumwa chini ya himaya ya wakandamizaji hao, na wengine wamefanywa mafukara kuhusiana na maisha yao, watawala wanaendesha mambo ya serikali kulingana na matakwa yao, huku wakipata aibu na fedheha kwa ajili yao wenyewe pamoja na ufisadi wao, huku wakiwafuata washauri waovu na kuonesha ufedhuli kwa Mwenyezi Mungu. Mmoja wa wazungumzaji wao mteule hupanda kwenye mimbari katika kila mji. Nchi haina ulinzi mbele yao na mikono yao hupora kila kitu watakacho bila kizuizi. Watu ni watumwa wao na hawana nguvu ya kujilinda wenyewe. Mmoja wa magavana ni dikteta kwa asili, habithi na mwenye chuki ya muda mrefu, mwingine huzuia kutambuliwa kwa Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho! Sio ajabu – vipi mtu afikirie ni ajabu, jamii ile ni mfumbato wa wakandamizaji wajanja ambao magavana wao hawahisi upendo na huruma kwa waumini walio chini ya mamlaka (yao).

Mungu Ndiye Atakayehukumu kuhusu kile ambacho ni mgogoro miongoni mwetu na kutoa hukumu ya kuamua kuhusiana na yote ambayo hutokea miongoni mwetu.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 94



Ee Allah! Unajua kwamba kila kitu tulichofanya hakikushawishiwa kwa upinzani kwa ajili ya kutaka nguvu za kisiasa, wala si kwa kutafuta utajiri na wingi wa mali, bali kimefanywa kuonesha watu kanuni na maadili ya dini Yako yanayong'ara ili kutengeneza mambo ya nchi Yako, kulinda na kuhifadhi haki za msingi za waja Wako wanaokandamizwa na kutenda kwa mujibu wa majukumu ambayo umeyaweka, kaida, sheria na amri ulizohukumia.

Hivyo, (enyi wanachuoni wa dini) mnatakiwa kutusaidia ili tufikie lengo hili, ili turejeshe hali zetu kutoka kwa hao wenye nguvu hizo ambao wanaona inakubalika kuwakosea ninyi na ambao wanajaribu kuzima mwanga wa taa iliyowekwa na Mtume (s.a.w.w.). Allaha Aza wa Jallah anatosha, Kwake tunategemea na Kwake Yeye tutarejea.

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 95



# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 96



25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 97



56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 98



85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 99



112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya

Azadari ( Bi. Zainab) final Lubumba.qxd 7/1/2011 12:32 PM Page 100



138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Tatu
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Elimu ya Ghaibu
152. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.1
153. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.2
154. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.3
155. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza

# Back Cover

Maana ya *azadari* – ni kuomboleza. Kiistilahi, ni mkusanyiko wa watu wanaokusanyika sehemu moja iliyoandaliwa kwa ajili ya kumbukumbu na kuomboleza ushahidi, hasa wa Imam Husain AS (‘***A****layhi ‘s-****S****alaam*: amani iwe juu yake). Katika mkusanyiko huo (ambao ni maarufu kwa jina la “majlis”) hutolewa hutuba za kuwahamasisha waumini kuendeleza harakati aliyoianzisha Imam Husain AS ya kupambana dhidi ya watawala madhalimu na mafisadi ambao ni kikwazo cha maendeleo na ustawi wa jamii. Mwanzilishi wa azadari hii ni dada yake Imam Husain, yaani Bibi Zainab AS, ambaye alitoa hutuba ya kwanza kabisa kuhusu masaibu ya Karbala mbele ya mkusanyiko mkubwa wa watu katika baraza ya Yazid na mbele ya Yazid mwenyewe. Kwa ujasiri mkubwa alitoa hutuba ambayo iliuliza umati ule wa watu waliokuwepo pale kiasi kwamba hata Yazid mwenyewe alinywea na kutahayari. Na kutokana na hutuba hii kali, Yazid aliamuru wafungwa hawa akiwemo Bibi Zainab na mdogo wake Ummu Kulthum, Imam Ali Zainul Abidin (Sajjad) mwana wa Imam Husain AS na kina mama wa familia za mashahidi wa Karbala, wafunguliwe minyororo waliyofungwa na watayarishiwe safari ya kurudi Madina.

Kitabu hiki ni johari nyingine na ni kazi ambayo haiishii kwa Mashia tu, bali ni kitabu cha *Ummah* wote wa Kiislamu, na kwa kweli kwa wale wanadamu wote ambao wana maadili fulani yaliyo hai ndani yao.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info